

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, BAHARI
CONSTITUENCY HELD AT KILIFI INSTITUTE OF AGRICULTURE**

ON

9th OCTOBER 2002

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

DISSEMINATION AND DRAFT REPORT OF COAST PROVINCE – BAHARI CONSTITUENCY AT KILIFI

INSTITUTE OF AGRICULTURE

HELD ON 9th OCTOBER 2002

Present

1. Com. Swazuri Mohammed

Secretariat Staff In Attendance

- | | | | |
|----|-------------|---|-------------------------|
| 1. | Nuru Awadhi | - | Asst. Programme Officer |
| 2. | Lydia Moraa | - | Verbatim Recorder |

Meeting started at 10:19 am

David Mwaringa: Hawa wakazi wa Kilifi ninawasalamia. Mmeamkaje?

Audience: Hatujambo.

Mwaringa: Naam nafikiri sasa tuko hapa kama mlipopata matangazo kwamba kuna marekebisho ya katiba, kuja hapa kuleta ule mswada ambao ulikuwa umeshughulukiwa. Lakini zaidi tutazungumza, ningetaka tufungue mkutano huu kwa maombi na tutafungua kwa maombi. Chairman wetu hapa wa 3C Bwana Daniel Mwangome tuombe, halafu jioni tukifunga, tutafunga kwa maombi ya Kiislamu. Kwa hivyo tafadhali Bwana Mwangome tuongoze kwa maombi.

Mwangome: Funga macho tuombe. Baba wa mbinguni katika jina la Bwana Yesu Kristo, Jehova mungu baba tunashukuru tunasema asante mungu wetu kwa jinsi ulivyokuwa mwema na mwaminifu umetuwezesha kutusafirisha salama kutoka majumbani kwetu, ili tuje tukutane hapa kwa ajili ya kongamano hii ambayo ni manufaa kwetu na kwa vizazi vijavyo. Baba ulibariki kongamano hili ili kwamba lolote ambalo litakuwa likizungumzwa ama kuletwa kama mswada, mungu wetu ukatusaidie na likaweze kutusaidia katika maisha yetu na zaidi upande wa Kenya nzima baba tunaomba tukiamini utaenda kutusaidia na kutubariki. Ni katika jina tukufu la mwanao Yesu Kristo, bwana na mwokozi wetu tumeomba na kushukuru, Amen.

Audience: Amen.

Mwaringa: Naam nataka niwajulishe, nilikuwa nataka sasa nichukue fursa hii niwajulishe wale waliokuja kutoka kwa tume ya

marekebisha ya katiba. Hapa tuko na commissioner wetu, Dr. Mohammed Swazuri ambaye ndiye atakaye tuzungumzia kuhusu mswada huu. Atatuelezea ili tuweze na sisi kuchangia, Dr. Mohammed Swazuri ndiyo huyu hapa tuko pia na Assistant Program Officer, Nuru Awali pia yuko hapa kunakili yale yote ambayo yatazungumzwa atayatia katika record katika hali ya kuandika ili hata akifika kule pia mkutano huu uwe na record yake. Hapa niko na huyu Lydia Moraa ambaye pia anatoka huko yeye anafanya recording kama hivi unamuona ile sauti yoyote ambayo iko hapa, lolote ambalo linazungumziwa pia litachukuliwa ili kuwekwa kwa maktaba yetu. Mimi ni district coordinator wenu, Daniel Mwaringa na upande ule pia tuko na Esther Mbagwa ambaye wanafanya registration na kijana wetu wa ofisi David Kayi. Iwapo mtakuwa na matatizo yoyote mkija kwa ofisi yetu hapa Kilifi County Council hapa ofisi namba 28 ya Constitution of Kenya Review Commission, iwapo pengine sipo niko field, David Kayi anawahudumia wakati wowote.

Madhumuni ya sisi kukutana hapa leo pengine mmekuwa mkijua yale mambo yanayoendelea kwetu nchini hasa kulingana ama kuhusiana na marekebisha ya katiba. Tulikuja nakumbuka wakati fulani ilikuwa sijui ni tarehe ngapi, lakini mwezi wa nne tukaja tukatoa maoni yetu, sivyo?

Audience: Ndivyo.

Mwaringa: Na ni hapa hapa tulitoa maoni yetu, na katika kuchukua maoni yale katika sehemu za wakilishi bungeni mia mbili na kumi ma-commissioner wetu waliweza kukaa na kuwasanya yale yote yaliyozungumzwa na kuyaweka katika mswada ambao uko mbele yenu leo.

Sasa hii ama huu ni mwanzo, utafanywa official launch katika constituency yetu hii ya Bahari. Halafu tutajadiliana mawili, matatu ama zaidi kuchangia mtauliza maswali kisha utakuwa ndiyo mwanzo kwa sababu tutafanya mikutano mingine kadha ili tujadiliane ili kuhusu mambo ambayo yamo humo, ambayo pengine hayafurahishi ama pengine yanatatanisha kidogo. Ama pengine mambo yaliyokufurahisha pia unazidi kusema hili mimi nalitilia mkazo. Baada ya hapa tutakwenda kwa hile National Constitutional Conference ambayo itafanyika kwa muda wa siku thelathini hivi.

Tayari tulifanya elections na tukapata wajumbe wetu watatu ambao watakuwa wanawakilisha district nzima ya Kilifi. Lakini wajumbe hawa lazima waende kule na maoni ya wananchi kutoka kwa zile sehemu za wakilishi bungeni ndiyo sababu lazima tuwe na vikao kama hivi. Kwa hivyo leo commissioner wetu akishaipitia huu mswada, mnaweza kuuliza maswali, mnaweza kuchangia, mnaweza kusema mbona jambo fulani tulilizungumiza hatulioni katika mswada wetu, pengine limeandikwa katika lugha ingine ambapo linajitokeza. Lakini unalalamika ama kupata shida kulielewa, kwa hiyo leo mkutano huu ni wetu sote tuwe watulivu wavumilivu tupate kusikiliza ili tupate ile Kenya ambayo tunaitaka.

Nafikiri Bwana Commissioner wetu Mohammed Swazuri nitakualika sasa uzungumze na wananchi.

Com. Swazuri: Habari ya asubuhi?

Audience: Salama.

Com. Swazuri: Kama alivyosema Bwana Coordinator tuliahidi kwamba tutarudi na mswada wa katiba, ili tuje tuwapatie halafu muangalie tuzungumze na tumetimiza ahadi yetu. Juzi tulikuwa Kaloleni Social Hall, jana tulikuwa Ganze na leo tuko hapa ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaangalia yale matunda yetu tuliyoyaleta halafu wajadiliane kama kuna makosa watatuambia, kama kuna usawa pia watatuambia, kama kuna kitu kimeachwa nje ambacho hakipo pia watatuambia na maneno kama hayo. Madhumuni yake ni kwamba baada ya hapa tuwe tumeridhika kwamba katiba ambayo tutaipitisha itakuwa ni ile ambayo tunaitaka. Kwa hivyo, wale ambao wamepata hizo nakala na wale ambao hawajapata, watapata. Mpaka sasa hatuna ili ambayo iko kwa lugha ya Kiswahili. Mimi huona watu wengi ambao wanachukuwa wengine, wanasema hawaelewi Kiingereza lakini bado wanachukua hivyo hivyo, tutawaletea bado zile za Kiswahili lakini bado tafsiri inaendelea haijamalizika.

Ningependa kwanza kueleza yale maneno ambayo ni mpya katika hii katiba ya sasa. Katika huu mswada ambao tumependekeza, nataka kuzungumzia yale maneno ambayo hata ukiangalia kwa kifupi ni mapya, hayamo katika ile katiba ya zamani halafu ndiyo tuangalia yale ya zamani na sasa tumechanganya, tumepata nini.

Kwanza katiba ya sasa ina utangulizi na ile ya zamani ilikuwa haina, hilo ni jambo jipya ambalo tumeliweka katika katiba. Mtauangalia utangulizi huo, msemi kama unafaa au haufai ama ufanyiwe marekebisho namna gani.

Neno jipya la pili tumesema ni kwamba katiba hii imetengenezwa na wananchi wenyewe sio katiba ya kutengenezwa na watu wadogo wale ambao walikuwa na fursa na nafasi na nia ya kuchangia, tuliwapatia nafasi katika mijadala yetu mingi mihadhako yetu mingi na maoni yao yote tumekusanya tukayachunguza na tukaonelea ni hivyo. Kwa hivyo hii ni katiba ambayo imetengenezwa na wananchi na tumeipatia nguvu kwamba wale wanaotekeleza ni wananchi ambao watakuwa na jukumu la kubadilisha ni wananchi. Hilo ni neno jipya ambalo kwenye katiba hii ya sasa halipo. Katiba ya sasa inabadilishwa na bunge peke yake.

Neno jingine jipya, kama husikii basi sijui nitasema vipi. Neno jingine jipya, tafadhali ungeniacha nikazungumza halafu utasema maoni yako tafadhali. Neno jingine jipya ambalo tumeweka kwenye katiba hii ni kwamba haki za kimsingi, haki za binadamu ambazo zilikuwa zimetajwa tu kwa ufupi katika katiba ya sasa, tumezitia katika kwa urefu zaidi nimezieleza kwa urefu zaidi na ndiyo katiba yote hapa ukiangalia ina sehemu nyingi sana ambazo ni za kuhusu haki za kimsingi, haki za kijamii ili neno jipya katika katiba ya zamani halikutiliwa umuhimu sana.

Neno jingine ambalo ni jipya katika katiba ya sasa, tumesema kwamba bunge litakuwa na sehemu mbili; litakuwa na Lower House, ya wale wabunge wa kawaida mia mbili na kumi halafu kutakuwa na Upper House ya wajumbe ambao watakuwa

wajumbe waakilishi. Hilo neno jingine ambalo ni jipya, tutaeleza watakuwa wangapi, watachaguliwa namna gani. Neno jingine jipya pia ambalo tumelitia kwenye katiba ya sasa ni kwamba tumelipatia nguvu sana bunge. Bunge limepewa nguvu ya kuamua mambo mengi sana ambayo zamani yalikuwa ya kuamuliwa na ofisi moja au mbili. Sasa yamefanywa kuwa yatakuwa mambo ya kuambuliwa na bunge. Kwa hivyo nguvu zake ni nyingi na tumefanya bunge liwe kidogo independent na executive, lisiwe linashurutishwa na wale wakuu wa nchi.

Halafu, neno jingine jipya tumependekeza si lazima mtu awe mwanchama wa chama wa kisiasa ndiyo apiganie uongozi, independent candidates wamekubaliwa, sio lazima. Kwa hivyo kama umekatazwa chama fulani kwa sababu fulani na wewe una hakika mwenyewe nikipigania nitashinda, iko nafasi sasa ya kwenda kufanya campaign yako na ukachaguliwa. Neno jingine jipya ni kwamba vyama vya kisiasa, tumevipatia kazi maalum sasa kazi zao tumeziandika sio ile kazi ya kungojea wakati wa kura, campaign ndiyo ujue chama cha kisiasa kiko. Tumesema vyama vya kisiasa kazi zao tunaziandika wahusike katika maendeleo, civic education, kueleemisha wananchi hizo kazi tumeshaziandika. Na kama chama cha kisiasa hakifanyi kazi zake hivyo, basi hakitasajiliwa au hakitaruhusiwa kupigania kwenye uchaguzi, kwa sababu ya hizo kazi zake ziko pia tumesema vyama vya kisiasa vitapatiwa pesa za serikali kuendesha shughuli zao. (*clapping*).

Neno jingine jipya tumeeleza katika katiba hii, wabunge hawakuwa na uwezo wa kupanga mishahara yao.(clapping). Wabunge hawatakuwa na uwezo wa kupanga mishahara yao. Viongozi wote wa uma na wale wakuu wa mashiriki ya serikali, mishahara yao tumeipangia tume independent kabisa, ambayo iko na wananchi ambao wataangalia mishahara yao. Jambo jingine jipya tumesema katika katiba hii ni kwamba, iwapo kiongozi aliyechaguliwa mbunge au councillor hafanyi kazi yake au rais au waziri mkuu, wananchi wana ruhusa ya kumtoa (clapping). Tumesema pia neno jipya katika katiba hii viongozi wote wa uma wale waliochaguliwa, walioteuliwa kuna sheria ya leadership code yaani maongozi ya viongozi, tumeyaweka pale kwanza lazima haswa kwa wale wa juu sana ni lazima waeleze pesa, mali zao walizipata vipi ndiyo waweze kuingia kwenye uchaguzi (clapping).

Pia neno jingine jipya tumesema, rais wa nchi hii atachaguliwa kwa wingi wa asilimia hamsini ya kura zote halafu apate asilimia ishirini katika mikoa mitano au zaidi katika jamhuri yetu. Endapo watakuwa haja wale wapiganiaji hakuna yule ambaye hajapata hiyo basi yule wa kwanza na wa pili wataenda kwa runoff wao wawili (clapping). Jambo jingine jipya tumesema, nguvu za ofisi ya rais tumezipunguza kwa hivi sisi rais atakuwa ni mkubwa wa nchi kazi zake tumezipanga tumeandika haswa ya kwanza ni hii ya pili ni hii ya tatu ni hii na akiwa atafanya kazi ambayo siyo hiyo ama ruhusa ya kushitakiwa hiyo tumezipeleka sasa kama nilivyosema mwanzo kutangulia nimesema tumezipeleka kwa bunge kwa mfano uteuzi na ufutaji kazi wa watu viongozi sasa si wa rais. Uteuzi ni wake atasema fulani nataka awe kiongozi fulani nataka awe kiongozi fulani lakini mwisho watakao amua ni wabunge. Fulani simtaki nataka afutwe mpaka apeleke akaomba kule bunge wabunge fulani simtaki nataka afutwe mpaka apeleke akaombe kule bunge wabunge wajaadiliane wakipitisha kwa asilimia sitini na tano au thuluthi mbili ndiyo yule awezwe kufutwa (clapping).

Jambo jingine jipya tumetia katika katiba hii, tumetaka waziri mkuu. Waziri mkuu atakuwa ni mbunge, wabunge tutawachagua wale mia mbili na kumi au mia tatu kuna wengine tisaini ambao nitaeleza baadaye, tutawachagua halafu kile chama ambacho kiko na wabunge wengi ndiyo kitatoa waziri mkuu na waziri mkuu huyu pia kazi zake pia tumeziandika. Pia ,safari hii kazi ya makamu wa rais ambayo ni ofisi ambayo haijulikani kazi zake, yuwategemea kazi ambazo ataambiwa na rais. Safari hii hata yeye tumemwandikia zake atafanya kitu gani. Halafu jambo jingine jipya tumesema mawaziri hawatakuwa wabunge (clapping). Mawaziri hawatakuwa wabunge na tumesema ni lazima wawe ni watu ambao wana ujuzi katika ile wizara wanayofanya (clapping).

Audience: Ndiyo

Com. Swazuri: Kwa hivyo itabidi watu wachague kama unataka kuwa mbunge utakuwa mbunge tu, kama unataka kuwa waziri hautapigania, utangojea ukiteuliwa watu watajadiliana, bunge litajadiliana kama unafaa utapitishwa wewe ndiyo waziri. Wakitakikana kwenda bunge wataitwa tu na wabunge kwamba tuna swala la mambo ya barabara hapa mwiteni waziri wa barabara aje bunge atueleze amefanya nini au kumekosekana nini au anataka pesa ngapi.

Jambo jingine jipya ambalo tumeliandika hapa, tumesema hata waziri mkuu, rais, waziri wa wizara wanaweza kuondolewa na kushitakiwa kazini ikiwa wanafanya makosa. Halafu hizo wizara tumesema ni lazima ziwe kumi na tano peke yake. Zisizidi kumi na tano, na mawaziri ni waziri mmoja kwa kila wizara kwa hivyo mawaziri pia ni kumi na tano manabu wao pia ni moja moja kumi na tano.

Neno jingine jipya tumesema kwamba serikali, wananchi wamelalamika kuhusu serikali ya unitary ya Nairobi peke yake tumesema sasa serikali nguvu za serikali ya centre pale tumeziondoa na tumepeleka serikali mashinani. Kwa hivyo tuko na serikali ya centre pale ya unitary ya Nairobi mji mkuu utakuwa ni Nairobi. Tuko na serikali ya majimbo, wilaya na tuko na serikali ya kijiji (clapping). Tutaeleza serikali hizo zitateuliwa au kuchaguliwa namna gani. Tumesema pia kuwa provincial administration imeondolewa (clapping). Katika upande wa mahakamani tumesema tutakuwa na Supreme Court, yaani ile mahakama ya juu kabisa kushinda Court of Appeal, maanake wananchi walilalamika kwamba ukifika Court of Appeal umefika mwisho, umepiga ukuta pale hujui uende wapi, hata kama uamuzi ni kwa kiholela lakini wamaonevu lakini ni mwisho sasa tunaweka ngazi moja zaidi (clapping).

Upande wa Kadhi tumesema tumezipanua, tumeziweka nyingi tumesema ziwe za chini ziwe wilaya za province halafu ile ya Chief Kadhi itakuweco. Halafu tumesema pia Chief Kadhi kwa vile ni mkuu wa waislamu atachaguliwa na waislamu wenyewe (clapping). Neno jingine jipya tumesema ma-judge wote, mahakimu wote watachaguliwa na bunge (clapping). Halafu kutakuwa na tume ambayo kazi yake ni kusikiliza mashtaka ya wananchi juu ya viongozi wa uma ambao wanawakosea (clapping). Tumerekebisha sana upande wa polisi, sababu malalamiko yalikuwa ni kwamba polisi wanadhulumu wananchi, wanafanyia mambo ambayo hayafai sasa tumeweka sheria kwamba wawe ni watumishi kabisa na kazi zao tumeziandika. Kama hatafanya

atakuambia kazi ambayo sio yake una ruhusa ya kwenda kumshitaki polisi yule.

Upande wa ardhi tumesema kwamba tutaondoa ofisi ya commissioner of lands na tumechagua tume ya kitaifa, National Land Commission ambayo itakuwa na ofisi zake mpaka huko chini mashinani hiyo ndiyo itaangalia maswala ya mashamba (clapping). Halafu tumesema ardhi ya mtu binafsi tumesema ni ipi? Kuna ardhi ya mtu binafsi tumesema ni ipi na halafu kuna ardhi ambayo tumeita ni community ile trust land yote tumeota kwa county council tumeipatia wananchi wao wananchi wenyewe (clapping). Wananchi wenyewe wataamua watamiliki vipi ardhi ile, watapeana vipi, wataitumia vipi, wataganya vipi wakikosea ni shauri yao (clapping).

Halafu tumesema pia katika ardhi wageni wote ambao sio raia wa Kenya hawatamiliki ardhi tena (clapping). Yule ambaye tutampatia ardhi ambaye si mkenya, atapewa lease ambayo haitazidi miaka tisaini na tisa basi lakini kwamba ni yake absolute ownership hakuna kwa wageni (clapping). Hayo ndiyo maneno ambayo ni mapya ambayo tunakuta kwamba, kulikuwa ni kilio cha wananchi kwa hivyo tumeweka vile vile ambavyo mlitaka tumeweka hivyo sasa akiwa kuna zaidi ya hapo mtasema nyinyi wenyewe. Sasa tukiangalia katiba yenyewe kwa ujumla wale ambao wako na hizo nakala mtaona kwamba tuko na sura karibu ishirini na tuko na article, sections, vipengele karibu mia tatu katika katiba yetu hii.

Jambo la kwanza tunasema ya kwamba wananchi walilalamika kwamba katiba ya sasa iko na lugha ya kisheria mno, kama haujui sheria huwezi kuelewa na hata wanasheria wenyewe wamelalamika kwamba maneno mengine hawayaelewi kwa hivyo tumeifanya hii lugha ya sasa rahisi kwa mtu yeyote ambaye ajua kingereza ataweza kuelewa. Kwa hivyo katika msururu wa hivi vipengele ambayo mnaviona hapa, ukianza sura ya kwanza tumeweka kwamba umuhimu wa wananchi, wananchi ndiyo wanakuja kwanza katika taifa hili, wananchi ndiyo waamuzi wa mambo yote katika taifa hili.

Tumeweka katika sura ya kwanza supremacy and sovereignty of the people ni wananchi wa Kenya ndiyo watu wa kwanza kuamua mambo kuhusu Kenya siyo viongozi tena. Tumetaja pia kwamba katiba ndiyo sheria kuu ambayo itatumika katika nchi ya Kenya. Halafu pia tumeleza katika katiba, Kenya ni ipi ukisema eneo la Kenya ni wapa hasa kwa hivyo tumeindika ni map ambayo hatajailita lakini pia tumeindika ile ramani ya Kenya iko vipi kidikoni iko wapi ukifuatafuata basi mpaka wa Kenya utaupata sababu tulikuwa na shida sehemu ambazo tunapakana na nchi jirani, kwamba watu hawajui mpaka wao ni upi kwa hivyo huu pia tumeutia katika katiba sasa. Kwa hivyo tukienda kama tunapigania na mtu sasa tunajua kwa nini tunapigana na mtu kama tumesema amechukua ardhi yetu.

Lugha tumesema lugha ya kitaifa sasa ni kiswahili ndiyo lugha ya kitaifa (clapping). Halafu tukaja kwenye siku za sherehe tumependekeza kulingana na maoni ya wananchi kwamba siku za sherehe za kitaifa zitakuwa tatu; Madaraka Day, Jamhuri Day tarehe 12 December, na Katiba Day siku ile katiba itakapopitishwa tukasema hiyo iwekwe siku kuu yake (clapping).

Halafu katika sura ya tatu tunaeleza maadili ya wananchi wa Kenya ni mambo gani ambayo sisi wananchi wa-Kenya tunataka

tuyajue kwamba kila mtu akisema kwamba huyu ni Mkenya anafuata mambo yale tumeweka pale, usawa wa kila mtu yuko sawa mbele ya sheria. Sote tu Wakenya, hakuna kubaguwana, sote tuko sawa no one is above the law. Hakuna mtu ambaye sheria atakuwa yeye anajifanya ni mkubwa zaidi kuliko mwenzake. Hakuna mambo kama hayo na mambo yetu yote tunafanya open transparent. Hakuna siri kila kitu kinafanywa open transparent, madili yetu ni kwamba kuna demokrasia katika Kenya, kura zetu ni za siri za kuchagua hakuna kura ya mlolongo sasa kura zote ni za siri ili mtu asijulikane amemupendekeza nani wala nani (clapping).

Tumesema pia katika madini yetu hongo, corruption sasa ni hatia kwa mtu yeyote anayechukua, anayetoa, anayetumia, anayeeneleza hao wote wako katika upande wa corruption tumesema sasa ni hatia na sheria ipo ambayo itakushitaki.

Upande wa raia tumetaja pale sifa za mtu kwa raia wa Kenya, hapo ni sasa sawa pamoja na yale zilizoko sasa tumeongeza zaidi, na neno jipya kabisa pale ni kwamba kuna watu amabo wametaka kura na uraia mara mbili kwa sababu ambazo tulizifikira kweli hawa wako na sababu muhimu. Kwa hivyo tumetoa nafasi mtu aweza kuwa na uraia wa Kenya na wa nchi ingine lakini tukatia kikwazo, ikiwa atafanya vitendo fulani basi automatically uraia wa Kenya ataupitiza na ataenda ile nchi nyingine.

Halafu tukasema sasa Bill of Rights yaani haki za binadamu, haki za kimsingi nimesema hizi ndizo zimedominant zimekuwa ndiyo nyingi kabisa katika kila kurasa ukifungua haikosi kilinga haki za binadamu. Haki za kimsingi nimesema hizi ndizo zimedominant, zimekuwa ndiyo nyingi kabisa katika kila kurasa ukifungua haikosi kutaja haki za binadamu, haki za kimsingi tumetilia mkazo sana na tumesema kwamba ni haki ya serikali ni jukumu sasa la serikali kuhakikisha kwamba haki za msingi zinapatikana sio kwamba ni privilege au favour. Askari asikufanyie kazi ni kama ambaye ni favour, anakufanyia lakini asingefanya kama angekuwa na wakati wake asingefanya au kiongozi afanye mambo lakini mkimuuliza awaambie mimi kwanza nawafanyia favour tu lakini mwenyewe nilikuwa na mambo yangu. Sasa human rights obligation ni lazima kwa serikali hakuna hiari tena hapa.

Sasa hizi haki tumezitaja pia tumeziandika kuna haki ya kuishi, ya maisha na tukasema kwamba kwa sababu hiyo tumeondoa kifo. Mtu akishitakiwa kwa kifo tumesema afadhali apelekwe akae ndani milele, maanake atakuwa amegungiwa kazi zake za kufanya. Halafu kubaguana, tumesema hatutaki mwananchi wa Kenya abaguliwe kwa upande wa ukabila, dini, rangi, eneo anakotoka kama ni mtu asiyejiweza. Hakuna kubaguana, wananchi wa Kenya wale walioa, ambao hawajaoa wote tunasema vijana, wazee sote tuko sawa katika sheria ya Kenya. Tumetoa pia pale, haki za wanawake tumesema ya kwamba wanawake pia wasibaguliwa wawe na haki za kimsingi sawa sawa na wengine zinapowezekana kutegemea na mila na dini ya wale watu.

Halafu kuna haki za wazee, wazee walilalamika kwamba wakimaliza miaka hamsini na tano hatuna kwenye darubini. Akisimama tunasema huyo mzee mwacheni busara. Sisi tunataka kusema hakifadhaa wazee bwana wameisha maisha yao sasa tumesema hawa kwanza ndiyo wanatakiwa kupewa heshima zaidi hawa ni senior citizens kwa hivyo wazee tumewawekea haki zao pale,

wana haki kushiriki katika maendeleo hata kama wamemaliza umri wao ambao walikuwa wakifanya kazi bado wazee wana ruhusa kufanya wanavyotaka.

Haki za watoto ndiyo nyinyi zaidi kwa sababu kuna mswada ambao ulipitishwa juzi juzi kuhusu haki za watoto, ndiyo tumeuleta hapa tukachanganya kuna mambo mengi sana hapo ambao tumeleza kuhusu watoto, lakini la muhimu ni kwamba watoto watakuwa wanapata elimu ya msingi ya bure hilo ndilo neno ambalo lipya kabisa katika hapo (clapping). Kutakuwa na free na lazima, compulsory sio bure hivi hivi lakini lazima kwa hiyo mtoto kuanzia katiba kupitishwa bila kupeleka shule tumetaja hadhari ambazo mzazi atazipata pale ni bure na tunasema serikali ihakikishe kwamba ni bure sio kwamba ni bure lakini ukifika kuna shilingi shilingi sijui ni kitabu shilingi kumi sijui nini tumesema ihakikishe kwamba ni bure hiyo sheria tumandika pale (clapping).

Tumesema ya kwamba watoto kwa mfano wamefanya makosa madhambi wameshikwa hao hawatawekwa seli moja na watu wakubwa saa hizi inatendeka halafu watoto wanapatishwa taabu sana. Tumesema watoto watakuwa na jela yao mbali na watu wakubwa watakuwa na jela yao mbali, halafu watoto kama wana kesi kama hivi ameshikwa na kesi lazima sasa serikali kupataia wakili ni lazima.

Halafu, tukaja upande wa family tumerudi kwamba kwa sababu sisi ni wafrika tumesema kwamba ni lazima ile family, jamii ile basic jamii ni lazima tuwe tunaishikilia mkazo zaidi watu wale ambao wanavilema, wasiojiweza tunawapatia haki zao hawatabaguliwa watakuwa na elimu yao ya kutosha vile vyombo vyote vya elimu yao vitapatikana na mambo yote wanayohitaji tunayaandika pale kusoma katika section 39 iko pale.

Halafu tumeeleza pia uhuru wa kuabudu, kuamini tumesema kwamba pale kila mtu yuko na hiari pia katika kufuata dini yake na muongozo wa dini yake, bora asiwe anadhuru dini nyingine. Kupigana mawe Waiislamu na Wakristo ndiyo hatutaki, hiyo ndiyo tumekataza. Wewe kama unaenda msikitini wewe nenda ukaswali huko usome Korani mpaka asubuhi, hakuna shida kama wewe una crusade yako nenda ukafanye huko hakuna shida lakini, kama sasa utaingiliana na mwenzako sasa hapo ndiyo tumekataza. Kwa sababu watu walilalamika kuna makanisa kuna dini zingine kuna ma-crusade mengine ambao huwa yanadhuru sana mazingira ya karibu pale kuna watu wiki nzima hawalali. Kuna seminar hapo sijui kuna nini hapo watu wakesha ngoma na nini na nini lakini huwezi kuingilia kwa maana wasema sisi tuabudu. Sasa tumesema una uhuru wa kufanya hivyo lakini sasa angalia jirani yako asidhurike.

Pia tukasema kwamba si ruhusa sasa mwananchi kufutwa kazi au kushitakiwa kudhulumiwa au kunyimwa haki maanake amesema siku ile ya kuabudu hakuenda kazini, kwa mfano Ijumaa. Kama Ijumaa imefika sasa tano Mwislamu anataka kuenda kuswali, wewe tajiri huwezi kumwambia haiwezekani hiyo maana hapa kwangu kazini wapewe uhuru sasa (clapping). Na wale watu wa Kiswahili Jumamosi, Sabato, Jumamosi kwao ni free sasa wataenda kufanya swala zao na Wakristo Jumapili ni hiari yake sasa kwenda kanisani.

Halafu, freedom of expression, kujieleza sasa tuko na uhuru kujieleza tunavyotaka bila ya kudhuru mtu mwingine bila ya kutukana. Tumetoa freedom ya press na magazeti tumesema tuna freedom ya wale wasanii kufanya michezo, kuimba nyimbo zao na freedom ya elimu mambo ya maswala ya utalamu kule kuandika vile unavyotaka na kufanya research unavyotaka hivyo sasa tumeviweka kwenye katiba. Maanake saa nyingine unataka kufanya unaambiwa lazima upate permit kwa mtu fulani, ukifika pale akishasikia unafanya maneno haya, anasema la hakuna ruhusa sasa mambo yako yanakwama sasa tumewapata uhuru ni uhuru wa kufanya unavyotaka.

Halafu kuna lazima mwananchi akitaka habari zilizo kwenye serikali lazima azipate. Access to information kila mwananchi ana haki ya kuenda kuuliza kwamba nasikia kuna register ya nini na nini hapa sijaona mimi nataka kuiona ana haki ya kupatiwa. Halafu uhuru wa kisiasa wananchi wanaruhusiwa kuunda vyama wanavyotaka. Wananchi walisema kwamba tuweke idadi maalum ya namba lakini tukisema ukisema kwamba kuna freedom of association, halafu tena uweke namba sasa utakuwa umepingana. Kwa hivyo wananchi wanaunda vyama wanavyotaka, lakini vyama tumeviweka kanuni zake na zile kanuni ni ngumu sana sio kila mtu ambaye ataweza kuunda chama. Ni lazima kwanza muwe watu watu ambao viongozi wote wametoka katika kila eneo, Mikoa minane ya Kenya ni lazima. Ni lazima kuwe na dini zote hapo, ni lazima kuwe na kila umri hapo, kila kabila sasa hapo si kweli kwamba utaunda chama chako cha kidini, kikabila, kieneo au cha kimarafiki hakiwezekani.

Pia tumesema kwamba uchaguzi wowote kama nilivyosema ni lazima uwe free and fair, wa haki na tumesema uchaguzi wote utakuwa ni wa siri. Upande wa property ni mali tumesema kwamba wananchi wa Kenya wanaweza kupata, kununua au kutengeneza au kupata mali, rasilimali pahali popote wanapotaka na serikali ndiyo italinda hizi mali za wananchi. Upande wa wafanyikazi, tumesema ya kwamba wafanyikazi ni lazima wawe na uhuru wa kugoma. Si kwamba ni hatia kugoma tumesemwa kama kuna mambo ambayo hayafanyiki vizuri pale, wale wana haki ya kugoma kudai haki zao hiyo tumeiandika (clapping). Na wana haki kujiunga na vyama vya wafanyikazi trade unions vile wanavyotaka.

Halafu, tumekuja upande wa environment, mazingira tumesema sasa itakuwa ni lazima kwamba mazingira yawe masafi, mazingira yawe mazuri ili tuweze kupata hewa safi mumonyoko wa ardhi kuzuia sasa itakuwa ni jukumu la wananchi na serikali kuhakikisha kwamba mazingira yao ni mazuri. Jambo jingine tumesema wananchi wa Kenya wana haki ya kutawala vizuri, fair administration. Uongozi mzuri na tukatia sheria number sitini na sita kwamba kila mwananchi ama haki ya kukatana utawala mbaya. Itakuwa si hatia wewe kukataa mtu aje kiongozi akwambie neno hili fanya neno hili fanya ukiliangalia lile haliingiliani kwa madaa. Mimi sifanyi bwana nenda unatakaa. Sasa sheria umetoa namba sitini na sita pale unaweza ukwambia hiyo si sawa sawa na katiba hiyo sifanyi sasa wawe angalia vile utafanya hatusemi ya kwamba wananchi wakiuke sheria au wakatae maadili ya serikali lakini tunasema lazima haki ifanyike hii ni basic principle hata hiyo kiongozi na yeye pia ana haki lazima atekeleze.

Jambo jingine tumetaja hapa ni wale washukiwa, mtu amefanya kosa anakuja kuchukuliwa na askari au polisi anapelekwa ndani haki zao sasa tumeziandika. Watu kama hao hawaruhusiwi ku... ile torture hawaruhusiwi kupigwa kuteswa ili waseme habari

ambazo ni za uongo lakini ziandikwe kwamba alikubali kwamba aliiba huyu. Tumekataa hapo tumesema mwananchi aweza pia akanyamaza na mimi sisemi lolote mpaka wakili aje hapa, na hana ruhusa kupigwa. Tumesema akienda ndani, seli kule sio ruhusa alale awekwe seli pamoja na wale ambao tayari wameshafungwa yeye itakuwa yake ni rumande tofauti na wale ambao tayari wana-serve sentensi zao tofauti mpaka afanyiwe kesi ajulikane kwamba huyu kweli na yeye alifanya makosa ndiyo atavuka aende upande ule mwingine. Hizo ni nyingi sana tumezieleza karibu kurasa tatu.

Halafu mwisho tukaeleza habari ya tumeunda tume ya human rights. Commission ya human rights and administration justice. Hii ni tume ambayo sasa itaangalia maswala yote ya haki za kimsingi na kibinadamu za wanakenya. Na katika tume ile tumeweka departments nyingi sana tumeweka departments za akina mama, yule bwana mnamwita public defender, ombudsman watu walitaka majina hayo. Yule ambaye unaweza ukaenda ukashitaki kiongozi, au askari au mlinzi akashitakiwa na akapelekwa kortini hiyo tumeiunda ina kazi nyingi sana.

Twende upande wa kura, uchaguzi. Tumesema kwamba uchaguzi ni wa siri, tumesema kwamba uchaguzi lazima ufanywe na tume ambayo iko independent. Hii tume ya sasa, ikishamaliza kazi yake tumeipendekeza uvunje tutengeneze tume mpya ambayo itakuwa na waakilishi wasiozidi kumi, commissioners kumi ambao watataoka kila mkoa. Kila mkoa utakuwa na mtu pale. Na hii tume tumeipatia kazi zake zingine tumesema hii ndiyo itasajili vyama vya kisiasa kwa sababu ya ile taabu ambayo tuko nayo vyama vya kisiasa saa hii vinagonganishwa, kwa hivyo tunasema hii tume ndiyo itasajili vile vyama vya kisiasa. Halafu tumeipa kazi tumesema kazi yake itakuwa ikiandikisha wapiga kura kila siku kila mwaka haitangojea mwaka wa kura ndiyo watu waambiwe wakaandikishwe. Sasa ni continuous voters registration kutoka siku tu katiba ikianzishwa yule mwenye kitambulisho na hana kipande cha kura, haya basi kuna kura hakuna kura mwaka huu wewe kazi yako ni kwenda na kujiandikisha mpaka tuhakikishe kila mwananchi amepata vitambulisho vya kura.

Na hawa wanatume ndiyo watakuwa wakifanya kura ya maoni, kwa sababu saa hizi kubadilisha katiba itakuwa ni sana kupita maoni ya wananchi. Kwa hivyo tumesema kwamba sasa itakuwa ni kazi yao hii tume kuhakikisha kwamba wanafanya kura ya maoni. Umri wa kupiga kura bado ni miaka 18. Na yule ambaye tunataka apigania kiti kwa mfano cha U-councillor au cha Ubunge, tumeeleza katika kitengo sabini na tisa(c) ni lazima awe ni mtu wa sehemu ile, ako na mali sehemu ile na anakaa sehemu ile.

Halafu tumekuja upande wa uchaguzi wa vyama vya kisiasa, tumesema pia uchaguzi huu saa hautaachiwa vyama peke yake maanake tunasikia kuna malalamiko kule. Kwa hivyo uchaguzi wa chama utakuwa supervised na electoral commission na tume nyingine za nje maanake kuna kuwa maonevu yanatokea kule.

Bunge, tumetaja kazi za wabunge sasa. Zimeandikwa kabisa, tumeziandika kazi za wabunge ili wasipofanya tunajua jinsi ya kufanya. Kama tunataka kuwatoa, tunaangalia tu kwenye katika kazi zao ni nini hizi, hakufanya hizi haya. Na kama tunataka kujua kuwa yule amefanya tunaangalia tunasema huyu ndiye huyu. Kwa hivyo tumeziandika kazi zao sasa itategemea nyinyi mumefanya nini kama mtakwenda bado mwafanyishe kazi kama vile mnazo zifanya sasa mtajua nyinyi wenyewe. Mnazijua zile

kazi mnazowafanyisha nyinyi hivi sasa.

Tumesema bunge kazi yake sasa umekuwa ni kubwa zaidi, wana uwezo zaidi wao ndiyo wanapitisha mambo mengi sana sheria zote wao ni lazima zipitie kwao. Yale mabunge mawili kazi yao ni kusaidiana na hasa lile bunge la juu kazi yake ni kuhakikisha kwamba usawa unafanyika nidyo maana tumesema mtu anayetaka kupigania kiti cha bunge cha ile Lower House miaka ishirini na moja mpaka miaka sabini. Lakini mtu anayetaka kupigania kiti cha uwakilishi, kile cha national council ile Upper House, ni lazima awe na miaka thelathini na tano kwa sababu hao ndiyo wanaangalia ile speed ya wale wengine kule kama wale ni vijana basi hawa kidogo wana umri wa juu zaidi.

Wabunge tumesema kuna mia mbili na kumi wa zile constituency zilizoko sasa halafu kutegemea na vile vyama vitakavyopigania, tumesema kutakuwa na viti tisaini ambavyo vile vyama vitachagua watu wao ambao watawakilisha, halafu tena kila wilaya itachagua mtu mmoja na thelathini watakuwa ni akina mama. Wanne kutoka kila mkoa, saba na wawili kutoka Nairobi na tumesema katika upigaji wa kura, kura zote zitapigwa kwenye madebe ambayo ni transparent yale ambayo yanaonekana (clapping). Na kura zitahesabiwa kwenye kituo.

Audience: Very good (clapping) (laughing)

Com. Swazuri: Halafu tumetoa upande wa kupitisha sheria kulikuwa na malalamiko kwamba wabunge hujadili miswada halafu ikawa ni yule mkuu wa nchi atie sign, halafu inaweza kumaliza miaka miwili, mitatu mpaka mwisho ikapotea hivyo hivyo hata mkija kukumbusha pia nimesahau kwamba kulipitishwa neno kama hilo. Sasa tumesema ni lazima atie sign katika wiki moja wakishapitisha wale basi tutampatia wiki moja ikizidi wiki mbili huo mswada umeshakuwa ni sheria. Pia tumeunda, tumeweka kazi za Parliamentary Service Commission, kuna tume ya mambo ya bunge aidha hawa ndiyo watakuwa wameandika timetable bunge litakaa lini litamalika lini sio ati kwamba siku watu fulani tu ndiyo wataamua kwamba bunge leo ndiyo mwisho na iwe namna hiyo kuna Parliamentary Service Commission.

Haya upande wa viongozi wa kitaifa, yaani executive kama nilivyosema hapo mwanzo, tumezisema kazi za rais katika namba 151 tumeandika kazi za rais ni nini hapo. Kazi yake kubwa ni atafungua bunge anaweza kwenda bunge akahutubia pale, anaweza kulivunja bunge lakini vikwazo tumeziweka kwenye 142 hapo halafu yeye ndiye mkubwa wa taifa la Kenya yeye ndiye analinda Kenya katiba na kadhalika. Lakini mambo mengi tumeyaondoa tukayapeleka kwa waziri mkuu, tumeziweka hata ukiangalia 152 kuna kazi nyingi ambazo tumempatia rais pale halafu ni kama nilivyosema mwanzo tunaweza tukamtoa ikiwa tunafikiria hafanyi kazi yake kulingana na tulivyo andika hapa. Tunaweza tukamshitaki kama tunafikiria kwamba hakufanya inavyotakikana na tumesema rais atakuwa kati ya miaka thelathini na tano mpaka sabini. Zaidi ya sabini haiwezekani. Na yeye lazima awe na shahada ya degree kutoka chuo kikuu (clapping). Na rais hatakuwa mbunge. Hatafikani kuwa mbunge, kama vile vile mawaziri si wabunge hata rais pia constituency yake ni Kenya nzima kwa hivyo sio mbunge.

Halafu tumeeleza pia kazi za makamu wa rais na yeye ana kazi zake tumeeleza kazi za waziri mkuu tumeziandika pale tumeeleza

kazi za wale manaibu wake, tumeeleza kazi za mawaziri na tumesema watu wote hao waziri mkuu pia yeye peke yake atakuwa ni mbunge kwa sababu itabidi watu wachague wabunge halafu mmoja wao pale ndiye atachaguliwa kuwa waziri mkuu.

Upande wa mahakama, na mnajua tumepolekewa kortini mara nne sasa na mahakimu hawa sasa nafikiri tatizo letu kubwa ilikuwa wananchi walisema kuna corruption. Pale ubajirifu kwamba kesi pia zinaweza kuamuliwa nje ya mahakama lakini ukapigwapigwa mdomo tu pale lakini uamuzi ulioko na ushatolewa wananchi walisema hivyo hivyo wananchi walisema kwamba kesi zinachukua muda mrefu mno hata miaka kumi kesi hiyo ni ya kutia tarehe sasa ndiyo vita vikaingia hapo tumesema kwanza kwamba corruption katika Kenya nzima pamoja na haya mahakama tumesema ni haramu sasa. Halafu tumezipanga zile korti zote za kutoka chini, Magistrate's Court na Kadhi's Court mpaka tukaenda Court of Appeal.

Halafu tumeteuwa ile Judicial Service Commission ambayo iko na watu ishirini na moja pia wananchi wakawaida watatu wamo humo. Watu wa NGO's wamo humo, mkuu wa sheria yumo humo, Chief Kadhi yumo humo yaani mwanamke wa Kiislamu moja yumo humo. Hii ni cross section ya Kenyans ndiyo watakuwa wanasema fulani judge fulani anafaa kuchaguliwa kuwa mkuu wa korti fulani wao watajadiliana wampeleke rais, rais apeleke waziri mkuu, waziri mkuu apeleke bunge, bunge watajadiliane wakikubaliana hiyo yatosha. Hivyo ndivyo ataingia. Kwa hivyo sasa watakuwa na hadhi yao tunawarudishia hiyo hadhi yao.

Na hata kufutwa ni hivyo hivyo kama judge anataka kufutwa kwa sababu amefanya makosa kwanza kutateuliwa kijitume cha watu wanne watano wapeleke mapendekezo yao kwa rais, rais apeleke bunge watajadiliane wakikataa hiyo judge yuwaendelea akikubali atolewa. Na tumesema na hii ndiyo imetuletea matatizo, ma-judge wata-retire miaka sitini na tano. Saa hizi hufika miaka sabini na nne, lakini watu wengi wamelalamika kwamba mwanadamu akifika miaka fulani kidogo huwa kuna matatizo. Sasa tukaonelea tusifanye ile hamsini na tano ya mfanyikazi mwingine wa kawaida, tukaweka miaka kumi zaidi. Sitini na tano na hiyo ndiyo imetuletea matatizo makubwa sana.

Haya ya kumi tumezungumzia upande wa serikali za majimbo, serikali za wilaya, serikali za mitaani, tumezieleza pale. Sababu zake za kuwa na vitu kama hivyo tumesema ni kwa sababu wananchi wanataka uongozi na utawala karibu. Wanataka services zipatikane karibu. Kwa hivyo principle moja ya hizo devolution of powers kupeleka serikali huko mitaani ni kwamba wananchi wapate huduma nzuri haraka kwa urahisi tena iko karibu kabisa hiyo ndiyo sababu ambayo umetufanya tufikirie upande wa devolution of powers. Kwa hivyo tukianza na serikali ya kijiji nyinyi wenyewe mmepewa ruhusa kama mtachagua kwa kuwateuwa au mtafanya uchaguzi kwa kura ya siri, mtaangalia nyinyi wenyewe. Na wale wanachama wa ile kamati ya serikali ya kijiji itakuwa na wanachama wasiozidi kumi hapungui sita hawazidi kumi. Baada ya hapo tutachagua wawili kati ya hao wataunda serikali ya location lakini yule mkubwa wa location ambaye atakuwa sawa sawa na councillor wa sasa atachaguliwa na wananchi. Huyo atachaguliwa direct debe lake litakuwa mbali. Watu watateuliwa waende kwa ile council lakini yeye atachaguliwa na wananchi. Halafu wawili wa hapo pia tutawapeleka tutawapandisha cheo waende kwenye district government.

Hii serikali ya wilaya ndiyo ambayo iko na nguvu zaidi kuliko hizi nyingine mbili. Hiyo mwananchi watachagua directly wale members wao. Wao wenyewe watachagu na watachagua pia yule district governor, district administrator wananchi wenyewe watachagua. Na hata huyo district governor pia kama hafanyi kazi vizuri, pia yeye yuwaenda. Halafu juu ya hapo tena serikali ya jimbo sasa provincial government na hiyo itakuwa na wakilishi kutoka kila wilaya ya jimbo lile na watachaguliwa pia pale provincial administrator au provincial governor. Hizi serikali zote zimepangiwa kazi zao za kufanya majukumu yao ni nini. Kazi zao ni nini na mwelekeo wao utakuwa vipi? Umeandikwa hapa. Kwa hivyo sasa wale mlikuwa mkisema twalilia majimbo sasa majimbo mmepeva mtaharibu wenyewe au mtengeneze wenyewe (clapping).

Upande wa ardhi nafikiri hapo tulikuwa na shida sana upande wa Pwani. Tumesema kwamba ardhi yote ni mali ya wananchi wa Kenya. Hakuna mgeni ambaye tumesema atakuwa anamiliki ardhi (clapping). Halafu tumesema ya kwamba kama alivyoeleza mwanzo tuna public land tumeieleza pale, tuna private land halafu tuna ile community land ambayo ni ya wananchi, wananchi wenyewe wataunda kamati yao au watafanya uchaguzi wajue ni akina nani watawapa jukumu la kumiliki hii ardhi yetu. Wao wenyewe ndiyo wamepeva katika kitengo mia mbili thelathini na nne na hao wenyewe watakaa waseme hii ardhi hizi ni zetu sasa mzee fulani, kijana fulani, mama fulani mtakaa kwenye kamati fulani. Mtu yeyote anayetaka ardhi ni hapa mtu yeyote anayetaka kununua ni hapa hiyo imepatikana katika 234 (clapping).

Kulikuwa na malalamiko kuhusu kupata hati za ardhi, title deeds. Zimechukua miaka mingi title deeds. Zingine zimeandikwa kutoka Nairobi, mtu hata hajui ardhi yake anapewa title deed anakuja anakuambia hapa ni pangu malalamiko haya yalitolewa na wananchi. Halafu wananchi wakalalamika kwamba kuna title deeds mbili au tatu lakini za hiyo hiyo plot moja kwa hivyo vita sasa watu wanateta na kesi zinachukua miaka milele na milele. Kama jana nilivyosema kuna watu ambao mpaka wazazi wamefariki walikuwa wameteta na mpaka watoto wameridhi hiyo vita na haijulikani pia vitaisha lini. Sasa tumesema kwamba tunapitisha sheria katika hii miaka miwili baada ya katiba hii kuanzishwa kwamba tutatengeneza sheria mwafaka sheria moja nzuri ambayo itakuwa mambo yote ardhi inaangalia hivi sasa sheria za Kenya za kuhusu ardhi zinapatikana katika sehemu sabini na sita. Tuko na sheria sabini na sita nyingi zinahitajika sasa kwanza tunasema tuna hamornize hizi.

Halafu tunasema kwamba tunatakikana sheria ipitishwe ya kuhusu kesi za mashamba zimalizike kwa muda fulani. Tumesema katika miaka miwili mambo ya mashamba, mashamba hayo kesi zake tumemaliza sasa tunaanza afresh. Kisha tukasema kwamba katika miaka miwili hii pia tutapitisha ya kwamba ikiwa kuna mtu yeyote au watu wowote au kampuni yoyote ambayo imechukua ardhi ya uma na si yake, land grabbing si yake, mtu yule au kampuni ile, ardhi ile is yake hiyo ardhi itarudi kwa wananchi na serikali. Halafu tumesema pia tutaangalia na hapa wananchi wengi wa Pwani ndiyo wanahusika. Kuna zile claims za wananchi wa Pwani kwamba ardhi zao zilichukuliwa miaka elfu moja iliyopita, miaka mia nane, mia tatu, mia mbili, ishirini. Tumesema hapa ni lazima vitu hivyo vichunguzwe ikiwezekana ikiwa ni kurudishiwa wenyewe au kulipwa ridhaa au vile ambavyo tutafikiria kufanya kuhusu ardhi kama hizo tumeandika katika kipengo hicho (clapping).

Tumesema pia ya kwamba kulikuwa na malalamiko kwamba tukikaa mahali halafu ukigunduliwa kuna madini sasa mali ardhi

hiyo si yako tena, kuna mtu anakuja anachukua anakuambia sasa wewe utakaa kando bwana utatupisha kidogo hapa tunaona kuna mali hapa. Sasa tumesema ardhi na mali yake pale ni ya yule mwenye ardhi (clapping). Kuna vitu fulani pengine vikipatikana hata wewe mwenye ardhi huwezi kuishi pale lakini sasa itategemea maelewano ya wewe na yule ambaye atakayekuondoa pale. Mtakubaliana vipi, lakini mali na ardhi ni yako.

Upande wa mazingira masafi, tumesema tumeunda tume ya mazingira National Environment Management Commission. Fedha za uma tumeleza pale kwanza katika sheria za fedha tumesema si ruhusa mtu yeyote kutoza kodi. Aina yoyote ya kodi ni lazima ipitishwe na bunge maanake watu wanalalamika kwamba mtu mara ameweka wevi pale akwambia shilingi tano haiwezi kupata hapa shilingi tano mara kuna jiwe limewekwa pale wataka kukanyaga maji unaambiwa ukitaka kukanyanga hili jiwe shilingi mbili ndiyo upite, tumesema hizo ni kodi hizo. Maanake yule atakayepata pesa jioni kodi zote ni haramu kuweka kodi yoyote mwenyewe kodi zote ni lazima zipitie kwa wabunge maanake tumesema tunataka kuwa transparent and open.

Upande wa central bank, banki kuu ya taifa sasa hii tumeandika hii ni constitutional office sasa iko katika katiba sio katika hio ministry of finance or treasury. Sasa ni ofisi ambayo iko katika katiba kazi, zake tumeziandika moja kazi yake ni kutengeneza sarafu ya Kenya na tumefanya sarafu ya Kenya isiwe na picha ya rais alioko (clapping). Halafu upande wa controller and auditor general office ile tumeikata mara mbili, kuna cointroller of budgets na auditor, yule mtu wa kuangalia matumizi ya pesa za serikali. Huyu controller of budget sasa kazi yake itakuwa, budget ya Kenya sasa itafanywa na watu wote sio waziri angojee tarehe kumi June ndiyo aje na kifurishi chake aseme tumeongeza bei hii. Sasa budget inatakiwa izungumziwe na wananchi miezi miwili kabla kila mtu ajue kwamba mwaka huu utakuwa na pesa fulani, mwaka huu bei zitaongezewa fulani isiwe ni ghafla saa sita ya usiku unaambiwa mafuta yamepanda (clapping).

Halafu utumishi wa uma public service pia tumeangalia sana vile watu wamesema pale tukasema ile Public Service Commission tutaiunda kivingine ingawaje itateuliwa na serikali lakini bunge ni lazima lipitishwe na katika sehemu hiyo ndio tukaja upande wa polisi. Polisi kwanza tumebadilisha jina lao sio Police Force lakini ni Police Service, kwa sababu kazi yao sasa wale ni watumishi, tumeziandika katika mia mbili sitini na nne kazi za polisi ni zipi hapa. Ni lazima wahakikishe kuna usalama wa wananchi, haki za binadamu zimelindwa, usawa wa wananchi, waondowe visa vya ujambazi pale tumeandika na kadhalika mambo yao yote tumeandika yote pale. Ndiyo maana tunaita Kenya Police Service sio Kenya Police Force, ile nguvu ambayo watu walikuwa wanafikiria wanatumia. Na tumesema kwamba polisi watakuwa trained professionaly, tumeandika pale katika (h). Police watakuwa trained professionally,, hapa tunasema wafundishe nyinyi kama ambavyo mlitaka public relations. Police itabidi wafundishwe maanake mlisema kwamba wakija wanapiga makofi hata kabla ya kukuuliza unapigwa makofi. Sasa tunasema tunataka kufundisha trained members into public relations jinsi ya ku-handle wananchi tumesema kwamba hiyo itakuwa namna hiyo. Na huyu commissioner wa polisi pia tumesema yeye ata-serve maximum miaka kumi na yeye awe mtu ambaye ana degree. Polisi mkubwa wa polisi lazima awe ni graduate amesoma chuo kikuu. Halafu tumesema yeye pia atachaguliwa na bunge.

Prison tumeziita Kenya Correctional Services, kazi yao ni kurekebisha wananchi nao mambo yao ni kama yale yale ya polisi.

Wanajeshi katika sura ya kumi na tano tumeunda majeshi sasa yako katika katiba. Zamani majeshi yalikuwa kwenye office of the president, Ministry of Defense. Hapo sasa tumewaweka katika katiba kabisa wawe wana ofisi zao maalum with a tenure of office. Wale wakuu wa majeshi pia nao wata-serve miaka kumi maximum na tumeunda tume ya taifa ya security, National Security Council ina wanachama pale kutoka rais mpaka mkuu wa sheria, mkuu wa navy, mkuu wa airforce, mkubwa wa polisi hawa ndio watakuwa na jukumu la kutulinda kama kuna vita hao ndiyo watakutana watoe uamuzi wao wapeleke bunge, bunge lijadili tuseme haya twendeni tukapigane na hawa watu.

Halafu sehemu ya kumi na sita nimeitaja mwanzoni tumeitoa sheria ambazo viongozi wa kitaifa, viongozi wa uma ambazo wanafaa kuzifuata tumesema ya kwamba mwananchi yeyote akiona ya kwamba hawafuati masharti hayo ambayo tumeandika pale, ni lazima mwananchi yule atalalamika na ikijulikana ya kwamba ni kweli yule kiongozi amekiuka hiyo sheria wana haki ya kumtoa. Halafu tumeunda tume nyingine, zile zilizoko nyingine tumezirekebisha nyingine tumeziacha vile vile zilivyo lakini muhimu ni kwamba wafanyakazi au maafisa au hawa wanatume wa aina yeyote sasa watachaguliwa na bunge sio mtu mmoja na au ofisi moja au ofisi mbili sasa zimeteuliwa na bunge.

Haya neno la mwisho abalo tumeliandika pale ni kuhusu ubadilishaji wa katiba, nani ataweza kubadilisha hii katiba yetu tuliyo pigania sana. Tumesema kwamba bunge lina haki ya kubadilisha hii katiba lakini si rahisi kwa sababu ni lazima Lower House wawe na two thirds, yaani thuluthi mbili. Halafu pia na Upper House pia wakubali na hapo tunajua haitakuwa kazi rahisi. Tumesema ikiwa basi kuna maneno ambayo ni lazima yarekebisha, lakini yanahusiana na maneno haya ambayo mtayataja ni lazima wananchi wenyewe wataitwa tena kama hivi ndivyo katiba ibadilishwe. Ikiwa kuna jambo la kuhusu mipaka ya Kenya inataka kubadilishwa either tuchukue zaidi au tupunguze wapatie wenzetu kilometer tano, hilo si jambo wananchi mtaitwa mshauriwe na mtoe uamuzi.

Ikiwa kuna sheria yoyote kuhusu uhuru wa wananchi sovereignty of the people hours za wananchi kitengo chochote katika katiba hii ambacho kinahusu sovereignty uhuru na nguvu za wananchi kule kujiamulia mambo yao neno hilo halibadiliki mpaka wananchi wenyewe waulizwe. Halafu haki za kimsingi ikiwa kuna section yoyote inataka kubadilishwa lakini ya kuhusu haki za kimsingi, maji, elimu, freedom of association haibadilishiki mpaka wananchi wenyewe. Kama kuna swala lolote kuhusu serikali hizo tulizozitaja za kijiji, location, wilaya, majimbo, kitaifa swala lolote kuhusu hizo. Serikali halibadilishwi na bunge ni wananchi wenyewe. Swala la uraia ni wananchi wenyewe na mambo mengi tumeyataja pale katika 294 hayo ni mambo ya wananchi wenyewe.

Sasa mimi nitakomea hapo ili ni wakaribishe yeyote ambaye atatuchangia yeyote ambaye atatuchangia, ambaye yuwaona ya kwamba tuliwadanganya tulifanya kazi ya upuzi ambayo yakuta ya kwamba mambo yenu tumefanya vile tunataka au bado zaidi tunataka tuongeza sasa uwanja ni wenu. Asanteni sana, wewe uko karibu ngoja kwanza. Nitaanza na mama pale useme jina lako na tunataka kukusikia kwenye kitega sauti...(inaudible)....

Regina Kalume: Sasa ishikwe na mimi au ishikwe na mtu.

Interjection: Sema tu wewe zungumza

Kalume: Mimi nina kitu kigogo tu nataka niongeze

Com. Swazuri: Jina lako

Kalume: Mimi naitwa Regina Kalume.

Interjection: Zungumza kwa sauti.

Kalume: Mimi ninataka kuongezea swali lako la habari ya madini, madhehebu. Nimeona umesahisha upande wa Christians na crusade zao ni kweli. Lakini upande wa msikiti ulipunguza, tunayo sababu na sisi hapa tunaishi hatubaguani kwamba dini ya Christian na Islam ni mbali mbali. Sisi sote tunamlalamikia hivyo Mungu, sote tunaomba Mungu. Msikiti hapa iliwekwa karibu, karibu sana kama ulivyosema lazima watu watazame afya za watu na habari ya usingizi unavyokuwa ni muhimu kwa mwanadamu. Sasa hapa pana msikiti ambayo imejengwa, wale watoaji wa plot wamezitoa kimakosa kabisa imezingiwa nyingi karibu na wakati ule wa usingizi unanza kuingia ndipo hapo utaona kwamba huyu anapiga kelele hapa, huyu anapiga kelele hapa, sasa katika hii boma tafadhali mkubwa hatutalala tutaamka tutaketi. Wengine tuna pressure, wengine wana wazimu unazidi anapata tembe haiwezekani. Sasa hiyo anayehubiri kuita watu waende kanisani, msikitini wakaswali ni lazima wapige kelele boma nzima? (laughter).

Sisi hapa tuko utumwani kwa hili neno umefanya vizuri kuligusia, hili neno lilikuwa laumiza watu wengi sana hawana pa kwenda. Na tunalaumu wale waliota zile plot ndiyo tunawalaumu kwa nini msikiti uwe hapa, uwe hapa, uwe hapa, uwe hapa yeye amezitoa kwa zile pesa au ametoa kwa ajili ya Mungu. Hatulali nakuambia, hatulali wacha ile crusade inakua mchana halafu watu tena iko mbali si katika manyumba. Lakini hizi ziko katika hapa hapa tunaomba kama inawezekana hiyo irekebishwe ili kuongea kwao wakiita watu wakienda msikitini iwe na sababu na mpangailio ya utaratibu.

Interjection:(inaudible).... Nikusikia

Cllr. Chullumuli: Jina langu ni Councillor Joseph Chullumuli. Mimi ni councillor aliyeteuliwa kwa chama cha KANU kisha ni secretary wa Bahari branch ya KANU. Nimefurahishwa sana, kitu cha kwanza ninaanza kwa kuwashukuru kwa kazi yenu ambayo hiyo ni kazi ngumu. Tukiongeza zaidi ni kwamba, sisi ambao hatujaingia kwenye mafiga kupika na tukachomwa na moto, kazi yetu ni kula tunajua tu kwamba chakula hiki kitamu hiki ni kibaya hiki ni kizuri kimeiva hiki hakijaiva. Lakini nenda kwenye mafiga upike ndiyo ujue hali ilivyo. Kazi hii ya kutengeneza hii katiba haikuwa kazi ndogo ilikuwa ni kazi ngumu lakini

tunashukuru ili speed mlikwenda mpaka mkaleta katiba ambaye iko. Katiba yenyewe sisi ambao tumeipitiapitia hii draft ambayo muko nayo kidogo kupitia kwa vyombo vya magazeti na vingine, tumeona ya kwamba katiba imetengenezeka.

Kitu ambacho nitatetea wananchi ni kwamba mambo haya ya katiba hasa katiba katika kuingalia na kuigeuza ilikuwa inataka elimu na taaluma wananchi wapewe wajue ni nini wanacho kigeuza na nini kinachotengenezwa. Tukienda kwao wengi hawakuelewa ile katiba iliyokwisha walikuwa wakiamabiwa tu katiba inataka kugeuzwa. Katiba si mkate, kwamba leo tunageuza tule chapati. Katiba ni chombo muhimu ambacho kinalinda masilahi ya mwananchi na kinampa mwananchi uongozi wa kuweza kuendesha masilahi yake ya nchi kwa amani bila fujo na yamulinda kwenye haki yake pia. Kwa hivyo ninaomba tu ninasitaka kukashifu kukosoa kidogo kwamba wakati haukuwako wa kuelelewa wananchi. Wengi wa wananchi hawakuelewa kabisa hiyo katiba inayogeuzwa ni kitu gani na waliletwa tu ni kama mfano kama mama kama huyu ambaye sasa leo mmemsomea mambo ya draft ya katiba lakini mnaona vile anavyozungumza ni kama ambaye anatoa changamoto zake kwenye katiba ni kwa sababu hajapata muelekeo kamili wa kuiona ile katiba iliyokwisha na ni mambo gani yalikuwa yanafanyika.

Yamefanyika vizuri na tunaomba tu yale yawe yamepita lakini haya tuliyoko nayo sasa tunatakiwa tuyaunge mkono vilivyo. Hasa tunwapa tena pongezi kwa kuleta nguvu mashinani na kuileta hali ya katiba na uhuru wa katiba na uhuru wa mwananchi na nguvu kumpatia mwananchi mwenyewe wa kawaida. Kwa sababu, tunapoisoma ile katiba hivi sasa tukiangalia hii sio katiba ile ambayo ilikuwa imepewa mamlaka kule huu mamlaka yamerudishwa chini kwa mwananchi. Kurudi ...

Interjection: Patia mtu mwingine tunataka ...(inaudible)...

Cllr. Chulumuli: Sasa ninataka kusema mamlaka hayo yamerudi chini kwa wananchi kwa kuzipa wilaya ama kuzipa baraza za wilaya majukumu, lakini kitu kilichoko ni kwamba. Samahani najua kuna changa moto zinakuja lakini lazima nikuelezee hata wewe uelewe ninasema nini. Tuna sema hivi.

Interjection: ...(inaudible)...

Cllr. Chulumuli: Sawa si swali tunaelezea basi tafadhali, tunataka kusema ya kwamba katiba hiyo ni nzuri tuliyofanya na tumeleta chini kwa wananchi. Mamlaka hayo yaendeleo kwa sababu afisi zilizokuwa zinatusumbua hapa ni afisi za utawala ndiyo zimekuwa zinatusumbua. Sasa mambo yamerudi kwa wananchi na nguvu imepewa wananchi kuchagua, kwa hivyo tunawapa pongezi kwa kufanya kitu kama hicho. Asante sana wale wametumwa waje hapa ni chief campaigner wa mtu mwingine lakini hakuna shida tunaonana kwenye jamvi (laughing).

Com. Swazuri: Mama tafadhali ...(inaudible)...

Suleiman Juma: Mimi jina langu naitwa Suleiman. Maoni yangu zaidi ni kulingana na kama vile mama alitoa ushauri wake

kulikuwa kwa upande wa msikiti. Sasa mimi nataka kumfahamisha mama ajue hivi kwanza. Hiyo katika kuabudu, hasa sisi waislamu vile tunajua kulingana na kitabu chetu sisi tumekuja duniani ni kubwa zaidi ni kufanya ibaada kwa ajili ya Mungu. Na vile tunaalezwa katika Uislamu ni kuwa pahali popote, wacha ndani ya msikiti hata kufika wakati wa kuabudu inafaa niabudu, kwa hivyo swala aseme la msikiti labda ploti zake zipunguzwe hiyo nakuta kidogo amekosea. Kulingana na sisi tutaomba zaidi tupatiwe nafasi zaidi tujenge nyingi.

Com. Swazuri: Naam.

Geoffrey Mwangudza: Kwa majina naitwa Geoffrey Mwangudza. Mimi ni vile chairman wa KANU, Bahari branch. Nataka nimpongeze hii katiba mpya, kwa sababu muligusa kila sehemu. Hasa upande wa kwamba hata wale wabunge tukiwachagua ikiwa tunaona ya kwamba hawa perform, na miaka mitano haijaisha ikiwa tunaona hawa perform na miaka mitano haijaisha tuna haki kabisa ya kuwaita na kuwatambua na kuwatoa na kuingiza mwingine. Hapo nimepongeza kwa sababu mara nyingi tumekuwa na wabunge wanaenda kule halafu wanalala, huko wananchi wanateseka hapo mimi ninapongeza. Na tena nataka niseme ya kwamba ningependelea uchaguzi ujao ufanywe chini ya hii katiba mpya, kwa sababu hii inapeana level playing ground. Kitu ambacho nilikuwa nataka niseme tu pale, mliposema kwamba kutakuwa na viti tisaini vya wabunge watakaofanya kuteuliwa, hapo mimi naona mliweka viti vingi sana tisaini ni viti vingi sana compared to 222. Kwa hivyo mimi nafikiria ingekuwa hata kama ingekuwa tu half of that, inatosha lakini tasaini ni vingi sana mtakuwa mmewapokonya wananchi uwezo wa kuchagua hayo tu asanteni sana (clapping).

Interjection: Jishikie mwenyewe kila mtu ... (inaudible)....

Dickson Kalama: Shukrani, shukrani sana Bwana Mwenyekiti. Mimi naitwa Dickson Muranga Kalama mkulima. Kitu kimoja ambacho hukukiguzia hapo hukuguza hicho kitu, na nataka ikiwezekana uki-note with seriousness ni kile wale walio-grab land kutoka tuanze uhuru, mwaka wa sitini na tatu mtu alikuja akanyang'anya ardhi ya mtu na hapa wewe haukusema kwamba watu wale ikigunduliwa kwamba ardhi aliechukua ama aliipata kiholelaholela iwe repossessed.

Interjection: Limetajwa

Kalama: Iko? Tena ya poli kwamba hawa polisi hawa tunawaita ati administration police, sisi kwa sababu ma-chief wameondoka na hao wawafuate wale watu wao (laughing). Asante sana.

Elias O. Onam: Mimi naitwa Elias Onam. Kuna pahali umeongea kuhusu haki za watoto, lakini shida yangu ni kwamba sijapata nafasi ya kwenda through, kuna kitu nilikuwa nataka niulize kama iko na kama haiko ningejaribu muongezee. Kuna wakati mwingine ni kisa ambacho nimekishudia mwenyewe. Police station mama anashikiwa na mtoto mchanga, kisha mama anatiwa seli na mtoto yule mchanga. Sasa hapa katika haki za watoto sijui kama hiyo pia nilikuwa mmefikira mkaiwekea provision yake. Kwa hivyo mimi napendekeza hpao muangalie mama akishikwa na mtoto mchanga mpaka iangaliwe njia gani

atakuwa treated yule mama siyo yule mtoto mchanga achukuliwe atiwe ndani na yule mama na yule mtoto hana makosa. Hiyo ndiyo mlikuwa nataka niseme (clapping).

Interjection: Wacha nikusikie

Reynold Mwangunya: Mimi jina langu naitwa Reynold Mwangunya ni mwenye kiti wa chama cha kuondoa umasikini, Kilifi (laughing).

Interjection: Nini wewe endelea

Mwangunya: Jambo la kwanza ambalo nimeliona katika kongomano hili, Bwana Commissioner mimi nimeshanga sana kuona wananchi wa Kilifi wamekusanyika wakipeana maoni yao kuhusu katiba lakini hakuna mjumbe mmoja hapa wa Kilifi ambaye angesaidia kusikiliza maoni ya mwananchi na akayapeleka bunge kesho hakuna. Councillors, labda ni Bwana Chulumuli mwenyekiti wa urban council pale na wachache. Tafadhali jambo hili limeturudisha nyuma kwa sababu ya katiba iliyopita hatukua na uwezo wa kuwatoa. Nashukuru vile kwamba mmetupa uwezo wa kutoa watu kama hawa ambao hawataki kusikiza maoni ya mwananchi na akayawakilisha kwenye bunge. Jambo jingine bwana nataka nilitaje kuna sheria za kazi, labour relations ulizozitaja pale mimi nilikuwa nataka nipendekeze wananchi kwamba mtu mmoja asiweze kukata shauri ya watu maelfu.

Nikisema hivyo nasema waziri ana uwezo ku-declare mgomo wa wafanyikazi kwamba si halali. Tunataka bwana commissioner, mtafute kifungu ambacho uta-limit uwezo wa waziri katika kazi, labour ili kwamba kunapotokea kisa kama kilichoko sasa cha mgomo wa walimu bunge likae chini kikatiba kuzungumza habari ya waalimu, kosa lao, haki yao na bunge likate ni hatua gani itakayochukuliwa kwa watu kama wale. Si waalimu peke yake hata madaktari, industries wapo na popote. Jambo lingine bwana umetuambia mumepeana land ownership ya lease kwa miaka tisaini na tisa. Jambo hili limetuudhi sana kwa sababu, mwanadamu maisha yake sasa hayazidi miaka sabini, leo unapompa lease ya miaka tisaini na tisa, yaonyesha kwamba atakufa yule bado ardhi ni yake, ni ya mtoto wake, ni ya mjukuu na kijukuu. Ningependekeza bwana commissioner kwamba, lease period ipunguzwe na ikiwezekana ifanywe miaka sitini.

Jambo la mwisho tafadhali mruhusu electoral commission mmeitaja, vizuri sana lakini kuna jambo ambalo linatuudhi sana watu hawa ambao wanaenda hapa na pale wakihuburi vita. Na ubaya ni kwamba electoral commission haina uwezo wa kuashika na kuashitaki. Mimi ningependekeza kwa umati huu Bwana Commissioner kwamba katika kazi moja wapo ya electoral commission kuwe na polisi ama prosecutor au judge au nani katika hiyo commission yenyewe. Halafu, mtu yeyote ambaye ataharibu siasa kama tunayosikia yametendeka hapa na pale commission iwe ina uwezo kumshika mtu yule pale pale na kumueaka ndani na ashitakiwe na commission yenyewe sio polisi. Kwa sababu sasa yanayofanyika haiwezekani tafadhali hayo ndiyo machache ambayo nilikuwa napenda kuyataja. Asanteni (clapping).

Lawrence Kazani Gohu: Jina langu naitwa Lawrence Kazani Gohu. Mimi ni mkaazi wa Kilifi township na pia vile vile ni mzee wa kijiji kinachotambulika kama Kisumu ndogo. Vile vile mimi ni chairman wa hiyo kamati hiyo sokoni sub-location ya village elders, wazee wa mtaa. Kwanza nafikiri ningerudia swala la huyu bwana ambaye ameongea sasa hivi juu ya hii lease ya miaka tisaini na tisa nafikiri hata huyu bwana labda hakuwa anafuata vile ambavyo swali labda uwali umeshaeleza. Kwamba watu wa nje ambao wanakuja Kenya ndiyo wanapewa lease ya mwaka tisaini na tisa sio, wewe mwananchi. Wewe mwananchi wewe yako si tisaini na tisa ya watu wa nje ndiyo tisaini na tisa. Wewe unataka kuturegesha.

Interjection: Huyo mgeni

Gohu: Mgeni ndiyo tisaini na tisa, lakini mwananchi yake ni zaidi.

Interjection: ...(inaudible)... endelea sasa

Gohu: Labda sikuelewa. Maombi yangu ni kwamba miaka hiyo tisaini na tisa ya lease ni sawa sawa. Kwa vile tuko nayo hata kwa wananchi. Hivi kuna wengine ambao labda walipata plot, zao kabla ya kufika miaka kumi haja-develop labda. Sasa hiyo miaka tisaini na tisa ambayo anasema labda atakuwa hata pengine baada ya miaka ishirini pengine ndiyo ana-develop. Jambo lingine la pili ambalo nimefikiria labda niwaeleze nina kelele na kila mtu ana wakati wake. Kuna hivi, ni kwamba ile katiba mpya naishukuru kwa vile ambavyo imetengenezwa. Katiba mpya hii imegusia kila kiwango cha mambo ambavyo tulipendekeza hapa na watu wengi walipendekeza.

Jambo moja ni kwamba katika uhuru, tunaita freedom of association na freedom of expresion. Ie uhuru wa kuwa watu wanaweza kukutanika na uhuru wa kutoa maoni na mambo mengineyo. Tunaona kwamba katiba kweli limeturuhusu lakini sasa tukirudi kwa sheria zingine za Kenya ni kwamba hii katiba sasa baada ya ile katiba kuna sheria zingine za Kenya ni kwa hii katiba sasa baada ya ile katiba kuna sheria nyingine za Kenya zile zinaitwa laws of Kenya ambazo zinapatikana katika volume nafikiri ni kumi na mbili ambazo ni sheria za Kenya sasa. Katika sheria hizo, kuna nyingine nyingi ambazo zile wanaita local arts ambazo nyingine kuna vipengele fulani ambavyo ni vya kumugandamisha mwananchi sasa tuki-deal kwa katiba peke yake. Tuseme katiba hiyo ndiyo tuatendeleza na zile sheria ziwe zinabaki vile na inaonyesha kwamba sasa wale wabunge kama hawakutekeleza hizo sheria basi sheria hizo zitaendlea zikitumika. Kama vile kuwa ile moja wanaita Public Order Act, na pengine wanaita Preservation Secret Act ambazo hizo, hizo watu wawili, watatu wakikutana washawe bila permit na mambo mengine kama hayo.

Kwa hivyo tunaomba kitu ninapendekeza ni kwamba wabunge kuwe na commission ambayo itakuwa na law review commission ya ile sheria ambayo ilikuwa ni ya kikoloni kama ni local act ama ni sheria gani wabunge wakishakutana wakae ili kwamba sheria hizi wazirekebishe kulingana na matakwa ya wananchi. Nafikiri hapo ni sawa asante sana.

Com. Swazuri: Kila mtu atapata nafasi.

Interjection: Angalia mana mimi niko mwisho ...(inaudible)...

Wellington R. T. Rassi: Mimi ni Wellington Rassi. Nina haya ya kuuliza. Umesema katika katiba mpya hii itakuwa na mawaziri kumi na watano. Sasa, swali langu ni kwamba mawaziri kumi na tano hawa mtachagua kulingana na mikoa au mtachagua kulingana na ujuzi wa mtu aliyonayo. Kwa sababu siku za nyuma tumeona kuwa watu wote ambao wanachaguliwa wanatoka huko juu huku chini kwetu pwani hatuwezi kupata nafasi hiyo. Sasa kwa maoni yangu mimi nilikuwa napendekeza hivi, kila mkoa upewe mawaziri wawili wawili na manabu wao. Mkoa wa Nairobi kwa vile ni headquarter, ndiyo kikao cha serikali wapate waziri mmoja.

Jambo lingine nilikuwa nauliza hivi katika hii muongozo. Sasa wasema constituency ni mia mbili na kumi, na kutakuwa na wale nominated tisaini. Sasa tunavyoelewa hivi sasa ni kwamba kuwa tarafa zingine ambazo zilibuniwa, ambazo hizo tunajua baada ya miaka mitano zitakuwa nazo ni constituency zile zitakuwaje. Maoni yangu ni kwamba zile baada ya miaka mitano nazo ziwe constituencies zichaguliwe wabunge, kwa hivyo namaanisha ya kuwa wabunge watazidi kutoka hiyo mia mbili na kumi mpaka pengine watakuwa mia tatu. Na wale tisaini baadaye waongezwe ili kuwe na uwakilishi kila pahali hayo ndiyo maoni yangu. Asanteni sana.

Com. Swazuri: Mtu wa mwisho kabla sijaanza kujibu ...(inaudible)... mwisho. Halafu ...(inaudible)... nitajibu

Emmanuel S. Safari: Mimi kwa majina naitwa Emmanuel Safari Stanley kutoka huko Masangoni. Niko hapa mkifanya shughuli zangu hapa, lakini swali langu ni kusema kwanza labda nimekuja kuchelewa kidogo kuhusu ile serikali ya kijiji. Nataka nifanuliwe kidogo. Halafu swali lingine ni kwamba katika sisi wafanyikazi tunaofanya wakati wa ku-retire maanake wengi wao nawaona hata kule kwetu wako wali-retire na wakatafuta pesa zao za NSSF mpaka wakafikiwa na kifo wakafa wakaacha. Hizo pesa zimebaki kule hatujui hapo katiba imesema kiviipi?

Kitu kingine cha mwisho ni kwamba, katika hii katiba iliyoko sasa na imesemekana tutafuata labda tutachagua watu, saa hizi tukawaambia ma-chief basi nyinyi hamumo kwa sababu tumepata katiba mpya. Asante (laughing and clapping).

Com. Swazuri: Nitakupatia nafasi, nikimaliza kila mtu nimesema atapata nafasi. Huo ndiyo mjadala ambao tunataka. Kwanza tumesema kuhusu upande wa civic education, tumesema kuwa hatukuiandika openly tumekubali kwamba haiko open lakini tulikuwa tumependekeza kwamba civic education kuhusu mambo ya katiba, utawala iwe inaendelea kila siku hiyo tumeandika lakini bado haijatokeleza vizuri. Kwanza tunatafuta mahali pa kuiweka, tumeiweka kwenye electoral commission. Electoral Commission inatakikana itoe civic education kwa wananchi siyo habari yao kura peke yake, lakini mambo mengi ya utawala. Lakini bado tunajua kwamba ikienda mashule itakua inawafaa zaidi wananchi maanake watoto wakisha kuwa wanajua haki zao ni nini. Upande wa vile viti tisaini hiyo ni sawa kusema kwamba vipunguzwe viwe 45 nimesikia hiyo.

Upande wa mama ambaye ameshikwa na mtoto mchanga, nafikiri hiyo kwa detail hatuko nayo lakini tumesema tu kwamba mtoto yeyote mchanga, chini ya umri wa miaka kumi na nane pahali popote alipo, ni lazima apate zile haki zake. Na ndiyo maana tukasema katika prisons hizi cell na prisons tumesema sasa itakuwa ni lazima serikali uhakikishe kwamba haki zote za mwananchi wa kawaida zinapatikana cell godoro zina safi, kama ni kitanda kisafi, chakula chake tumesema pia watibiwe na kama serikali imesma haina pesa pale, jela kama una uwezo uite daktari wako aje akutibu pale tumeandika hiyo. Kwa hivyo tutaangalia hilo swala lakini tuna hakika kwamba tukifuata zile za kibinadamu yule mtoto pia amechukuliwa mambo yake.

Halafu upande wa labour relations bwana Mwangonya ameeleza, hiyo ni sawa tutatilia umuhimu kwamba mtu moja asiwe na uwezo na yeye pia ametaka miaka sitini ya lease. Halafu electoral commission, hilo ni wazo zuri sana kwamba electoral commission nalo lipewe nguvu ya kuweza kuwashtaki wale watu ambao wanaleta fujo kwa sababu sasa ni electoral commission ikiona mtu ipeleke kwa polisi. Polisi naye apeleke mahakamani. Sasa kuna stage tatu pale hapo katikati hutokea kutosikizana hapo tena halafu hiyo kesi inapotea.

Halafu kuna mtu aliuliza habari ya administration police mlikuwa nimesahau kuwaeleza lakini administration police hapo tena (clapping). Itakuwa haipo tutawatia katika regular wale polisi hao wengine ambao tumeanza afresh tutawatia huko tuwe na jeshi moja tu la polisi. Halafu mtu mmoja bwana Lawrence, ameeleza kwamba kuna sheria nyingi ambao ni za kikoloni au sheria ambazo tumezirekebisha pahali pengine zitakuwa zikiendelea. Kwanza kitengo cha kwanza cha hii kinasema sheria zote za Kenya ni lazima ziambatane na katiba. Sasa hiyo ime-solve maneno yote haya. Maanake ni kwamba tutoa muda, tumetoa muda wa miaka miwili kuna tunaita transitional mechanisms, yaani kule kupokezana hii katiba ya zamani na hii katiba mpya. Katika miaka miwili yote sheria zote zitarekebisha kuambatana na hii katiba. Na sheria yeyote ambayo itakuwa kinyume na katiba hii, basi sheria hiyo haifai. Ndiyo first section tumeiandika.

Wellington umesema kuhusu mawaziri kumi na tano, principle yetu tumeiandika lakini hilo kwa neneo hilo tutaliandika wazi. Katika principle yetu ya Kenya tumesema kila uongozi wa kitaifa ni lazima uzingatie eneo, dini, umri, kabila na kadhalika. Kwa hivyo, mawaziri si kweli kwamba kumi na tano kumi watatolea kwa mkoa mmoja lakini kwa sababu ni neno la muhimu sasa sitaenda pale pale penye sehemu ya mawaziri pia tutaandika kwamba mawaziri lazima watoke equally kutoka kila mkoa. Hiyo ni sawa.

Halafu upande wa boundaries, tulisema kwamba sheria imekuweco mpaka sasa hivi sema kwamba sehemu za uwakilishi bungeni au za ma-councillor, madiwani zitabadilishwa kila baada ya miaka kumi. Lakini haiufatwi vile inavyotakikana kwa hivyo tumeweka kikwazo sasa kwamba lazima zitafanyika hivyo hivyo baada ya miaka kumi na electoral commission ndiyo ambayo itaangalia mipango hiyo ilikuwa tume-propose boundaries commission pia bado tunaiangalia. Kwa hivyo itakuwa si sawa mtu kuwekewa constituency kwa sababu aonekana akiweka kule atashindwa akatiwe yake awekwe pale ashinde hiyo itakuwa sasa haiwezekani.

Kuna msemaji bwana Msafiri alikuwa anauliza kuhusu village government, ile serikali ya kijiji tumeona ya kwamba wananchi mtaamua mmepewa uhuru either mfanye uchaguzi wa siri ama mteuwe nyinyi wenyewe. Kwa sababu kijiji ni pale ambapo watu wote wanajuana pale. Sasa mtachagua nyinyi wenyewe wale ambao watasema wafanya uchaguzi tutakubali wale ambao watasema tunateuwa tu mama fulani, mzee fulani, kijana fulani huyo yuwatosha. Haya nyinyi nendeni uamuzi ni wenye wananchi.

Halafu tulikuwa na swala la retired workers NSSF, pesa ambazo zinapotea baada ya miaka fulani tunasema hii ndiyo sababu ya kuleta serikali za mitaani. Sasa kwa hivyo, itakuwa sasa kila organ ya serikali au ya kitaifa lazima itaambatana na vile viwango vile vya serikali kwa hivyo hizi zitakuwa zinapatikana kwa districts. Sio lazima uende Nairobi ndiyo ufuatae NSSF, road licence. Kila kitu kule sasa tumeleta hapa hapa sasa tunashindwa sisi wenyewe.

Haya round ya pili sasa, Bwana Chairman ulikuwa unataka kuuliza swali tafadhali. Uliza halafu tutaenda sasa kwa wale ambao wame ...(inaudible)... wewe bwana hapa na ule mzee wangu wa pili na yule bwana pale wa tatu nitachukua hawa watatu baada ya chairman halafu nitakuja kwa hao wengine kila mtu atapata nafasi.

Cllr. Hamed Mubarak: Mimi ni diwani Hamed Mubarak mwenyekiti wa Kilifi Town Council. Katiba iliyotolewa asilimia themanini katika katiba hii ni katiba ya wakenya na ni maoni ya Kenya. Leo tutakubaliana nanyi ndugu zangu kwamba hakuna nchi hata moja katika dunia nzima ambapo watoto wanakaa nyumbani hawaendi shule. Kenya tunaingia katika record kwamba ni nchi peke katika duniani kwa wiki mbili na nusu watoto hawaend shule na swala hili halishughulikiwi na wale walioshika hatamu za utawala bali wanashughulikia ni nani atapanda kile kiti juu azidi kukanyaga wakenya (clapping).

Tulikuja na Phoebe Asiyu hapa, kuna mambo ambayo tuliyazungumza mengine hayakuwekwa. Katiba hii haikushughulikia sana katika mambo ya uendeshaji na hasa uchaguzi wa mabaraza katika Kenya. Katika ile draft ya katiba, tulikuja tukaongea hapa kuhusu qualification za madiwani kuwa wanaweza kugombania kiti cha udiwani na katika katiba iliyotoka hii draft. Wameshikilia sana upande wa wabunge na rasi na nguvu za watu ziko katika madiwani the lowest political unit. Na tulisema hapa kwamba ikiwa uwezo wote huu unaletwa kwa baraza baadala ya mtu kwenda kukata road licence Nairobi, wapi itakuwa hapa kwenye mabaraza. Kwa hivyo diwani ni lazima awe mtu amesoma, amefika kidato cha nne na katika mfumo wa 8-4-4, tulisema kwamba hata ukichukua manamba a-register mtihani wa kidato cha nne aandike jina lake tu na ile index number atapata E na atapata certificate kwamba amefika kidato cha nne.

Tukasema kuwekwe minimum requirement hata kama ni D, maanake tukiweka juu zaidi kuna wenzetu kule Mandera na kule wataanza kwenda Eastleigh kuuliza Wasomali ambao wamesoma wapigania kura. Iwekwe at least minimum D. Hiyo haikutazamwa na vile terms of office katika draft constitution, tulisema wenyekiti na ma-mayor wachaguliwe na wananchi wamechaguliwa na madiwani. Maanake wakiulizwa leo kwa nini hakuna maji hapa maanake uwezo unakuja kwa mabaraza, hayo hayakuzungumza katika draft constitution. Watu walishikia ngumu katika upande wa ma-judge na nini na nini hayo yote.

Kuna vita vikubwa hivi sasa kuhusu ma-judge na mawakili. Mimi nasema kwa kiswahili ma-judge na mawakili ni mavi na mkojo. Tukisema ma-judge, ni mtu magistrate baadala yeye achaguliwe apande ngazi mpaka afike judge, mtu anachukulia wakili kwa sababu kuna mtu yuko karibu na ikulu ama na rais hasa huyu mtu wangu mchague judge kesho anachaguliwa judge. Na yule ambaye ameanza district magistrate hapandi kule juu. Na hao mawakili pia ambao wapiga kelele kubwa wana katiba zao na nini lakini kwa sera za kulindana asilimia sitini ya mawakili Kenya ni majambazi, wahuni (clapping). Kitu hicho kitazamwe, mmezungumza habari ya ma-judge miaka sitini na tano. Na hao mawakili ambao wananyanyasa wananchi wako wengi na kuwadanganya, haswa watu wanaopata ma-accident na nini, pesa zao hawapewi na nini litazamani jambo hili aliweke.

Vile vile katika katiba hii twataka iandikwe katika katiba miaka mitano kuna uchaguzi kama vile Amerika, tunajua tarehe nane November ni uchaguzi wa rais sio mtu mmoja awe waziri mkuu wa rais aanaza kutubabaisha hatujui tutakufa tunaenda uchaguzi utatajwa ama hautajwi iwekwe kwenye katiba Kenya baada ya miaka mitano kama ni tarehe kumi na tano December baada ya miaka mitano kumi na tano December iwe pale haifutiki (clapping).

Na kitu kingine, hawa tumesema katika katiba hapa twataka nominated members of parliament, wabunge maalum tisaini ukiweka wabunge maalum tisaini hawatachagua mtu ambaye ana uwezo na ana zile qualification za kwenda pale atatazama nani alimunga mkono katika campaign hii, amuweke. Mimi nasema tufanye kama Uganda, Namibia, Zambia kwamba katika wale watakao kubaliwa ni tisaini sitini 35% wawe wanawake (clapping). Maanake mimi naamini kwamba wanaume ni wafisadi zaidi kuliko wanawake. Wanawake wana kauoga. Kwa hivyo kama kutakuwa ni watu sitini watakuwa nominated, ishirini lazima wawe ni wanawake.

Na lingine twataka kuzungumza ni kwamba hizi nguvu nyingi zimepelekwa katika waziri mkuu, katika hii draft constitution yule rais pale ameachwa ni kama ceremonial. Basi ikiwa yule rais atakuwa ceremonial, asiende akapiga kura iwe kama India ama Israel, Uingereza kuwe na waziri mkuu ama Italy. Prime minister awe ndiye anaendesha serikali halafu bunge lichague ceremonial president haina haja kuwa sisi tuende tukapige kura ya rais na rais anakwenda hana mikono hana miguu. Afadhali tupige kura kwa sisi ya prime minister halafu yule ambaye ni ceremonial kama India hata leo ukamuliza mtu rais wa India ni nani hajulikani. Kazi yake ni kukaa ikulu kuchukua karatasi za mabalozi basi na kumpokea rais anayekuja aende hata hampokei aende akamtembelee kama mfungwa. Waziri mkuu ndiye ana power zote kwa hivyo, yule atachaguliwa na bunge wale watakokwenda kwa hivyo tupige kura ya prime minister na running mate wake na wabunge.

Na hili swala la kuchagua watu ambao si wabunge kuwa mawaziri ni jambo nzuri sana lakini, liwe ina mipaka. Kama mmesema mwataka mawaziri wawe kumi na tano mimi nasema wawe kumi na nane. Katika kumi na nane wale, yule waziri mkuu watakayechagua apewe sita awachagua kutoka kwa watu wa kawaida ama sasa si aambiwe achague aweza kuchagua wote. Sita kwa nii hatusemi wabunge wote wawe nominated twatoa kiwango fulani, basi na waziri pia naye apewe watu saba ama sita watakavyo kubaliana wao watachaguliwa kutoka kwa watu binafsi si lazima wawe wabunge na wengine lazima wawe wabunge.

Nasema kwa hayo machache nasema asante sana (clapping).

Com. Swazuri: Asante sana nilikuwa nimesma nani baada yake?

Interjection: Huyu hapa.

Jason Auko: Kwa jina naitwa Jason Auko. Mimi ningetoa pendekezo langu kwa katiba mmesema, mimi sina mengi sana kwa hii katiba maanake naona mmefanya kazi vile mlivyozunguka Kenya nzima, mkachukua maoni ya wananchi wa tabaka mbali mbali. Mmetuletea hapa na tukasoma na tukaelewa vizuri sana. Mimi ningesema jambo lingine kwa idara hii ya polisi, wawe na heshima kidogo hata kama mwananchi wa kawaida amefanya kosa wanaweza kumuendea nyumbani na wakimpata, saa zile bibi yake anamwekea chakula kidogo wamuache ale sio ati wanamchukua wanampeleka kule kama punda mpaka ijumaa ama jumatatu ndiyo apelekwe kortini. Hayo ni matatizo tunaona sana mtu anawacha chakula nyumbani yuko juu ya meza yeye anachukuliwa juu juu yaani... lakini ile heshima pale amepewa na hata wala hataki kutoroka.

Ya pili mimi ningeomba hii katiba ama hii tume, waende ama waangalie mbinu zozote zile za kusaidia wananchi wa kawaida kwa hizo upande wa magari. Maanake wananchi wengi Kenya hii imefikia kiwango cha kwamba imeenda juu mpaka wananchi hawana hata pesa ya kununua baiskeli. Sasa unakuta mtu amenunua gari hata kama wewe uko na mgonjwa anakupita tu, na yeye ni mtu jirani wako saa ingine. Tungeomba kule wananunua hizo magari, itolewe percentage fulani ambazo inaweza kuwa tuna ruhusa ya kuwaomba na watusikize kama wananchi wasaidie hawa hawana uwezo (Luo dialect) (laughing).

Tena ningeomba kwa upande wa barabara, kuna watu wamebahatika na wakanunua baiskeli, na kule barabarani hatambuliki kabisa. Unakuta yule mwenye gari anakuja kumfyeka tu. Tunataka barabara iwe wazi kwa hao watu ambao wako na baiskeli zao, hata akionekana yaani afanyiwe overtaking vile anaweza kufanyia gari, sio ati yeye akanyagwe tu halafu pesa yake hata ya nini hapati yule mwenye gari ameenda zake. Kwa hivyo mwananchi yule anateseka sana. Asante sana.

Com. Swazuri: Wa pili alikuwa ni nani? Yule mzee wangu pale wa Miwani.

Hamilton Baya: Mimi naitwa Hamilton Baya. Yangu ni machache sana tu. Kwanza nashukuru katiba ni mzuri isipokuwa kitu kimoja ambacho tunaomba katiba ya zamani nafikiri haikuzungumzwa mahali popote lakini hii ime-set record kwamba kila mmoja anaweza kuzungumza. Mmesema lugha za katiba ni mbili, kizungu na kiswahili. Tunaomba kwamba hii katiba iwe katika language zote mbili kizungu na kiswahili na ifanywe kwamba kila mmoja anaweza kuifikia isiwekwe tu katika government printers halafu kila mmoja aende Nairobi kununua. Bali iwe katika locational level kuna mahali ambapo mtu aweza kuenda kupata hiyo katiba akaisoma. Na pia ifundishwe shule watoto wa shule wajue kutoka nursery wajue hiyo katiba yao ni nini.

Kitu kingine nilikuwa nazungumza habari ya huyu public defender. Huyu ni mtu muhimu sana, na kama huyu nafikiri hangekuwa

tu katika central point angekuwa powers zake ziko hata katika sub-location level ana katika village. Hii ni kwamba nimekosana na askari hapa anaweza kukimbia kwa huyu mtu nikamwambia bwana mambo yameharibika hivi naweza kifka mpaka kule ambako yanatakikana.

Jambo jingine ambalo ningezungumza ni kwamba habari ya national youth service, sioni kama mumeweza kui-cover iko mahali popote katika constitution kama iko basi sijui. Naitonal youth service ni service ambayo ni nzuri na hasa kwa vijana. Na ni jambo ambalo pengine kama ningewekwa mkazo lingesaidia nchi yetu kwa sababu vile watoto wangejua kutoka mwanzo lile la kufanya. Na hasa ni watoto wadogo mtoto wa kama miaka kumi na saba kumi na nane wamemaliza standard eight, ni aibu kwamba watoto hawa ijapokuwa hiyo national youth service ingesaidia vijana lakini watoto hawa hata wakienda kule katika national utakuta wanawachwa hivyo ovyo ovyo baadaye hata wanaweza kuwa drops ikawa sasa kitu kingine sasa amekaa nyumbani anatafuta kazi.

Ingekuwa muhimu kwamba wale vijana wakienda katika national youth service wanaweza kuangaliwa hata kupewa katika kuingia katika course fulani za ufundi. Kama udaktari ama u-nurse ile ya kutoka pahali tayari wako absorbed katika kazi lakini sasa hapa utakuta tu wamekaa national youth service. Leo anaambiwa kuna u-polisi anakuja tena uwanjani anakimbia mbio mpaka akitoka hapa amechoka. Tena anaambiwa umewachwa na hali alikuwa national youth service ni aibu sana kwa watoto na tungetaka kwamba kuwe na njia ambazo vijana hawa tunaweza kuafikira badala ya kuwatakana kama sisi tunawatakukana asante sana.

Bakari Salim Bakari: Kwa jina naitwa Bakari Salim Bakari. Pendekezo langu nawaomba katika katiba wafanyakazi wa biashara ndogo waacha kutozwa ushuru. Maanake uchumi wa Kenya uko chini. Mtu anatafuta ...(inaudible)...kwa watoto wake. Anatakikana alipe pesa kwa council ama kwa serikali hana uwezo. Sina mengi ni hayo tu.

Charles Kulala: Kwa jina naitwa Charles Kulala. Ninapendekezo kuna kitu ambacho imenikera sana katika maisha yangu, kuhusu mambo ya kuniita serikali na sijui mimi ni serikali kivi. Basi hapo, nimeitwa mimi ni serikali na ninapotentemba njiani mahali hakuna magari ninapopitwa na gari ya government of Kenya nikisimamisha haiwezi kunibeba. Naambiwa mimi ni serikali hiyo ni gari yangu hasa nayo hapo inanipita hiyo gari ni yangu kivi kama mimi ni serikali kweli mbona napitwa na gari (clapping).

Pili, kuna sehemu ingine pia inanitatiza mimi kama mwanakenya nimepigwa njiani na wahuni na nikajaribu kufanya speed na mguu wangu ukani-serve, nimekimbia mpaka polisi. Kufika polisi ninaambiwa gari haina mafuta, kule nimepokonywa hela mpaka hata huku nimeponea chupu chupu wallet yangu imebaki huku naambiwa nitoe pesa ya mafuta ndiyo gari akashike wale watu ambao wamenipiga hapo katika katiba itanisaidia vipi? Sawa. Asanteni sana.

Com. Swazuri: Mwingine pale nyuma, halafu hiyo mwingine tukimaliza tafadhali songea karibu ambapo unaweza kufikiwa.

James Otieno: Kwa jina naitwa James Otieno. Mimi nina maneno mawili. Kwanza nitawashukuru sana kwa ile kazi ambayo mmefanya ya kutuletea katiba mpya ambayo ni yetu. Na swali langu ni moja tu, katika neno langu la pili ni ya kwamba katiba tumepewa lakini starehe zetu hatujapewa. Hata shule lazima kuwe na kiwanja ya mpira na wazee baada ya kazi wanapenda kuburudika. Kuna wale wanaenda kwa ma-bar wengine wanataka kunywa mnazi na huku polisi wanatarajika sana kuhusu haya maneno ya pombe mnasema ni haramu. Sasa hii katiba mpya, starehe zetu tumekubaliwa ama zimekatazwa. Hilo ndilo swali (laughing and clapping).

Com. Swazuri: Katiba haikutaja hiyo.

Salim Maalim: Kwa jina langu naitwa Saalim Maalim Mzee. Swali langu nauliza hivi, kuhusu swala la NSSF ambalo kwa ufupi sikuelewa vizuri sana. Na ninataka kuelewa kwa nini ile NSSF mtu aki-retire hawezi kulipwa hapo kwa hapo saa ile amefutwa kazi alipwe hapo kwa hapo mpaka angoje baada ya miaka kadha ama kwa nini hapatiwi baada ya wiki mbili hivi akapatiwa pesa zake kiharaka.

Samson Hassan Ndor: Kwa majina naitwa Samson Hassan Ndor. Nilikuwa nina pendekezo kwamba, ukiangalia hata hapa tulipo utakuta kuna watu wengi hawana kazi. Lakini utakuta Kenya hii kuna wengine wanafanya kazi hata tano na wanalipwa. Kwa hivyo, pendekezo langu kama katiba mpya ingependekeza kwamba hapa Kenya mtu mmoja kazi moja. Nafikiria tungesaidika sana. asante (clapping).

Nzingo Gahal: Mimi jina langu naitwa Nzingo Gahal kutoka Kisumu ndogo. Upande huo ni mama wa mtaa. Mimi nikifikiria hyo katiba vile inageuzwa lakini kuna mambo mengine ambayo pia sikusikia kwamba hayo yamegeuzwa.

Jambo la kwanza, kuna misaada ambayo inatoka kwa serikali hapa Bahari shule za hapa zote haziwezi kupata hiyo misaada. Misaada inaenda nje na hapa ndiyo shinani. Kitu kama hicho kinakutatiza sana.

Jambo lingine vile vile huwa tunaambiwa tuandike majina watoto ambao wamezaliwa na wazazi wao, na watoto ambao wana vilema na sisi kama viongozi wa mitaa ndiyo tunaona wale watoto ambao tunajua kabisa hawa hawajiwezi au baba na mama wamekufa hata baba hata watoto uandike list upeleke. Ukiangalia msaada utapatiwa mtoto mmoja tu wale wengine wote hawatapata. Mambo kama hayo pia yanatutatiza.

Jambo lingine ni kuhusu hawa viongozi wetu ambao ni macho yetu. Utakuta kuna mbunge na councillors ambao watu kama hao ni sawa wawe ofisi moja. Maanake huyu councillor huwa anachukua ripoti zetu sisi huku, anapeleka kwa mbunge. Sasa unakuta councillor amefanya kazi yake ya u-councillor, halafu anachukua ya ubunge anafanya yeye. Yule mbunge kazi yake hafanyi kabisa hata hawakutani baada ya miaka mitatu miaka minne, hiyo hatuijui huko nyuma hatukuiona na kwanini inakuwa hivyo.

Hivyo wanataka viti na unaona ni kama wanapigana, lakini wakipata tu basi hata hawakutani tena mpaka miaka mitano. Sasa watapanga nini? Utakuta shida zinajaa watoto wamemaliza masomo hawana kazi mambo kama hayo. Sisi tumechoka iangaliwe sana. hayo machache Mungu ayabariki.

Interjection: Tuwafute ...(inaudible)... ndiye huyu hapa ...(inaudible)...

Clr. Mwinyi: Mimi naitwa Councillor Mwinyi haji ni mmoja katika wale waakilishi wa Kilifi District ambao watawakilisha katika kongomano la kitaifa. Kwa hivyo bwana Mwanginya niko hapa kusikiza maoni yenu ili niende niyasaidie huko mbele. Haya ni maoni yangu ambayo ninazungumza. Kuna Upper House na Lower House ambayo imezungumziwa huko juu kuhusiana na mabunge mawili. Vile tumesema tumepata pengine kutakuwa na conflict ya interest ikiwa kutakuwa na Upper House na Lower House. Kisha tunarudi tena council ya mkoa, district na kijiji sas tunashangaa hayo mabunge mawili huko juu sijui kazi yao hasa ni nini. Tungependa kuwe na bunge moja tu ambao litakuwa lina-represent hao walioko huko.

Halafu lingine labda swala la kuzungumza, ni elimu yetu ya 8-4-4. Tunasema 8-4-4. Pengine ingekuwa inazungumziwa ni mfumo gani wa elimu ambao tungekuwa inatusaidia hapa Kenya na ikawekwa kwa katiba. Na mwisho ningesema uchaguzi uende kwa katiba mpya asante.

Harrison Karisa: Jina langu ni Harrison Karisa. Mimi niko na maoni mawili. Kuhusiana na swala la kwanza ni ardhi na swala la pili ni kuhusu hazi za wanawake. Maoni yangu kuhusu ule uwezo kwa ile tume ya ardhi, ni kwamba ingekuwa vizuri waangalie sana kuhusu hili swala la ardhi. Kwa sababu tunakuta wengi wamejiletea matatizo wenyewe, wengine wamepewa ardhi halafu wakaanza kuziuzua sasa wanabaki wanaangaika wale watoto wanahangaika kwa hivyo hata iwapo hizi ardhi zitarudihswa kwa wenyewe, lakini ile tume ambayo itakuwa ni ya kijiji iwe ikiangalia sana wale wazee ambo huza ardhi bila mpango wawe wakiangaliwa.

Halafu swala lingine kuhusiana na haki za wanawake. Nafikiri haikufanuliwa wale wasichana, wasichana tunaona wana matatizo makubwa kwa sababu msichana unaweza kuona amepata mimba halafu na ule kijana anamtoroka anabaki na kulea mtoto.

Emmanuel S. Safari: Ndiyo wanakosa elimu kwa sababu hawana msaada wa kutoka kwa wazazi wawili. Kwa hivyo hili sawala liangaliwe liwekwe mahali fulani katika ile child abuse. Asanteni.

Com. Swazuri: Haya wacha tujibu hapa halafu tutakuja kwa round ingine. Nimekuona mama nitakupatia nafasi. Councillor, Bwana Hamed, chairman ameondoka lakini ametupatia mapendekezo mengi. Kwanza kuhusu qualifications za madiwani hizo kweli tutaziandika. Lakini tumesema ya kwamba madiwani kwa upande wa districts ambazo sio urban area tumesema madiwani sasa nafasi yao imechukuliwa na lile bunge la districts ile serikali ya wilaya. Kwa hivyo hakuwa chairman wa county council ni

yule (clapping). Chairman wa county council hayuko, alioko ni governor wa district au district administrator na huyo atachaguliwa direct na wananchi na hiyo nimeeleza hiyo (clapping).

Akauliza tutafanya nini kuhusu mawakili ambao pia hao ni wakora kama alivyosema yeye. Nafikiri sheria iko ingawaje haijaitiliwa mkazo lakini sheria iko ya deal na watu kama hao. Mkikumbuka upande wa malalamiko ya wananchi ya kwamba pesa zao za ajali za insurance walikuwa hawapati nafikiri kulikuwa na mgogoro sheria ikapitishwa kwamba ile cheque lazima iandikwe kwa jina la yule mteja. Kukatokea mgogoro baina ya wale waliandika sheria na wale wanasheria hata sijui mgogoro huo umefika wapi lakini kulikuwa na hali ya kurekebisha kwa sababu kweli ni wananchi wengi huwa hawapati malipo yao. Kwa hivyo hiyo ni sheria ambayo ni lazima itiliwe mkazo.

Amesema pia siku ya uchaguzi iandikwe katika katiba. Sisi tumeiandika tumeweka nafasi yake hapa. Sisi tulikuwa tumependekeza ya kwamba uchaguzi uwe unafanya kila jumanne ya kwanza ya mwezi wa nane. Kila jumanne ya kwanza basi itakuwa ni siku ya tarehe mbili, ishirini yaani tarehe tatu, tano lakini jumanne ya kwanza ya mwezi wa nane. Hapa tumeandika in brackets maanake hatujakubaliwa kwamba tuseme uchaguzi huu utakuwa lini wala lini na tumesema hata kama uchaguzi huu utakuwa lini au lini natunasema hata uchaguzi huu utakuwa lini au lini na tunasema uchaguzi huu utafanyika hivi sasa bunge hili litakuwa na muda mrefu zaidi tutaliongeza miezi mitano zaidi kwa sababu yule mwingine uje jumanne ya kwanza ya miaka mitano kila miaka mitano jumanne ya kwanza na ya mwezi wa nane. Na tumetoa mwezi wa nane makusudi kwa sababu tumekuta mwezi wa kumi na mbili huwa ni kwa wakati kuna masherehe mengi siku kuu nyingi. Halafu wazazi wengi huwa wanashughulika na mambo ya mtihani ya watoto halafu campaign inaingilia katikati pale tukasema hiyo tuondoe kule tuweke hapa mwezi wa nane. Kwa hivyo tarehe itakuweko na katiba ikipitisha hakuna mtu anaweza kupita hiyo tarehe itakuweko.

Halafu wakaeleza habari ya wale wananchama wa wabunge ambayo watakuwa nominated, wabunge tisaini katika sheria ya hapa tumefanya ya kwamba kila chama ambacho kitakuwa kimepata viti katika bunge, kitakuwa na party list kitakuwa na majina ya wale wajumbe wao ambao watawachagua kutokana na priority, lakini nimesema hapa wa kwanza ikiwa ni mke wa pili ni mume watatu ni mke wa nne mume alternate namna hivyo. Kwa hivyo wakisema tutachukua wa kwanza watakuwa ni kumi wanawake kumi wanaume wakisema watachukua saba wa kwanza wanne ni wanaume watatu namna hiyo.

Halafu akaeleza habari ya rais na waziri mkuu kwamba tunachagua rais lakini hana nguvu. Halafu waziri mkuu ambaye ana nguvu anachaguliwa na bunge. Kwa vyovyote tutakavyofanya lazima moja awe juu mwingine awe chini sisi tumeamua hapa kwa sababu malalamiko ya mwananchi sio waziri mkuu. Waziri mkuu alikuwa hakuna, tuliambiwa tusikize malalamiko ya wananchi mawazo ya wananchi ni rais ofisi ya rais ina nguvu zaidi kwa katiba ya sasa tupunguze, tumeipunguza hivyo. Sasa huwezi kupunguza ukaziwacha hivi hivi, maanake ni kazi lazima zifanyiwe zile na mtu fulani ndiyo tukapunguza tukaweka kwa waziri mkuu na bunge na hizi serikali zingine za chini. Kwa hivyo hata tukisema tuchagueni waziri mkuu lazima kuna rais achaguliwe. Na mawaziri akapendekeza wawe kumi na nane baadala ya kumi na tano. Hilo ni pendekezo tutalichukua, lakini tulisema kwamba wizara zikiwa nyingi mawaziri wakiwa wengi pia nazo huwa ni shida. Hakufanyiki kazi halafu wizara nyingine zinafaa

kuwa ni idara katika wizara nyingine kwa hivyo zitengenezwe kama basi atafanya vipi lakini ziwe kumi na tano.

Halafu habari ya mzee wangu hapa amesema wakati wala chakula askari anaingia, hawakungojea pia ukamaliza chakula ukavaa suruali nzuri wengine hupelekwa pia na shuka cell. Tumesema kwamba katika sheria zile tuliziandika, haki za mtu ambaye anashikwa anashukiwa hayo sasa hayapo tena. Tumesema ni lazima ikiwa ni mtu ameshukiwa ameshikwa apelekwe ndani lakini katika masaa arobaini na nane ni lazima awe kortini bila ya hivyo sasa tutamshtaki. Yule alimshtaki public defender hayuko.

Upande wa baiskeli nafikiri hiyo ni Traffic Act iko wazi kabisa kwenye baiskeli inafaa kuendesha baiskeli yako ana sheria za barabarani. Halafu mzee Baya, hii katiba tumekuja nayo ni ya kingereza lakini kama nilivyosema tumeacha watu wakifanya tafsiri muda ulikuwa hautoshi kufanya tafsiri lakini ipo itakuja na bwana Mwaiunga ataita katiba ya kiswahili. Tumesema lugha ziwe mbili kingereza na kiswahili lakini official language, national language yetu ni kiswahili kwa hivyo tutaleta zile katiba kwa lugha ya kiswahili. Hata huu mswada naona uko pia katika lugha ya kiswahili ile short version ile ripoti yetu iko ya kingereza na pia tumeleta ya kiswahili ingawaje nakala zake ni kidogo sana tutazileta nyingi zaidi. Na tumesema ifundishwe shuleni nimesema pale mwanzo tutaangalia hapo tuweke na iwe inapatikana kila mahali hilo pia tumeliweka.

Yule public defender, yule mtu anaweza kwenda kushitaki mtu wa serikali mfanyikazi wa uma tumesema awe na branches mpaka chini. Sio kwamba lazima uende Mombasa au Kilifi peke yake tumesema iwe na branches mpaka district mpaka chini huko. Mtu anaweza kushitaki wakati wowote. National Youth Service ni kweli hatukuiangalia kwa hivyo tutaangalia pahali pake.

Small businesses, wenye biashara ndogo ndogo Bwana Bakari amesema wasitozwe kodi kiholela holela. Tumeandika pale kodi yoyote lazima ipitie bunge. Charles ameuliza serikali ni nani? Mimi naambiwa serikali ni wewe lakini nikiona gari ya serikali siwezi kupanda. Ni kweli kwamba ni hivyo, lakini maana ya kuambiwa serikali ni yako wewe ni kwa sababu hii yako wewe ni kwa sababu hii katiba umeiandika wewe halafu mamlaka yoyote hawa wafanyikazi wa serikali. Mamlaka yote wameyatoa kwa niaba yako wewe. Hawawezi kuenda pale isipokuwa wewe kwa sababu wewe ndiwe unalipa. Serikali haina njia nyingine ya kutafuta pesa lakini ni kwako wewe, lazima itachukua ushuru kwako wewe.

Kwa hivyo tunasema kwa sababu hiyo uwe na nguvu zaidi ya zile pesa zako unatozwa uwe unaweza kusema mimi ninataka hivi, uwe unachagua kiongozi fulani. Nataka hivi na iwe hivyo. Sasa wale wafanyikazi wa serikali tukishawapatia zile kazi ni lazima watekeleze ndiyo maana tunawanunulia gari. Sasa tukisema zile gari za wale watekelezaji, wale watumwa wenu sasa ziwe kila mtu akitaka yuwapanda sasa ni sawa maanake zitaharibika mara moja mapema halafu itakuwa kila siku tunanunua gari. Kwa hivyo sisi tunasema serikali ni yako maanake wewe ndiyo haya mamlaka yote kama si wewe hao hawana mamlaka. Ndiyo maana tukatoa nafasi kwamba kiongozi yeyote katika katiba hii atakayechaguliwa na wananchi, kama hafanyi kazi yake kiongozi huyo ataenda. Hizo ndiyo serikali yako hiyo unayo sasa.

Mambo ya nazi nafikiri tumesema tutakwenda kuyaingiza kwamba na sio mnazi peke yake kuna watu wa busaa, muratina, chang'aa pia walisema. Kuna nyingine zina shida kuna kumi kumi zinaua watu hatuwezi kuhalalisha vitu kama hivyo. Lakini kuna nyingine watu wamesema kwamba ndiyo uchumi wao sana. Tuliambiwa tofauti ni kwamba mnazi huwa unagemwa, hautengenezi wewe mwenyewe ukifika ukienda ukitega pale tayari sio kwamba una mix chemical ama ni vipi? Iwe inatokea kwa hivyo wenyewe wamesema ni natural iangaliwe.

Upande wa zile pesa za NSSF, kwanza sheria siku hizi imerekebishwa ya NSSF pesa zinatakikana zilipwe haraka inavyowezekana ni utekelezaji tu ndiyo hakuna lakini sheria sasa imerekebishwa. Na ukiangalia NSSF, huwa wanatoa ripoti yao kila mwezi huwa wanatoa kuonyesha wamelipa watu wangapi wanadai watu wangapi kwa hivyo hiyo ni improvement kubwa sana.

Kazi moja mtu mmoja tukiangalia swala hili lakini tukakuta kwamba tumetoa uhuru wa watu kufanya mambo fulani hatuwezi kuwapokonya teana kusema kwamba usifanye kitu fulani. Halafu pili hizi kazi zinazosemwa ni kazi za kuchaguliwa sio za kuandikwa hawa ambao wana kazi nyingi hawa. Na wamepewa wamechaguliwa na wananchi kwa sababu wananchi wanakuta fulani yuwafaa fulani si wa mambo haya. Kwa hivyo tunawapatia uhuru hao wenyewe wakuwachagua. Ikiwa wenyewe watasema tayari ni chairman wa board mbili hatutaki basi hawezi kupigania yeye. Kwa hivyo tukisema kwamba sidhani kwamba kuna mtu ambaye ameandikwa kazi Kilindini halafu mtu huyo anafanya kazi power. Hakuna sijaona mtu kama huyo hata yeye atashangaa hata yeye mwenyewe. Hizi kazi tunasema ni uongozi na uongozi wengine wanakipaji cha uongozi huwezi kuwanyima ikiwa mtu amechaguliwa hapa halafu watu wa kwao wamesema hivyo lazima awe chairman wetu wa kijiji huwezi kuwagawa shauri yenu, huyu tunamchukua hapa.

Halafu kuna mama amesema pale kwamba kuna misaada mingi haifiki serikalini sasa haya mambo ya misaada tumeyaweka upande wa serikali hizi za chini sasa. Maanake ni majukumu yao sasa kuangalia serikali za chini wao ndiyo watekelezaji wa haya mambo ya misaada, bursaries, watoto wale orphan children sasa ni jukumu la serikali kuwangalia.

Umeeleza kwamba wabunge na ma-councillors wananga'nga'na halafu wakati wa kupata kura hawapatikani. Sasa tumesaidia kwa kusema kuwa ikiwa watakuja wafanye campaign hapa mwapatie halafu hamuwaoni, sasa mnawatoa sheira iko sasa. Kama kwa mfano tumesema lazima wabunge kazi yao sasa ni full-time sio ile jumatatu mpaka alhamisi ndiyo la sasa ni jumatatu mpaka ijumaa full-time. Na ground moja ni kwamba kama haudhurui yeye anataka kutolewa sasa kama hamwoni yeye hafanyi kazi yake. Mmepewa ruhusa sasa kukutana na wenzako wazungumze mkifika ile idadi inayotakikaka kutia sign basi mambo kwisha.

Kisha bwana mmoja mwenye haji akaeleza kuhusu kwamba anataka chamber moja, tuliangalia sana hayo mambo lakini wananchi wengi walisema kwamba wanataka kuwe na chamber mbili. Kwa sababu walisema hii chamber moja hupitisha mambo haraka haraka yenyewe kama yajifaa mambo yale kwa wao. Nafikiri wananchi walisema hivyo, ili kuzuia hii kazi tabia

hii sasa tuweke chamber pale ambaye ina waakilishi kutoka wilaya iseme hapana nyinyi mtaongeza aje kitu kama hicho mara moja jii kwa hivyo hiyo ni checks and balances. Tumesema tunataka checks and balances, hata huyu waziri mkuu ambaye watu wanafikira tumempa nguvu nyingi, hana nguvu yeye bila ya bunge hata akitaka nini lakini mpaka aende kule tana ipatikane, two thirds katika Lower House na two thirds katika Upper House ndiyo waziri mkuu ndiyo aseme mimi nimeaumua kitu fulani. Tumeiweka hii kwa sababu tumeona watu wengi ukimwachia power mtu mmoja au fisi moja huwa zinakuwa abused na hatutaki kufanya experiment tena na wakenya.

Land commission, uangalie upande wale ambao wameuza mashamba wenyewe nafikiri sasa hiyo nimesema pale mwanzo, mlikuwa mnalilia serikali za mitaani, majimbo, serikali za majimbo zimeletwa. Sasa nyinyi wenyewe mtauza mashamba kwa bei ya shilingi mia moja sasa makosa ni yenu, kama mtauza kwa milioni moja faida ni kwenu, kama hamtauza uamuzi ni wenu. Sasa serikali ni kama katiba imesema kila kitu ni uamuzi nyinyi wenyewe. Msije mkalaumu mtu mkasema kwamba nimeambiwa na mtu mkasema nimeambiwa niuze sasa uamuzi ni wenu wenyewe.

Wananawake wamesema kuna wasichana swali hili nafikiri tuliulizwa pia jana kwamba kuna wale wasichana, wavulana ambao hao wanaume hutunga mimba wasichana halafu wakaingia gizani. Sasa tumesema hii sheria ambayo lazima tuingalie hatujaiandika kiwazi, tumeindika kwa upande wa right lakini hatujaiandika kiwazi kwa hivyo tutaiandika vile mnavyotaka.

Haya round ingine sasa. Nitaanza na mzee wangu hapa halafu sasa nataka mzee hapa, wazee. Halafu kule nyuma yule kijana mwenye kofia watatu wa kwanza kuna mwingine ambaye ameinua mkono tangu kitambo wewe nakuona. Sasa huyo mzee hapo haya, sasa kila mtu atasema.

Alex B. K. Mzerahi: Asante sana wananchi. Naitwa Alex Mzerahi na ni chairman wa skuli hii kwa parents na pia nafanya kazi na shirika lisilo la serikali la MIDO. Mimi nilikuwa na matano lakini matatu yashazungumziwa na singetaka kuchukuwa nafasi ya mtu mwingine, lakini mawili bado kuzungumza. Moja ni habari ya wazee najua mumesema kuwa kuna kipengele ambacho kinashughulikia mambo ya wazee sijakisoma lakini swali langu mimi ama ombi langu mimi ni kuwa kuna wazee hapa wengi ambao wame-retire miaka ishirini iliyopita ni ile ile. Na ile kazi ambayo alikuwa akifanya yule ambaye alichukua pahali pake yuwaendelea kuongezewa kila mwaka. Je, katika kipengele hicho cha wazee kuna pahali ambapo kidogo wanasaidika maana hali ya uchumi inazidi kuzorota. Sasa kwa hivyo wakiwa wanaweza kuwa kuna kipengele cha kuwasaidia kuongezewa ongezeewa nafikiri itakuwa ni vizuri sana.

Lingine ni habari ya mashirika yasiyo ya kiserikali, non-government organisations. Sijui sijasoma sawa sawa lakini kama hawa kushughulikiwa mimi ningepomba waweze kuingiziwa na kuweza kushughulikiwa ili waweze kujua kuwa wao nao wanalindwa na katiba. Asante.

Justus Kahindi Katana: Jina langu naitwa Justus Kahindi Katana. Mimi shida yangu ambayo nataka kuuliza, ni kuhusu hawa

wanyama wa porini na wa majini. Kuna wanyama wa porini ambao wanamaliza mimea ya watu katika mashamba, na ukizungumza kwa serikali unaambiwa hiyo itachunguzwa na utalipwa kama imeliwa. Na kuna wengine wanaenda kwa kuuawa mtu ameuawa na wale wanyama msituni akisema wanansema ngojeni tuatchunguza na hakuna mtu mmoja hata ambaye amelipwa. Hapo tunaona ya kwamba hayo mambo inazoroteshwa sana. Wengine ni wanyama wa majini kwenye mito watu wanamalizwa na mamba. Na akienda kwa shughuli ya kwamba anaenda kwa serikali wale watu wa wildlife wanasema kwamba hayo mambo tutayachunguza na hakuna kitu kinachoendelea. Je tutafanya vipi hata tulipwe? Mambo yamekwisha.

Com. Swazuri: Na yule pale ...(inaudible)... haya wewe halafu tuje hapa katikati hapa kwa wazee.... (inaudible)... njoo mara moja hapa.

Bernard Makuri: Kwa jina naitwa Bernard Makuri. Mimi naishi hapa Kilifi na shughuli zangu nafanyia hapa Kilifi. Lakini, kwa maoni yangu katika katiba hii mpya hii sisi tumeteseka sana na hii katiba ya zamani na kama hayo mambo itatekelezwa kulingana na vile tulivyosikia hiyo katiba mpya kila mtu atanufaika. Lakini tunataka tujue mtu anaitwa maskini, hiyo serikali imepita haikutambua mtu alikuwa akiitwa maskini. Lakini saa hii tunataka tuone kwamba masikini anatambuliwa kama kawaida. Kwa sababu chochote kinatendeka hapa masikini ndiyo wa kwanza kuitwa na hakuna kitu kinatekelezwa. Utaona masikini anahangaika njiani akitafuta huku na huku, amefukuzwa hapa mambo ya squatter, mambo mengine na hakuna kitu kinatambulikana kwa serikali. Kwa hivyo kama itawezekana serikali iangalie, hii katiba mpya kuhusu mambo ya squatter, kuhusu mambo ya masikini na mambo mengine. Sina zaidi.

Com. Swazuri: Ni nani yule mwingine ...(inaudible)... Mwingine kuna watu wanatafuta hayo nyote wawili hapo wewe halafu ..(inaudible)...

Hamisi Juma: Mimi naitwa Hamisi Juma. Kitu ambacho nitachangia ni habari ya squatter wa pwani. Nasikitika kwamba Kenya tumepata uhuru kitambo lakini sisi ni watu wa pwani peke yake ndiyo ma-squatter. Hiyo tu ndiyo swali nataka kuuliza.

Andrew Kai: Mimi jina langu naitwa Andrew Kai. Kuna mambo mawili au matatu ambayo ningetaka niulize hapa. Jambo la kwanza tumezungumza habari ya hawa councils za villages hizi na district. Hawa wazee wa mitaa watakuwa wanalipwa au hawalipwi. Maanake wasipolipwa, ile corruption ambayo tunazungumzia tunataka kuiiondoa haitaondoka. Jambo lingine ni kwa hiyo shauri ya recruitment ya watu ambao wanakwenda katika majeshi au skuli za utabibu, yaani recruitment ya zile taslimu ambazo watu wanachukuliwa kwa serikali. Mara nyingi watu wanachukuliwa lakini sisi watu wa pwani hapa tunachukuliwa kisha tukishafika huko juu tunaambiwa hatuku-qualify. Sasa jambo hilo mimi nataka liangaliwe maanake nafikiri kila mkoa huwa na quarter yake sasa ile quarter yetu iliwa wale watu wetu wanaondolewa huwa inakwenda wapi?

Jambo lingine ni juu ya hawa refugees. Refugees katika nchi ingine nimeona kwamba kuna watu kama hawa wanawekewa camps, sijui kama limetajwa katika hii katiba mpya. Lakini ninavyofahamu ni kwamba kila nchi wale wageni wanapokuja

huwekewa au kutengwa mahali ambapo wanawekwa. Lakini leo katika Kenya hii, utakuta hata katika vitongoni hapa Kilifi utakuta hata refugees wako. Na hili jambo lisipoangaliwa vizuri litaleta hatari kubwa kwa wananchi. Kwa hivyo ningetaka jambo hili kwa katiba mpya liwe linaangaliwa na kuwe na mwafaka mzuri ambao utaandikwa ili wale refugees wanapokuja wasiwe wanaketi vitongojini na kuleta mabunduki zao na nini hawa watu mwisho watakuja kutuua sisi hapa.

Interjection:(inaudible)...

Com. Swazuri: Kuna wazee wamekuja kutoka kitambo halafu tutakuja kwenu kwa mama tafadhalini.

Daniel O. Mwangome: Asante jina langu ni Daniel. Nilikuwa na maswali mawili kuhusu elimu imetajwa kwa wafuadhi sasa ama katiba inaruhusu watoto wasome na ni lazima na ni wazazi wasipoleta watoto kwenye shule watapata ijara yao. Sasa kitu ni kwamba, elimu iko hapa ya primary hata ya chuo cha upili. Ajabu ni kwamba mpaka tangu ajadi ya elimu mpaka leo hatujapata hata university moja hapa, tunataka hivyo iweko kwenye katiba (clapping).

Taratibu za elimu. Pili ni kwamba mara nyingi watoto wetu wanafukuzwa huko university wanaambiwa hapati ile loan sawasawa. Na loan hizi ukiangalia mtoto wa waziri wangu anapata 100%, lakini mtoto wa masikini hapa atafukuzwa shule hapati bursary kabisa. Nimeona na nimesikia na nimeona na jicho langu na sikio langu limesikia. Kwa nini inakuwa hivyo katika katiba? Tungependekeza watoto wa masikini kwanza, wawekwe nafasi ya kwanza katika bursary ama loan higher education loans board (clapping).

Samuel Kadenge: Mimi jina langu naitwa Samuel Kadenge Wanje matano manne. Mimi langu la kwanza lilikuwa ni kuunga mkono wazee wa vijiji. Sababu wazee wa vijiji, wanafanya kazi ngumu anaweza kuzunguka kutoka asubuhi mpaka kuitwa ile kazi hataimaliza kesho anairudia hiyo kazi kuzunguka kusema mikutano hata aweza kumaliza kwa siku tatu ama nne ndiyo akamaliza ile kazi ya kuzunguka. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nataka walipwe tena kitu kingine ambacho nilikuwa nikianza kuzungumza ilikuwa wao wapate uniform ili watambulike wapate uniform. Ingawaje hawatakuwa wengi kama ilivyotajwa kwamba kila kijiji wawe kumi. Ingawaje kama itakuwa kama watano, lakini wawe wanapata uniform wajulikane maana sababu wanafanya kazi ngumu sio kuachwa hivi hivi kwa hivyo mimi kwa sababu kazi nilikuwa nimeifanya vizuri, (laughing) niliandikwa kwamba mimi ni senior village elder kwa hivyo mimi ninataka wazee wa vijiji watambulike.

Com. Swazuri: Vizuri sana

Suleiman Said: Kwa jina naitwa Suleiman Said Musanzu kutoka mwanzo ngo'mbe block ten na maswali yangu ni matatu. La kwanza, nataka kujua katika katiba hii mpya je imeangalia wale watu ambao wameishi shamba ambazo ni za Mazrui kwa muda mrefu sana na hawafikiri bali wao juja na ma-title deed na wale wakaanza kufukuzwa katika ardhi ile hilo katiba hii ifikirie.

La pili ni kwamba katika barabara zetu za mashambani ni mbovu sana mfano kama hizi za kwenda Bamba na nyingine je katika katiba hiyo wizara itafikira ama vipi?

La mwisho kabisa, ni kuhusu mambo ya Uislamu. Je katiba hii, imetilia mkazo miswada yetu ya Kiislamu kupokelewa kisawa sawa ama itabakia vile vile kuzibwazibwa bila mafanikio yeyote, na hali sisi nasi ni dini kama dini zingine za kikristo? Asanteni (clapping)

Com. Swazuri: Naona amekuwa commissioner sasa.

Interjection: Wamekuwa huko nyuma mpatie huyo mama.

Josephine Mrabu: Mimi ni Josephine Mrabu nina maswali kadhaa. La kwanza, ni kuhusu sisi wasichana ama wanawake. Jambo la kwanza, kuna hali ambayo hupata wanawake kama rape. Sasa ile serikali ama kule polisi ukiwa umerapiwa mpaka uambiwe uende pale na exhibit, ama umetoka kufanywa kile kitendo ndiyo uwende kule ndiyo watakubali. Na kuwa hali zingine you have been forced lakini ile hali pengine umejaribu yaani haikuwa vile kama alitarajia yule mtu awe sasa kwa sababu pia hakuna aliyekuona karibu utachukukuliwa wewe wamezingiria na hali kama ile haitachukuliwa umuhimu ilihali.

Pengine ingekuwa yaani yule mtu angewachwa wewe kama msichana angedhuruika ukapata madhara na siku hizi kuna mdudu ambao ni ukimwi. Na wanaume huchukua zile nguvu alizo nazo kwa sababu yeye ni dhaifu akikukaba yuwajua kabisa hata kama ana mdudu kama ni mimba atakupatia na sisi ni wanawake hatuna uwezo huo wa kuteta na wanaume. Kwa hivyo katiba itilie maanani ripoti yoyote itakayopelekwa kule iwe kuna shahidi hakuna shahidi itiliwe maanani na itiliwe mkazo yule mtu apewe haki yake.

Pili, kuna corruption na hii corruption iko kwenye uwanja wa magogo ijapo hivi hawako lakini mumesikia kuwa serikali za vijiji mimi kama kijana nasema hivi, natetea haki yangu. Sasa watakaosimamia misaada kwa sababu misaada watoto wengine hawajiwezi kuna family tu fahari ambayo haijiwezi. Sasa ile misaada ikiletwa wale amabo wanasimama hivi si ma-chief wale watakaokuja. Wakichukua ile misaada kwa hicho ki-group tayari wakakubaliana sisi tutachukua magunia kumi kumi wale wengine ni mkebe moja tena huo mkebe mwambiwa mlipe shilingi kumi kwa sababu ya kugharamikia transport. Kama ni msaada huwa ni msaada imetolewa na ule msaada nafikiri huwa wanampatia mtu asiyejiweza kwa hivyo huwezi kumwambia ati ashughulike na transport. Kama watoa msaada utoe msaada na ule msaada uhakikishwe umetolewa.

Mimi kama mwananchi mumeniambia nilipe shilingi kumi na shilingi kumi sina. Nafikiri nataka kuwe na ile haki naweza kumshitaki mtu kama huyo. Kwa hivyo ile msaada tiotolewa kwa kila mtu maanake pia hapat town hakutolewi misaada na mimi naweza kuwa naishi hapa town na nikawa ni masikini kwa hivyo ile misaada wale watakao simamia serikali za vijiji watambue wale masikini wa hapa kijiji wajue pia wale masikini nao ni wapewe sio mashamba peke yake na hapa sisi twafa na njaa.

Jambo lingine ni kuhusu interviews especially kama hawa mapolisi na majeshi huwa wanaweka qualifications ambazo wanajua watachukua watu wao. Sasa mtu kama mimi kama kijana nitapelekwa kule uwanjani kwa sababu nina ile hamu ya ile kazi na ninajua urefu ni nao pia kusoma nimesoma na mambo mengine kadhalika. Sasa pale mpaka tuondolewe mbio sijui tuende wapi mpaka wengine twaenda zirai kule halafu wanajua nikirudi pale tayari toka ufai wewe ni bibi, huyu yuaambiwa wewe toka sijui uko hivi toka ilihali wanajua wana watu wao ambao walikuwa watawachukua.

Kwa hivyo mimi ningeomba, kama wana hiyo hali hiyo wakifike pale uwanjani, uwanja umejaa wanambie tayari wale ambao wanaona hawafai wawambie tokeni, badala ya mtu umikimbize mbio azirahi aondoke na kuchoka akirudi kule hawezi kuenda kuuazi mandazi kwa sababu ni mgonjwa halafu mmechukuwa watu wenu (clapping). Sasa hiyo serikali ijue na wale watakao umia au watakaodhuhurika wao watapewa msaada maanake kuna gari za first aid lakini hazifanyi chochote, yuwachiwa mzazi anataka tena mtoto wangu atafuta kazi akifika kule analazwa mahututi yuharisha kule ward yuwabaki sasa ni mzazi angemtunza yule mtoto wake na ilihali mzazi hana chochote, kwa sababu alikuwa yuwataka hiyo mtoto apate kazi.

Pili, hawa ma-major ama hawa ambao wako kule wachukue watu kwa sababu ati wanawajua huyu ni mtoto wangu ama ana shemeji yake kwanza atachukuliwa. Mimi ambaye sina mtu nabaki hivyo hivyo kwa hivyo ile jamii yabaki kuwa maskini mpaka milele. Kwa hivyo hili nalo liliwe nini. Pia hizo interviews, kama kwafanyika interviews natunajua kuna watu wa electoral commission wanachukua watu pengine watasimamia vikura watawekwa Kilifi primary uwanjani nini, hao watu wana tabia ambayo mimi sipendi, maanake mimi tayari sina kazi hao watu wafanya kule maofisini. Sasa watachukuana wale ambao wajuana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu ule alifanya electoral commission iliyopita yuwachukuliwa hivyo hivyo yuwawekwa mimi pia ambaye ninafaa sionekani na nikienda naambiwa mambo yako yatachunguzwa waambiwa tu hufai hufai. Sifai kama sifai nieleze sababu ambayo yanifanya sifai kwa sababu pia mimi ni mwananchi nimejitokeza (clapping).

Interjection:(inaudible)....

Cllr. Chirenje: Kwa majina mimi ni councillor Chirenje kutoka Choni, elected. Mimi nilikuwa na maneno mawili, ijapo la tatu la nne limeshatajwa. La kwanza, ni kuweza kusambaza hali ya elimu. Tunakuta ya kwamba, waalimu haswa wa shule za misingi, upili na university na kuendelea wanalipwa. Lakini tunaye mtu mwingine ambaye ni maskini kabisa anashindwa hata kupata yale mahitaji yake ya kawaida, na watoto wake anashindwa hata kumpeleka hata hizi shule za msingi. Na kuna wengine kwa wakati huu ambao kwa jumla familia zao zimeshindwa kumpeleka mtoto wake au yule mwenyewekujisaidia ni kwenda katika hizi shule za watu wazima au shule za watu wa ngumbaro. Shida moja iliyoko ni kwamba, kwa wakati huu wameanza kufuta wale waalimu na wale walioko serikali inasema hamna pwsa ya kulipa adult education. ssa utakuta wale ambao hawakubahatika kwa sababu ni kutoka kwa jamii kwa hawa waalimu ningeseema ya kwamba kila mahali kwenye shule ya msingi kungekuwa na mwalimu wa shule ya ngumbaru ambaye atalipwa na serikali ili kuwezeshe familia ambazo hazikupta kusoma zisome. Hakuna huku kwetu hawapewi mishahara na ndiposa watu hawataki kwenda kusoma kwa sababu walimu

hakuna.

La pili, ambalo liko ni land tribunal board, hii wakati mwingine tunakuta kwamba hii land tribunal board wanachagua watu ambao hata pengine hawajui kabisa. Wachaguliwa kwa interest za mtu fulani especially the administrators ndiyo wanachagua hao land tribunal bodies ambazo hukalia haya makosi ambayo yako very sensitive kwa wananchi na kwa sababu yeye yuko na pendekezo au yuko na interests za watu fulani utakuta hata yule uamuzi si ule wa haki anafanya uamuzi wake kulingana na yale mapendekezo au kumpendekeza yule ambaye amechagua. Kwa hivyo, pendekezo langu ningesema ya kwamba wale ambao ni land tribunal board kuanzia tarafu hadi mikoa wawe ni watu ambao wanapendekezwa na wananchi wenyewe, si watu ambao wanachaguliwa tu na ofisi za utawala au ni watu fulani ambao wana-cover interests zao asante.

Samson Matano: Kwa majina naitwa Samson Matano mkaaji wa Kilifi mfanyaji biashara ndogo ndogo. Mimi nilikuwa nataka kupeana maoni kidogo au pendekezo kulingana na madada zetu kwanza, ambao wakati mwingi kwa siku moja au jingine mwanamume mmoja au mwingine lazima amelala na msichana mahali. Katika kulala kwake amepatisha msichana huyo alipompata mimba. Kuna ule wakati wa kwamba, either wakubaliane kwamba waowane au kuna wakati kwamba wamekaa pamoja kama 'come here we stay', kama wakati huu ambao kuna ukame wa pesa. Bwana hawezi kuoana anaka na msichana wake kwa miaka ya kuhesabu ameenda miaka kwamba akienda akizaa mtoto anaka bila kwamba hawa makao maalum. Mzazi wa bibi wamekatalia kwamba aolewe mtoto amekaa muda mrefu anaenda mpaka miaka kumi na nane hana makao pa kukaa. Sijui katika hii tume yenu mmefikiria aje katika hili jambo, because atakaa mtoto baada ya kwamba apate makao anataka kuowa anaambiwa hapa si kwenu, sijui jambo hili nyinyi mumefikiria namna gani katika hizi hali za hawa watoto ambao munasema kwamba tunataka tu kuwapatia haki zao. Mmewapata ahadi kwamba watagawanya hili mzigo ambayo bwana na bibi wamulee huyu mtoto au ni bibi peke yake au ni bwana peke yake? Hili naona kwamba hamkufafanua na nafikiri kwamba utatutulia hilo tatizo.

La pili ni kuhusu tenders katika upande wa biashara wafanyi kazi wa kupeana tenders. Utaona kwamba kuna wafanyi biashara tofauti hapa. Wakati tender zimefika wafanyikazi pengine mjengo wa shule utaona kwamba wengi tender zikishapelekwa mtu anataka ile kazi haionyeshi ile uwazi kwamba hii kazi imepatiwa nani ile njia ambayo amepitia mpaka apate ile kazi yule haionekani upatikana namna gani. Utaona tu kazi imepewa mtu fulani na ile njia ambaye imepitia hujui ni njia ya aina gani kama ni kufungua zile tenders. Haijulikani, ni kina nani wamekuwa pale hiyo si jambo ambalo lahusisha sana popote.

Jambo lingine pia ni kuhusu kuna jumba lilijengwa pale stage likaambiwa kwamba ni la wafanyi biashara. Atakaye ataandika application ikiwa mimi moja wao niliandika application tena mbili nika-apply hapo mahali kutumia jina tofauti langu la biashara na langu binafsi baadaye tuliambiwa mwaka jana kwamba ingefunguliwa mwaka jana mwezi wa nne hilo jango limeenda hivyo baadaye nilipoanza kuuliza naona watu wanaanza ku-occupy, haijulikani aliingia kwa njia gani. Ukiuliza unaambiwa kwamba nenda ukamuone councillor Chiunge upate block ingine basi sasa zimeenda mpaka ukienda hapo utaona kwamba zime-occupy nusu zingine zimebaki vile vile because inatakiwa umuone councillor mwenye haji mumuone councillor Chulumu sasa mulikuwa

mnajenga ya kazi gani lile dude pale. Kama halina kazi liondoeni mukaliweke pahali pengine au kama ni councillor Chirenge mpelekeni kule kwao likakae kule kwake (laughing and clapping).

Halafu kuna jambo lingine ambalo pia nilikuwa nataka kulizungumzia kuhusu watoto wanazaliwa wakiwa wana different religious. Pengine mumefanya penzi na msichana wakati ule sijajieleza za mimi matano ni nani, baadaye tukishazaa nakaa nikiambiwa nilete mzigo mimi nasema kwamba mim nimeokoka hilo jambo hilo nimetoka.

Mimi nilibadilisha dini tafadhali hayo yalikuwa na ya jana ni hivi sasa mimi nimeokoka siingilii dini yoyote lakini nazungumza tu yale ambayo hutendeka. Je wale nao mtachukulia jukumu gani? Asante ni hayo tu kidogo.

Com. Swazuri: Asante sana nitaanza kuyajibu halafu ndiyo tuchukue maswala mengine. Bwana Mzererah niliua habari ya pensions nafikiri hilo ni swala ambalo tumejadili. Nafikiri tutaliweka ndani hiyo ni kweli pensions za wazee, mshahara linatajikana iongezwe kulingana na miaka inavyoenda. Halafu maswala ya non governmental organisations kuna kipengele ambacho tunawahusisha hata katika ile Judicial Service Commission, watatu wao watatoka kwa NGO's. Kwa hivyo wao pia wana nafasi yao katika hii katiba.

Wildlife mzee ameuliza wale ambao wanaliwa wanauwawa na mamba na wanyama kifungo chake kiko section 239, kipo hapo ambacho kinasema ni lazima wananchi wapatiwe compensation ile undani details za kuhusu compensation ni ngapi ni kiwango gani sasa huyo inaenda kwa wildlife compensation Act. Na tumesema hakuna sheria ambayo itatengenezwa iwe kinyume cha katiba.

Maskini waangaliwe, nafikiri katiba yetu mmeangalia sana upande wa masikini upande haswa wa zile basic rights, tumesema ni jukumu la serikali sasa na serikali zote tumezitaja. Ni jukumu lao kuhakikisha kama mwananchi wa Kenya anaishi maisha ya kibinadamu. Maji ni lazima ni lazima wapatiwe si kwamba ni hiari, ni lazima serikali iliyoko ifanye mipango iwapatie sasa zile details zitakwenda kwenye Water Act, health namba hiyo hiyo education namna hiyo.

Swala la ma-squatter Bwana Hamisi nafikiri tumejaribu kulitatua kwa kusema kwamba ile mikataba ambavyo imefanya watu ma-squatter yote uchunguzwe tumeandika katika land section hapo ichunguzwe na wale ambao watapatikana kwamba ni wenyeji wapewe ardhi tumeandika wazi wazi hapa.

Wazee wa mtaa walipwe mishahara tulisikia hiii Kenya nzima. Lakini tumesema kwanza muelewe hii serikali ya kijiji tunayoitengeneza sio serikali ya wazee, ni serikali ya kijiji watu wataambiwa kuna nafasi kumi za kupiganiwa. Hapa sasa electoral commission imekuja wananchi chagueni wale watu kumi sasa wenyewe nitachagua sasa kama mtachagua wazee, hiyo ni shauri yenu mtachagua vijana hiyo ni shauri yenu mtachagua vijana hiyo ni shauri yenu mtachanganya nyama hiyo ni shauri yenu. Kwa hivyo hao mshahara wao automatically upo maana hao ni wabunge tayari wameshachaguliwa na location namna

hiyo, district, province namna hiyo mpaka wale wabunge wa kitaifa. Sasa basi ikiwa wale, ile serikali ya kijiji itachaguliwa halafu isiwe hapa kwetu ni lazima tuwe na wazee wa kijiji sasa hiyo ni by-law yao, sheria yao watatengeneza lakini sikiuke katiba ya Kenya.

Upande wa recruitment hili ni swala ambalo hata jana tulilisikia wakati wa uteuzi huwa kuna mapendeleo fulani either ya kikabila au ya kieneo au hata dada zangu huambiwa mpaka hata utongozwe ndiyo au hongo. Kuna vyyo vingine nasikia mpaka elfu kumi sijui elfu ishirini hata kama ume-qualify. Hayo ni maswala ambayo tumesema sasa yatakuwa maanake hayapo kwa sababu hongo nimeeleza pale mwanzo anayeota anayeomba, anayechukua, anayetumia, anaye-encourage hao wato wako hatani hao kwa hivyo huna haki wewe ya kutoa elfu kumi upigizwe mbi hapo kiwanjani halafu uende zako zile elfu kumi kwanza wampa nani? Receipt iko wapi? Wampa za nini na wewe una haki yako. Kama hau-qualify tumesema watu wa (C+) waje ukija na (D+) shauri yako tumesema tunataka watu wa (C+) kiwango tutakachoangalia ni (C+) na ndiyo tumesema hizo rights hizo zimetawanywa katika kitabu kizima. Hakuna kubaguwana kwa eneo, kwa nini kwa nini lakini la muhimu zaidi, tumesema serikali ya wilaya district council ndiyo ambayo itakuwa na uwezo wa recruitment. Sasa nyinyi wenyewe ndiyo mtaoneana nyinyi wenyewe lakini jukumu lile sasa limetoka kule limekuja kwa wilaya.

Refugees, sheria za refugees si zetu hapa ni za kimataifa umoja wa mataifa una sheria zake za wale wakimbizi wa kisiasa refugees kwa hivyo sisi tumechukua tu sehemu yake tukaweka hapa lakini ni utekelezaji na kwa sababu ya hongo lakini refugees wanatajikana wawe kando kabisa maanake maana ya refugee ni mtu anayeishi kwa sababu kule kwao kuna shida fulani. Kuna tamaa kwamba siku moja itatatuka halafu atarudi kule kwao kwa hivyo ukimweka hapa sawa sawa na sisi ni kwamba umemukubali kwamba huyu ni raia wa hapa hizo na sheria za kimataifa ni utekelezaji ndiyo hakuna.

Chuo upande wa pwani nafikiri tumepigania sana na tukausika kwenye sheria lakini hakuna chuo hiyo ni kweli. Bursaries huo ni utekelezaji bursaries ni za watu ambao hawajiwezi hiyo ndiyo maana ya bursary kwanza. Lakini kwa sababu ya utekelezaji ikabidi nyinyi wananchi ndiyo mtakuwa macho sasa.

Wazee wa vijiji nafikiri walipwe mishahara na uniform nimeshajibu hilo kwamba wale serikali ya kijiji itamua yenyewe. Mazrui land nimeshaeleza kwamba nitapitisha sheria katika miaka miwili kutakatua mambo haya yote barabara sasa ni kazi ya district hiyo si kazi ya kule tena kama serikali ina jukumu la kugawana usawa wa natural resources Kenya nzima tumeandika kwenye katiba lakini jukumu kubwa ni la district. Halafu misaada ya waislamu nafikiri hili ni swala ambalo limekuja kwa sababu ya September 11 yale mambo ya Osama Bin Laden kule ndiyo unaona kumetiliwa handa kidogo kwa upande wa misaada ya Waislamu lakini nafikiri ni neno la muda hili litatatulika sababu ulivyosema ni kweli waislamu hata wao wana haki ya kupata misaada.

Mambo ya rape victims hiyo tumeiweka lakini hatukuiweka directly tumesema lakini sio directly kwa hivyo tukiweka maanake tumesema kwamba hiyo kwanza msichana kunajisiwa kwanza ni kiukaji wa haki yake ya privacy. Tumeandika hapo sasa ni vile

tu hatujasema unajisi wa wasichana ni hivi lakini kuna sheria yake na ikiwa tunataka wananchi lazima tuitie hapa tukaiweka. Tatizo lilikuja kwamba kuna wasichana huenda kushitaki mtu na pengine kweli hakufanya hapo ndiyo tulikuwa na wasiwasi.

Halafu ule upande wa recruitment, tena ukaeleza interviews nafikiri tumetaja na wale electoral clerks sasa itakuwa si kazi yao ni kazi ya district. District ndiyo ambayo itaangalia kila kitu kama kimekuja electoral commissioner ataka kuandika watu sasa ni lazima serikali iliyoko pale ndiyo ambayo ina jukumu la kusema tutaandika kina nani.

Councillor Chirenje umeeleza habari ya adult education. nafikiri tutaliangalia swala hili sisi tulikuwa tunafikiria kwamba maanake si watu wengi walituambia, walilalamika nafikiria kwamba ni vile tunajua kwamba ni vile tunajua kila shule ya msingi pana darasa la gumbaro pale lakini kumbe ule tutaangalia.

Na land tribunal tumesema hizo zita-form-iwa na serikali ya pale chini kwa hivyo ni wananchi wenyewe wata form land tribunal si kwamba kutoka mtu mbali watu walisema kwamba kuwa surveyor anatoka mbali huko anakuja anakuwa ni mwenyekiti na matatizo ya hapo hayajui kwa hivyo hiyo haiwezekani. Wa tatu Samson Matano watoto ambao hawako kwenye ndoa. Hili tatizo tumeliweka kwenye upande wa children rights. Mtoto tumesema mtoto amezaliwa kwenye ndoa, wazazi wamewachana, hayuko kwenye ndoa yoyote haki yake ni lazima apate ataenda wapi kosa si lake ni wale wawili waliokutana wakamtoa yule mtoto duniani. Sasa hatuwezi kumuadhibu huyu kwa sababu ya ujenga au kukosana kwa watu wawili tulizingatia hilo sisi. Sasa kitoto cha miaka miwili kimeachwa barabarani hakijui kiende wapi mtu akasema wewe utakipiga bakora useme wewe nenda zako na wazazi wajua ni fulani na fulani lakini wamekataa kusikizana kwa hivyo tumeandika pale kifungu namba 37 mtoto yeyote ana haki zake. Sasa upande wa kugawanya kuangalia masilahi yake tumesoma kwamba mzazi, mke na mume waliotoza mtoto yule basi wataelewana kama wawe utatoa school fess mimi nitatoa uniform hayo ni maoni yao lakini haja yetu ni kwamba yule mtoto lazima yake iendele hata kama wale wawili wamekosana.

Upande kama wataridhi mtoto kama yule amekuja amezaliwa nje ya ndoa kama atakuja kuridhi au la swala hilo tumelihudhuria kwa mila na dini maanake hatuwezi kuweka statement moja ile kwa sababu dini nyingine zina mikakata yao ya kuridhi mila nyingine hilo ni neno swala ambalo litatambuliwa na wananchi wenyewe kulingana na sehemu zao wanazoishi. Wengine kulikuwa mikono mingine hapa. Moja mbili kila mtu ashike namba yake 1,2,3,4,5,6,7,8,9, 10, 11 kule mama haya kila mtu ashike namba yake. Number one.

Said Nathan: Mimi kwa majina naitwa Said Nathan kutoka Katahungu. Sina kazi, tunashukuru sana serikali mpaka sasa tumepata uhuru lakini huku pwani tukinyimwa hayo matunda ya uhuru. Sisi hatujayafurahi hayo ya uhuru sawa sawa na sababu yenyewe ni kuwa pwani pia watu wamesoma kisawa sawa kama kule sehemu za bara. Kwa hivyo ambavyo vilikuwa viko huku pwani vinatufaidi sisi wenyewe.hivi sasa tukiangalia viwanda vile vimevunjika kabisa. Kwa mfano nikitaja,ni kiwanda cha sukari. Tukiangalia mwaka jana kulikuwa na matatizo ya sukari. Sukari ilifika mpaka shilingi mia na ishirini kilo moja ambayo sisi wananchi wa chini tulishindwa kununua sukari ile. Je, leo ingekuwa serikali katika budget zake sisi tusingenunua sukari kwa bei

moja. Kwa hivyo kiwanda cha sukari kimeuliwa kabisa watu wakiangaliwa sukari ile ile matajiri wanatoa sukari kutoka nchi za nje kwa bei nafuu. Wakija huku wanatuuzia sukari kwa bei ya juu sana kwa hivyo tunaomba serikali katika mipango yake kwa budget iangalie mradi huo wa kwanza wa sukari.

Pili, tukiangalia viwanda vyetu ambavyo ndivyo vinatarisha Kenya huku pwana sisi hatufaidiki na maendeleo kama yale mfano tuko na port. Hapa port ile tukiangalia wafanyi kazi wengi walioandikwa na watu kutoka sehemu za bara, sisi huku chini tunakaa vijana wazee hatuna makazi kabisa. Kwa hivyo tunaomba serikali katika kupanga katiba ihakikishe kuwa port ile kila tane moja ambayo itakuwa inatoka hasi faida ile hata kama ni shilingo moja iwe itanufaisha watu wa huku pwani. Vile vile tukiangalia mahoteli ya wazungu yameenea kutoka Lamu mpaka South Coast tukiangalia wafanyi kazi wengi ni mtu kutoka bara kwa hivyo tunataka hata kama ni kila mzungu atakaye kanyaga hii ardhi ya Kenya iwe anachangiwa hata dola moja iwe pesa ile itanufaisha maendeleo kutoka huku sehemu za pwani. Kuongezea kuna zao letu ambalo tumelitegemea kuna kahawa, majani, chai na wizara ambazo zinasimamia bei hizi nje kabisa.

Tukiangalia huku kwetu pwani nazi ndicho kitu cha mazao lakini bei kabisa na korosho. Kwa hivyo, tunataka kuona mipagangilio katika katiba ikipangwa iwe zao hili la huku pwani litaangalia vizuri ni kwa sababu sisi hatuna kitu kingine cha kutegemea isipokuwa ni mnazi na korosho. Mnazi ule hakuna hata kitu kimoja ambacho ni hasara pale ndani tukiangalia kwanzia kuti mpaka mnazi wenyewe mwisho unaweza kutolewa hata kamani mbao kwa hivyo serikali ikipanga budget zake iwe kuna viwanda ambavyo mnazi ule utatunufaisha sisi hata kama ni tembo la mnazi. Wazee wanaeliminisha watoto tunalisha familia tukitegemea kwa hiyo mpaka sasa ikifika wakati wa kura unasikia tembo la mnazi limefunguliwa kura. Zikipita mnazi ule umefungiwa, tumedekezwa mimi sisi watu wa pwani.

Haya, tukiendelea tena ni kuhusu university, twajua kuna waislamu wengi sana pwani lakini utakuta wanasoma madrasa wakifika mwisho, utakuta hakuna university hata moja huwa inasaidia vijana wakiislamu kuendelea mbele. Utakuta wengine wanapelekwa Sudan, Morocco na Saudi Arabia kwenda kusomea, kwa hiyo katika budget za serikali tunaomba kuwe na university moja hapa pwani hata kama ni mbili sio vijana wale wakimaliza kusoma wanaendelea mbele.

Juma Kadosho: Asante sana mimi kwa majina naitwa Juma Kadosho youth leader wa KANU. Mimi nitaeleza kulingana na utaratibu vile ulivyo. Mimi niko kagaa, tuko kagaa wengi karibu maelfu ya watu. Leo hii, hatujijui kama tuko wapi kagaa ni barabara ya Ganze, Kakanjuni kule ambapo wenyewe wanaita farmers. Swali langu ni kwamba tunaomba serikali hii ambaye itapendekeza kulingana na katiba hii ijaribu kutia maanani sana kwa ma-squatter wale ambao wako kule wawe hawatasumbuliwa hata kidogo na mkizungumza hivyo nazungumza kwa sababu mimi ni mkaaji wa huko hata pia isitoshe pia mimi pia nami nina shamba hata ina minazi.

Kwa hivyo, nafikiri kuongeza hapo nikulilia sehemu nyingine ambayo vijana wetu ambao tunazaa. Tunaacha vijana wetu vizuri sana tunawaweka skuli vizuri sana lakini unakuta utasoma ikifikia wakati wa kwamba aende mbele havezi kuenda mbele kwa

sababu ya mzazi ameshindwa kwa utafutaji wa manufaa ya kumpeleka mbele yule mtoto. Atakomea pale pale mwishowe wake itakwenda mpaka aanze kuiba. Ushanielewa?

Tatu, nataka katiba hii mpya itilie maanani kampuni zote ambazo zilikuwa zimekufa papo awali zirudishwe zote tafadhali. Wananchi wale ambao ni wezi, wakome kuiba kwa sababu hawatakuweco kazini. Kwa hivyo nikisema hivyo nasema kwa sababu mimi nami ni mzazi. Asanteni sana sina zaidi.

Pastor Mangi: Mimi kwa majina ni mchungaji Joseph Mangi. Nilikuwa ninauliza kwamba katika hali ya katiba kuwe na kipengele ambacho kitahusiana na jamii bora kwamba iweze kuidhinisha katika katiba kwamba kuwe mtu analazimika kuoa mke mmoja na mume awe ni mmoja, kwa sababu kuleta jamii iliyo nzuri. Kwa sababu tukiangalia umasikini uliyoko, umeletwa na watu kuwa na wake watano, wanne na ikiwa kuna mtu na wake zaidi ya wanne aweze kushitakiwa ili abaki na mmoja na ili itulike maanani (clapping and laughing). Hiyo itatusaidia kuweza kupunguza hata maradhi ya ukimwi na mambo mengine na hali ya kiuchumi itaweza kunawiri, na itaweza na italeta pahali ambapo wazazi wataweza kutunza vyema jamii zao.

Jambo la pili ni kwamba hiyo katiba kuwe na kipengele ambacho rasilimali ya nchi itaweza kulindwa. Kusiweko na hali ile kwamba mtu anaweza kuweka hela nje, lakini hela yote iwe inakuwa hapa nchini ili kulinda rasilimali za Kenya (clapping).

Pastor Dickson Jembo: Mimi naitwa mchungaji Jembo ni msimamizi wa kanisa la Light of God Evangelism Kilifi au Kenya. Jambo la kwanza nilikuwa nataka nianze na kusema kwamba ninaunga mkono kwamba katiba au uchaguzi ujao ufanyike katika katiba mpya hii ambayo tunaitolea mapendekezo yetu ili iwezeshe kuleta mabadiliko yale ambayo tunayataka kama wananchi wa Kenya. Hata kama itatubidi tucheleweshe uchaguzi iwe hivyo sawa lakini uchaguzi ufanyike chini ya katiba tunayoitaka na ndiyo hii ambayo tunaijadili sasa (clapping).

Jambo la pili ambalo nataka niongee japo ni kuunga mkono mpendwa hapa ni lile la kuhusu mke mmoja, mume mmoja. Naunga mkono na ikiwa katika inaweza kuchukua nafasi hiyo itatusaidia ili kwamba nchi yetu ya Kenya ikaweze kuwa na jamii iliyo na heshima, uchumi mzuri, inayoweza kupeleka watoto wao shule kwa hivyo ninaunga mkono pendekezo la mpendwa (clapping). Ikiwa inawezekana katiba inakili hilo.

Jambo lingine la tatu, nilikuwa ninatoa wazo hili kwamba kulingana na hali ambayo nimeiona hata katika mkoa wetu wa pwani ninazungumzia juu ya elimu. Kuna tamaduni zingine au mila zingine ambazo zimewafanya watoto wao kutokwenda shule, wakiweza tu kushikilia habari ya mila yao au hata habari ya dini yao. Ningeomba katiba ile ambayo tunapeana mapendekezo sasa, kwamba itilie maanani kwamba kila mtoto akizaliwa ahakikishe anaenda shule hii ya msingi hata kama itagharimu kiasi gani. Lakini alazimishwe mtoto huyo aende shule ili kuondoa ujinga ambao unaendelea kutatiza watu walio katika nchi hii. Kwa hivyo ningeomba kwamba hata kama itikadi za kwao ni za mtu hapendi au zinamfunga, lakini elimu ikiwezekana iambiwe ni lazima. Na pia nikongeza kwamba kuweko na uwezekana kwamba elimu iwe inayoweza kufanya mtu asome ikiwa si ya bure

basi, ikiwezekana iwe katika hali nafuu ili watuwaweze kufaidika. Ni hayo tu nasema asanteni.

Johnie Kazungu: Mimi kwa jina naitwa John Kazungu ni mwenyekiti wa shule ya kutoka Maweni. Maoni yangu ni moja tu, ni kuhusu elimu hii ya msingi. Katika upande wa elimu ya msingi kuna pahali tunaanzia nursery, na nursery sijasikia ikitajwa. Nursery hii ina gharamia kubwa sasa na maanake walimu ni wazazi wanawalipa. Kwa hivyo kuna fees za juu sana. Wazazi wanalamika kulipa ndiyo mtoto aende nursery na watoto wengi wa wazazi masikini hawaendi shule na hapo ndiyo mwanzo. Kwa hivyo tungeomba walimu wa nursery waingizwe kwa wizara ya elimu kama wale wenzao wapate mshahara wa serikali ili wazazi waondolewe huu mzigo wa kulipa gharama za nursery. Watoto na nursery wachukulie sawasawa na wale wa primary wenzao hao ndiyo maombi yangu. Asanteni (clapping).

Peter V. Mweresa: Nashukuru kwa sababu ya katiba hii mumeleta hapa na jina langu naitwa Peter Mweresa na pia nashukuru kwa sababu ya hii katiba, ambayo mumeleta hapa kwa wakati wa sasa nikiwa na maoni ya kuwa kama itatumika kweli itakuwa ni mafaa kwa wakenya wote.

Jambo ambalo ningetamani kugusia ni kuhusu kuoa bibi wengi kulingana na vile watu wanavyotoa maoni. Hilo ni jambo ambalo ni upande wa kidini na mumezungumzia mkasema ni kwamba ni mtu ana uhuru kwa upande wa kidini. Sasa tuna mama wetu ambao walikuwa wameolewa tayari wawili watatu sasa jambo kama hilo je wale wangeliweza kuachwa kwa sababu mtu aoe mke mmoja? Sasa hayo ni mambo ya mwenyezi Mungu na tusiweze kuyaingilia sasa.

Halafu jambo lingine pia ni kuhusu miji yetu ya Kenya kuna town kama vile Nairobi, Kisumu, Eldoret. Miji kama ile ukisafiri unakuta kuna watoto kama chokora, halafu wale watoto ukienda ukishuka mjini kwa mfano jiji la Nairobi wanakutisha sana. Wanakushikia kinyesi wanakuambia angalia mzee toa kumi kama kama hautatoa then tunakupaka ama utoe shilingi mia moja sasa ikiwa serikali inaweza kutoa jukumu na ikasimamisha jeshi. Je watoto kama wale wanaweza kushinda serikali? Ikiwa kuna refugee wanaweza kuhifadhiliwa sehemu zao na hata watoto wengine wakajaliwa masilahi yao vipi kuhusu chokora pia watiliwe mkazo.

Japheth Choga: Asante sana mimi kwa majina Japheth Choga kutoka Lunga Lunga. Langu ni pendekezo kwa serikali za majimbo. Ningependelea katika serikali ya majimbo ile, ile council ya provincial kuwe na kipengele au tume yao zile 75% katika hasa kazi ya kuwa wenyeji hasa hiyo itiliwe mkazo sana 75% wawe ni wenyeji wa pale. Qualifications zifanywe lakini ile 75% iwe ndiyo lengo.

Halafu pili ni katika pesa mapato hapa sisi twategemea sana utalii. Lakini sasa utalii huu inaonekana kuwa hasa haifanyi kazi kwa sababu imekuwa watalii wanakuja kwetu pwani ama kuangalia wanyama kule porini lakini mtalii yule yule pesa zinalipwa huko ng'ambo na sisi hapa tunatarajia tupate hizo pesa ambazo zitatusaidia sisi. Kwa hivyo kuwe katika ile tourism board kuwe na hakikisho kwamba mtalii aje hapa na malipo alipe hapa hapa ili ile pesa iwe ina-circulate hapa ikatusaidia sisi. Kwa hivyo si

mtali anakuwa huko ng'ambo anaambiwa oh inclusive anambiwa anakuja Serena hotel kila kitu analipa huko ng'ambo sisi twasaidia nini hapa. Kwa hivyo maneno yote ya-fanyiwa hapa hapa ni wanyama ni mambo ya tourism kwa mahotelini walipe hapa ile pesa twaitaka sisi. Asanteni.

Albert J. Ruwa: Kwa majina ni Albert Ruwa kutoka kwa roga roga ni katibu wa Kenya Herbalist and traditional dancers. Natumaini tulikuja tukapendekeza hapa kwamba katiba hii mpya itambue uchawi. Sijui maanake nimechelewa, katika kupitia pitai sijui kama pengine kulitajwa lakini ikiwa haikutajwa wala kutiliwa maanani. Lengo ni kwamba, watu wanaosomesha watoto wao wengine kuenda mpaka university huwa wanawapoteza wasomi wale sababu ya uchawi, leo hii katiba yetu haijatumbua kuwa mchani ni nani.

Tuna chama hiki chetu, kilikuwa kikisaidia sana mambo mengine ambayo inawezesha kuwatambua wachawai. Lakini sasa serikali hiyo ama katiba hiyo ina kitengeli ambacho kwamba judge yule ambaye pengine hata mimi amenitunia bibi yake, ama mtoto wake nimuage hawezi kumhukumu mtu yule kwamba yeye mchawi maanake haikuandikwa humo hivyo basi umuhimu twataka utiliwe katika katiba hiyo mpya mambo haya tuepukane nayo. Asante.

Daniel Mwandongahayo: Mimi kwa jina naitwa David Mwandongahayo. Mimi ni mkaaji wa hapa Kilifi tu 'site.' Mimi swali langu nauliza kwamba ukinunua kwa mwenye shamba ambaye mtu ana shamba yake na amenunua mahali kama ploti mahali pa kujenga. Lakini mimi nimenunua tena kama laki moja ama nusu lake na tumesikizana nikanunua na kila mwisho wa mwezi yeye anataka nimpatie mia mbili, mia tatu.

Sijui kama mmechunguza jambo hilo katika mfumo wa sasa ambao tuko nao msururu wa katiba mpya. Nataka watu kama hao serikali iwachunguze. Sina mengi ni hayo machache tu. Asanteni.

Anthony Tangai: Kwa jina naitwa Anthony Tangai, mkaaji wa Marani. Nataka kuuliza kuhusu hali ya tatizo la kazi kidogo. Kufikia wakati huu nafikiri Kenya kuna matatizo mengi kuhusu hali ya kazi. Na mara nyingi utakuwa kuna watoto wetu ambao amesomea kazi fulani na amehitimu, na kuna mwingine ambaye amesomea tayari ameifanya na mtu yule mwingine ambaye amesomea tayari ameifanya na mtu yule mwingine anapokea mshahara kama elfu thelathini wa mtoto wangu mimi amesomea kazi ile ile lakini hana kazi. Je, katika katiba mpya umechukua hatua gani ikiwa yule anapokea elfu thelathini na mtoto wangu naye ana ujuzi wa kazi ile ile, lakini anatamani hata angalau awe na elfu tano peka katika katiba mpya mmechukua hatua gani?

Interjection: ...(inaudible)... Mbona nyinyi hamukuenda huko?

Cllr. Amina Kisasa: Mimi katika hiyo katiba numeenda through. Majina yangu ni Councillor Amina Kisasa wa Njunjo location. Katika yale mapendekezo ambayo tulitoa mwanzo kuna hilo Kadhi's Court nafikiri mimi mwenyewe binafsi nilikuwa nimeongea kuhusu kina mama ambao huwa wanakaa eda ikikiwa ni wafanyaji kazi. Nikawa nimesema kina mama wakiwa eda

wale watapewa ruhusa ya kukaa eda mpaka kumaliza eda ndiyo wawe watarudi makazini. Nilivyoenda through nikaona kile kipengele kimeachwa sasa sijui kama mtakitilia mkazo kivi lakini ikiwa kitaingia kiwe kitasaidia kina mama. Ni kitu ambacho tulikuwa tumezungumzia na tumekizungumzia na akina mama ambao ni Waislamu ningomba kipengele hicho tafadhali pia kitaonenekana mahali ikiwa kitawezekana ama sijui vile mumeandika ndiyo ameshapita ndiyo hiyo katiba haitarekebishwa ama ni vipi kwa vile tulikuwa hapa tangu mwanzo. Sasa kipengele kama hicho nimeenda through hapo ndani kiko upande gani nimeenda hicho cha eda hakikutajwa. Inavyomtaka lakini kwenye kazi kweli wewe utajengwa vile unavyotaka na kulingana na kuandikwa. Ana-practise dini yake.

Com. Swazuri: ...(inaudible)....

Cllr. Kisasa: Basi mngeliandika ndiyo mngekuwa mmeridhisha mimi na yule mwingine aliye chini (laughing). Mngeandika vile mngekuwa mmerudisha. Halafu nikaa katika hizo rape cases tulikuwa tumesizitiza yule ambaye asikize mambo ya rape asiwe polisi mwanaume peke yake. polisi mwanamke ambaye atamzungumzisha yule mama kwa sababu mara nyingine unaenda kukuta mwanaume ambapo mwanamke anashindwa kujieleza zile details za ile case yake, tungeomba polisi mwanamke ndiyo awe atashughulika na zile rape cases za akina mama.

Halafu wazee wa mtaa, katika maelezo yetu siku zile tulikuwa tumetajia ama kweli wamesema inaweza kuwa vijana, watu gani lakini iwe nusu na baba na nusu kina mama ili kusaidia wale wamama pia huwa hawana freedom of speech wakiwa ni akina baba peke yao. Halafu kulingana na serikali za mitaa, kuna cess collection. Labda utapata mwananchi sana huwa anaumia zile sheria huwa zimeshawekwa aina mara ingine wanakuja wanalaumika madiwani lakini wamesha semekana pengine kama ni serekali mama anayeuzua samaki anakatiwa pesa ngapi, lakini mara ingine itakuta mama yule anauza samaki si sawa na yule wa samaki kwenye fridge wengi. Mama labda ana samaki wake kumi tu lakini ni yeye aliye kodi sawa na yule mtu ambaye ana samaki wengi. Labda katika hiyo sales selection ije iangaliwe mare nyingine yule mwananchi amefanya biashara ndogo kabisa awe atalipa kiwango.

Okay ...(inaudible)... halafu elimu labda ya ngumbaru imezungumwa lakini mkazo kule tunapata elimu ya gumbaru kina mama hawaendi hata waalimu wakiwako kwa vile huwa wanachanganywa kina mama na akina baba na ni watu wazima. Wamama mara nyingine tulichunguziwa badala ya kuwa baba aende kule akisoma anza kufanya mambo ya kutongoza kule kweli magumbaro iwe kando kina mama na baba iwe ni kando kando (laughing). Nafikiri yangu ya kuongezea ilikuwa ni hayo asante.

Samuel K Charo: Nimeshukuru sana kwa furusa hii ambayo Bwana mwenyekiti amenipa. Jina langu naitwa Samuel Charo mimi ni mkaaji wa Ganze. Kwanza kuna hii sehemu ya ubaguaji wa wanawake ningetaka katika hii katiba mpya kuwekwe kipengele ambacho kitawalinda ana kitawazuia wakina mama kuvaa zile nguo za nusu uchi kwa sababu mare nyingi ndizo zinachangia kubakwa (clapping).

Kuna sehemu moja hii katika sheria ya kwamba mwizi wa mabavu anaweza kuhukumiwa kifungo cha kunyongwa ilihali mtu ambaye ameua anaweza kufungwa tu miaka miwili, mitatu na atolewe na bond hii kitu imenitatiza kwa muda mrefu sana. Hapo katiba hii ikaweza kuangalia, kwa sababu mtu ambaye ameua ni tofauti sana na yule mtu ambaye adhulumu mtu ama ameiba kwa mabavu nafikiri kuna tofauti ya mtu ameuwa pale na mtu amefanya kuiba tu kwa mabavu na yule mtu akaachwa salama tu pale.

Halafu kuna hii sehemu ya village level nataka kuwekwe qualifications angalau yule mzee wa kijiji atakayechanguliwa awe anaweza kuandika na kusoma. Hii sehemu ya wachawi tafadhali mtanisameheni nataka kuongea kidogo. Kuna hawa wachawi lakini kuna wachawi wale wa kuroga na kuna wale wachawi ambao ni waganga. Sasa kuna yule mchawi mwenye kuroga watu na kuwaua. Saa zingine inaonekana kwamba ni kuchukua sheria mkononi kuchoma mchawi ama kukatakata mchawi kwa mapanga. Nataka katiba hii iangalie vizuri mchawi yule atalindwa vipi na katiba hii asiweze kudhuru maisha ya watu wengi na yeye aendelee kuishi. Halafu kuna sehemu nyingine ya wale wanaokaa sehemu za hardship zones tuseme Goshi, Ndigiria huko mbali Jila wakaaji wengi wa huko wanahamia sehemu za Kilifi. Kwa sababu hakuna security. Katika katiba hii nataka kuchungia kidogo kwamba ikaweze kuatambua vizuri watu wale kwa sababu ya ukosefu wa usalama na ningetaka kusema hivi ya kwamba, kama serekali itakubali kuwapa kama hawataweza ku-deploy watu wa kualinda huko wapewe silaha za kualinda wenyewe. Kwa sababu huwa maisha yao yako katika hatari. Ningesema hivi ni kwamba, sehemu za bara kule kuna wakaaji wengi wamepewa silaha na wanajilinda na utakuta silaha hizo pengine wanakosa kuzitumia hata ingawaje waki-raid mifugo ya wenyewe na hali kadhalika. Lakini wananchi coast vile nimewaona ni watu ambao wako very humble na wanajali masilahi ya watu wakipewa hizi silaha kijilinda sehemu hizo si rahisi kuzitumia kuua watu wengine na kadhalika. Kuna sehemu hii ya mwisho nilikuwa nataka kuiguisia, hii sector ya elimu. Kuna hawa walimu ambao wanalipwa hardship allowances. Pole ninagusia hii sehemu kwa sababu kuna walimu wengine wanakaaa town kama hapa Kilifi lakini anafundisha shule ya mbali sana na apengine katika ile shule ambaye anafundisha hawezi kulala huko lazima alale town na akienda kule kila siku na mwalimu huyu hakuna hardship allowance. Pamoja na mwalimu yule ambaye anakaa pale pale akienda masaa manne ya kutembea ama ku-ride na baiskeli nataka hapo tume hii ikaweze kuangalia katika sector ya elimu.

Kuna ule muda wa kuondolewa, ama kuhamishwa mwaalimu anatakikana ahamishwe mahali fulani. Nasema kuhusu waalimu baada ya miaka mitano mwaalimu ahamishwe apelekwe shule ingine. Utakuta hawa ambao wanapelekwa shule za ndani ndani ama zile sehemu ngumu kukaa kule miaka mitano ni vigumu sana kutoka kule baada ya miaka kumi na tano atakuwa amepunguza nguvu za uzazi jambo la kwanza atakuwa amekuwa mgonjwa mumelea hasa kiakili, viungo atakuwa ni mgonjwa kabisa. Kwa hivyo, nataka katiba hii ikaangalie masilahi ya mwalimu kama kutakuwa na muda mrefu wa kumueka mwalimu sehemu zile na awe ana-ride kila siku tafadhali muda ule uweze kupunguzwa sana. Ikiwezekana muda mmoja hi hayo machache. (clapping)

Com Swazuri: Naona sasa twaanaza kusikiza vituko sasa. Kwamba wale walimu wanaofundisha zile sehemu kama halafu huwa hawana nguvu za uzazi sijaisikia hiyo naisikia leo. Haya viwanda vya pwani vimekufa kulingana na katiba hii itabidi vifufuliwe na

serekali ya jimbo, wilaya sasa ndiyo majukumu yao kwa hivyo ikipitishwa katiba hii kama mtambo wa sukari haujaanza sasa si problem ya kule juu tena, katika kazi ambazo tumewapa serikali hizi, hiyo ni sehemu yao kabisa. Habari ya kutafuta research ya mnazi mpaka uwe mnazi uwe na authority yake ni kazi ya jimbo la pwani lenyewe na korosho. Sasa hiyo ni kazi yetu sasa ule uwezo mlikuwa mnautafuta sasa ndiyo huo maanake kwa katiba ya sasa huwezi kuunda coconut development authority. Wewe mwenyewe utauliza imetoka wapi bunge haijapitisha lakini kulingana na hii check tuliyopewa blanket cheque hii sasa ni ya wale wenyewe wa pwani wakae waseme sisi tunaangalia mambo ya korosho itakuwa namna hii si hatia kuanzisha viwanda katika kazi ambayo tumewapatia wenyewe majimbo na wilaya.

Na kweli tunakubali ni lazima wafanyikazi wawe sehemu ile wenyewe ndiyo watatia mkazo. Revenue collected iwe inabaki pale, tumetoa percentage zake wenyewe ndiyo watoe mkazo. Chuo kikuu tunataka cha waisilamu. Hapa pwani tunapigania vyuo karibu vitatu sasa kimoja ni cha waisilamu, vile vingine ni vya watu wote tunapigania lakini mpaka sasa bado natujafanikiwa. Mimi mwenyewe niko katika kamati ya hivyo vyuo vyote vitabu niko lakini mambo bado ni magumu sasa naona yatarahihishwa na hii uwezo ambao watu wamepewa. Sasa halafu squatter problem kagaa kote tumesema kwamba hiyo tumeshaandika mambo ya masquatter hapa.

Halafu, tukaenda upande wa jamii bora mke mmoja mume mmoja hiyo wazee wengi nimesikia kunung'unika ingawaje kuna mama moja alikuwa anajaribu kusema pale sijui nani, nafikiri hilo ni kama kijana wetu amejaribu vizuri itategemea dini na desturi. Kwa sababu kama dini ya islamu imesema kwamba waanaweza ikiwa watatimiza ile masharti wanaweza kuoia mpaka wanne. Wengi huwa hawatimizi yale masharti wanachukua ile namba tu kwamba ni wanne basi wanachukua wanachukua waqnasema basi mwisilamu mimi nimeruhusiwa kuoia wanne. Lakini wale wanawake wanne kweli wana shida maanake huwezi kutekeleza hata moja. Hata dini yenyewe ya kiisilamu imekataa lakini hasa atasema mimi ni mwisilamu bwana nimeruhusiwa wanne huwezi kunifanya lolote. Kwa hivyo hiyo haukufuata dini ya kiisilamu kuoia mwanamke mmoja mpaka ukanitekelezea kwanza ni ngumu sana. Halafu tena ugawanye useme wote wawili uatekelezee haiwezekani lakini sasa wewe umewarundika wengine hufanya hata sita. Pia sasa hiyo inategemea yule mtu anafuata dini na madala hatuwezi kuweka sheria ya kusema kwamba Kenya hii mke ni mmoja mume ni mmoja itakuwa dini ingine imekiuka.

Halafu sasa kuna nyinyi wenyewe mfanyiane ile kama vile pastor mlivyosema, kunatakikana civic education, kubwa sana hatamu za kuoia bibi wengi na kuzaa watoto ambao bibi wengi na kuzaa watoto ambao hauwezi kuwalea ni ipi na faida.

Kipengele lakiini kuna sehemu ambayo inasema uongozi kwanzia permanent secretary mpaka juu hawaruhusiwi kuwa na account nje nilikuwa nasitafute lakini sijakiona tumesema hivyo kwanzia permanent secretary mpaka juu president, sasa watakuwa hairuhusiwi uweke account yako nje pesa zako ni lazima zitakuwa hapa.

Nursery fees, ziko juu tumesema elimu ni ya bure ya watoto kwa hivyo tukisema elimu ni bure ya watoto tunajua elimu inanzia wapi. Nursery mpaka huku juu ni bure mpaka primary school standard eight yote ni bure. Mambo ya swala ya watoto street

children nafikiri nimetaja pale kwamba watoto hawa wote sisi itabidi ni jukumu letu la kualea.

Uandikishaji wa kazi, toursim board lazima tu-apply wananchi wote wawe wako hapa 75% hiyo ni sawa ni jambo lenyewe litaamua na ile habari ya kwamba wanalipa huko ng'ambo hii ni mipango tu ya kulipa lakini kwa kweli wanatumia hapa kwa sababu wakilipa shilingi elfu kumi anakuja Kenya ili hoteli lazima itanunua chakula zile pesa zitafika mwisho lakini watatumia ile hotel. Sasa ile hoteli lazima itachukua ile pesa tasilimu ikanunue nyama pale sokoni. Kwa hivyo hiyo ni mbinu tu ya kuarahishishwa wasiwe wanachukua pesa mkononi kwa sababu ya wizi lakini pesa huwa zinatumiwa hapa hapa.

Halafu wachawi, kwa kweli hatukutaja neno lolote hapa kuhusu uchawi directly. Lakini tumesema kwamba sera zozote ambazo zinadhuru wananchi hazitakikani. Sasa sera hizo moja wapo ni uchawi, ikiwa nimedhirika mimi halafu unifanye ramuli zangu nijue kwamba mchawi ni wewe imeingia kwenye katiba hiyo. Na mchawi anaadhibiwa kutokana na witchcraft act. Kuna sheria ya Kenya chapter 11 inaitwa witchcraft act ya uchawi tu. Hapo imeeleza mchawi ni nani anayefanya vitendo kuhusiana na uchawi ni nani ataadhibiwa namna gani sasa nafikiri ile kwamba sheria zinaonekana hazina nguvu ndiyo wakiona huyo ni mchawi wanamkatakata mapanga wenyewe.

Pia wale wanaotoza kodi ya mashamba hayo ni maelewano. Hili ni neno ambalo bara haliko hii ni maelewano ya sisi wenyewe watu wa pwani tuna historia yetu kule ambayo tulikuwa nayo maanake sisi tunaamini kwamba ardhi ni ya mungu. Wananchi wanatumia ardhi kwa niaba ya mungu kwa hivyo mtu hana haki ya kusema hii ardhi ni yake. sasa ile imani ile ndiyo nasema kwamba mtu akija akisema bwana nataka mahali nilimee unasema okaya huna lakini usipande mnazi maanake huyo ni permanent usipende niende. Akija mtu anataka kujenga unamwambia sikuuzii maanake mimi siuuzi ardhi ni ya mungu lakini jenga kila mwezi nipatie shilingi mia mbili. Hiyo ni arrangement yetu kwa sababu ya ile social cultural history yetu lakini kule kwa wenzetu hakuna hilo neno. Kwa hivyo ni sisi sasa tumepewa uhuru kuamua. Utauza, utakodesha, utatoza vipi sasa uamuzi ni wa wananchi wenyewe.

Mishahara, mzee amesema watoto moja anapata elfu thelathini mwingine elfu kumi na tano sasa tumesema tumeunda salaries board. Hii ni ku-harmonise kuhakikisha kwamba mishahara ya wananchi wote wafanyikazi wote inawekwa vizuri kabisa. Na mama councillor Amina, nafikiri umekuja kuechlewa bahati mbaya lakini maswala karibu yote uliuliza, tulikuwa tumeshayapata. Upande wa eda kama nilivyokuambia atukuiandika hiyo eda hapa maanake tukisema hivyo hivyo tutaandika mambo mengi katiba yetu itakuwa ni kubwa sana. Lakini tumesema uhuru na kufanya mambo ya kidini ni lazima yazingatiwe na hakuna mtu ataajibiwa kwa sababu amefuata sheria yake ya dini.

Rape cases tulikuwa tumeshazijibu hapa. Na Josephine ameuliza hiyo mambo ya collection ya sales tulikuwa tumeshataja hapa labda swala ambalo umeuliza ni kwamba wale wanafunzi wa gumbaro waume na wanawake wasomeshe mbali mbali ingawaje huwe tunafikiria hatari labda ingekuwa kwa wale watoto lakini hawa ni watu na akili zao. Anyway, tutaliangalia swala hilo.

Kuna swala la wakina mama hawa wavae nguo vizuri. Bwana Samuel Charo ameeleza tulitaka kuliingiza hili lakini sasa likawa na ushindani mkali kwa hivyo ni swala ambalo tumeliweka pending kuhusu mavazi ya akina mama. Ni kweli tumekubali sote kwamba kuna mavazi mengine ya akina mama ambayo yana wame-encourage wale ambao wana akili za kufanya maneno maovu. Hilo ni swala la kwamba ni tubishane tena hilo linaeleweka kwa sababu kama msichana amevaa matiti yake wazi au kijitaru hii yote inaonekana au mabaya yote yanaonekana ingawaje ana uhuru wa kufanya anayotaka lakini uhuru huu unamudhuru mwingine hiyo tumekulaliana sasa tufanye nini hapo ndiyo baada tunajadiliana.

Village leaders, lazima wawe qualified ni kweli hatukuandika hapa qualifications zao na tutaandika. Na halafu akatilia sana muhimu swala la walimu ambao wamekuwa hardships areas na pale aliposema kwamba nguvu zao zinapungua. Nafikiri teachers act education act iko na teachers service commission wanajua vile hizi system zao wanafanya hatuwezi kuandika kwenye katiba hapa kwamba waalimu wawe-transferred baada ya kila miaka miwili tuseme kwamba sheria zote za Kenya ziambatane na katiba na kama katiba imesema mtu asidhurike sasa ni wazi wale wafuate sheria hiyo kwamba mwalimu katika hardship area ata-serve miaka miwili au mwaka moja halafu mwingine anakuja kuchukua.

Haya nafikiri nitachukua maswala ya mwisho sasa round ya maswala matano tu ya mwisho tufunge maanake naona watu wengin wanaandika ondoka haya namba 1,2,3,4,5,

Interjection: Naona mzee hata watoto wadogo wachague kwanza maana pia wako na maswala sema moja na pia watoto wana maswala wanataka kukuliza bwana.

Com. Swazuri: Kuna vijana hapa ambao sikuwachagua hapa. usitumie lugha hiyo, bwana ukasema ni wazee hiyo ni mzee ngoja huyo ni mzee.

Interjection: Haya basi wapatie nafasi hao, ...(inaudible)... abaki na wasiwasi.

Felix Makasi: Asante sana mimi kwa jina naitwa Felix Makasi ni mkaazi wa hapa. Mimi katiba hii tuliyonayo sasa hivi unazungumzia kuhusiana na elimu ya bure kuanzia shule za mwezi hadi pengine shule ya msingi. Wasiwasi wangu ambao kwa sasa nikasema ninaomba ufafanuzi, japo wengine wanafahamu tayari jinsi elimu hii ya bure ilivyopangiliwa. Wasiwasi wangu ni kwamba, kwa sasa hivi shule haziko katika viwango sawa. Shule nyingine ziko katika hali ya shida, madarasa mpaka sasa hazijatosheka nayo nyingine ziko katika viwango vizuri. Shule zingine kwa sasa hivi zina vifaa mpaka zimefika viwango vya kuwa na maktaba. Shule nyingine hilo ni jambao ambalo ni la kuota halijafikiriwa kabisa kwa hali ya maktaba. Sijui mpangilio uliyoko mpaka hali hii itakavyokuwa iwe sambamba kwa shule zote bila kuwe na manung'uniko pale wala pale. Pengine nigpeata ufafanuzi kutoka kwako jinsi swala hili la elimu ya bure lilivyopangilia na serikali yetu. Asante.

Com. Swazuri: ...(inaudible)...

Johana C. Kusa: Kwa jina mimi naitwa Johana Chibungu Kusa. Langu ni moja tu vyuo vya uma viregeshwe kila town. Tena wanfanyaji kazi walipwe mishahara yao vizuri ili waweze kulinda vile vyuo vizuri. Asanteni.

Abdul Ali: Mimi naitwa Abdul Ali. Swali langu ni moja tu. Nimependelea orodha ya katiba ilivyopangwa lakini jambo moja ni kwamba, hata katiba ile ambayo tulikuwa nayo ile ya kikoloni ilikuwako na watu wanaivunja. Je hii itakuwa na uzito gani? Mtu akifanya makosa na kuivunja katiba, hilo tu.

Ali Tajiri: Mimi naitwa Ali Tajiri Mwakangaja. Nauliza kuhusu kitabu, kama nitaondoka kama sikupata kitabu nitaendelea namna gani kusubiri.

George Arunda: Mimi naitwa George Arunda, afisa wa usalama hapa Kilifi. Hasa mimi maoni yangu natoa hivi. Nasema hapa nimekaa kwa muda mfupi, lakini naona hapa huu ugonjwa unaitwa ukimwi uko mwingi sana, na wale watoto wamefiwa unakuta wengine ni werevu sana. Sasa mimi nilikuwa natoa maoni hivi, tuseme mtoto mwerevu kama hawezi kupata karo na anaweza kufanya mzuri nilikuwa naonelea apewe elimu ya bure kuanzia shule msingi hata wakifika secondary watu wa nini. Serikali iangalie vile inaweza kusaidia. Kwa nini unakuta mwingine ni mwerevu mama na baba, wamekufa hakuna mtu wa kunisaidia hasa utakuta nyumae ndiyo atakuwa kijana mkora hiyo ndiyo maoni ya kwanza.

Halafu, ya pili nilikuwa naonelea hii maneno ya mashamba hii, wakianza kutengeneza wagawe kwa usawa. Kwa kuwa unakuta mahali pengine kama tuseme tunaweza kuongea tu story ya bara unakuta watu wanatoka family moja mwingine ako na acre tano mwingine acre moja kama wanagawa sample wagawe kwa usawa hata kama hata mtu akishashikilia hiyo yake unaangalia ni acre ngapi inagwa hiyo hiyo kama ni mbili ni mbili. Asanteni.

Elias Kiti: Kwa majina ni Elias Kiti. Mimi ni mkaaji wa hapa Kilifi. Nitaongea juu ya magereza ya Kenya. Unakuta magereza ya Kenya unakuta yale magereza iko yale amaho si sawa kabisa. Maana vile mambo tunajua ni kwamba gereza ni mahali ambapo mtu anaenda kurekebishwa tabia, wala si mahali pa mtu kwenda kuadhibiwa. Maanake mtu anaweza kuwa hapa huku nje ni mbaya lakini akiingia kwa gereza akitoka kule yule mtu unamuona anakuwa mtu mzuri kabisa.

Kwa hivyo kusema hivyo ni kwamba gereza sio mahali pa mtu kuadhibiwa bali ni mahali ambapo mtu anaenda kurekebisha tabia ili akitoka kule awe anaweza kuishi maisha ya raia vizuri. Sasa unakuta kama ni mfungwa amepolekwa kule, mfungwa hata ukimwanguka ni kama mtu ambaye hana haki, yale mavazi yake yenyewe ni machafu, amevaa unamkuta hata ile uniform yenyewe imerarukaruka kabisa imekatika mpaka imeingia kwa miguu huku anatembea uchi kabisa na yeye ni mfungwa. Kwa hivyo, mimi ningependelea yale magereza yarekebishwe ili kusitokee mambo mabaya.

Amos W. Noah Malaba: Mimi kwa jina naitwa mzee Amos Wamukoya Noah Malala kutoka Kakamega district nimeishi hapa Kilifi miaka kumi na tano na sio Mgiriama, sio Mijikenda lakini nashukuru ni m-coast. Na vile nitasema nakwambia ile kitu

ambayo ni kweli. Hapa bwana, tunataka hawa wenye katiba watupangie kitu cha maana kwa sababu jambo la kwanza siku ya kuchagua hawa wabunge watu kwanza tuangalie ana ukimwi ama apimwe kwanza (clapping and laughing). Kwa sababu na maana ni kwamba unachagua mbunge kumbe yuko na Aids anaenda kulala hospitali ten years baada ya five years analala tu hospitali. Councillor vile vile sasa tunataka mutusaidie kwa roho safi. Asanteni sana. (clapping)

Interjection: Hapo ametoboa hapo ni sawa kabisa lalamika.

Nyale Kiti: Mimi kwa jina naitwa Nyale Kiti. Nilikuwa nataka tu kuzungumza mamba kidogo. Kwanza nitaanza na juu najua kwamba katiba mpya ambayo ishaatungwa ishagusia sana uhuru wa raia lakini kuna shida moja ambayo huwa inatokea hata baada ya katiba kama hizi kupitishwa inakuwa ni vigumu sana askari kutambua kuwa raia wana haki zao. Kwa mfano, utapata kwamba sheria inasema kwamba kuna uhuru wa mtu kutembea, kujieleza au kuji-express au pengine hata mtu amefanya makosa lakini wakati askari anakushika, hana haki yakuwa anapiga lakini unaona kwamba askari anapiga na hata mahakama au korti haijamua kwamba nina hatia sasa inakuwa ni shida raia kutekeleza kitu kama hiyo kwa hivyo nafikiri katiba hii mpya ingesisitiza juu ya swala hilo.

Kitu kingine muhimu ambayo nilikuwa nataka kuzungumza ni kuhusu health au afya ya raia. Utapata kwamba sasa hivi kuna magonjwa kama vile ukimwi na ugonjwa mwingine ambayo hayana tiba lakini imekuwa ni vigumu sana mbinu nyingi ambazo serekali inatumia kukomesha au kujaribu kufukuza magonjwa kama hii inakuwa ni vigumu kwa mfano unapata kwamba mbinu nyingine zinatumika lakini unaona kama makahaba, malaya hawatiliwi maanani na ni watu ambao bado wanaendeleza ku-spread hiyo disease ni vigumu sasa tunadai ya kwamba eti ukivuta sigara inadhiuru afya yako mpaka tumeandikiwa lakini we are allowed to smoke halafu government inashindwa kutekeleza kututibu an malaya anarushiwa kama vile msusi mkavu they are there na government inajua kwamba hawa watu wana-spread the disease halafu then tunakuja tunasema we are fighting the disease we are lying ni kama ambao hatukuelimika. Kwa hivyo nafikiri inakuwa vigumu serekali ichunguze na watu kama hao wakomeshwe.

Kitu cha mwisho kuhusu katiba ambayo tunaitunga unaona kwamba ile katiba ya nyuma haikutekeleza kwa sababu maasi ambayo yamefanyika sote twajua. Je, katiba hii mpya ambayo sasa tunaita ndani, kuna uhakika gani kwamba mambo haya yatatelezwa? Ni jambo ambalo litiliwe maanani, because tunaweza tukapitisha mambo mazuri lakini isitekelezwe tupigwa na askari tufanyiwe maovu ambayo hayaeleweki. Asanteni (clapping).

Com. Swazuri: Acha huyo mzee halafu yule.

Said Rasi: Mimi kwa jina naitwa Said Rasi kutoka Kikambala sub-location. Ninatoa pongezi zangu kwa katiba hii, kwa sababu nimeona katika ya kingereza na tumeona katiba ya ukoloni na pia tumeona katiba hii ambayo imetutawala kwa miaka arobaini sasa. Tofauti iliyoko ni kwamba, haikutia maanani mambo ya mwananchi. Lakini katiba hii ambayo sasa tunaiendeleza

ukweli kwa hakika itaweza kutusaidia.

Ombi langu kubwa ni kwamba ikiwezekana uchaguzi tunasikia hivi sasa iwe chini ya katiba iliyopo (clapping). Sina mengi ni hayo tu.

Michael Ombati: Mimi naitwa Michael Ombati, mtu wa Kilifi hapa. Ingawa nimechelewa namba thelathini na saba, hapa akina mama na akina watoto. Tuna watoto hapa wote mtu Nairobi unakuta mtu ame-rape mtoto wa miaka mitano na anafunga miaka mitano kwa binadamu ni fair. Wewe ni mwalimu unafundisha mtoto una-rape mtoto wa miaka mitano ni fair korti kule Makadara unafungwa miaka mitano ni kweli? Kama wewe ni binadamu kwa nini huwezi kunyongwa (laughing). Ngoja mwaka sitini na tatu huyu ni mwana America, mtu mweusi ali-rape mke wake yeye alinyongwa na machine. Yeye ali-rape mke wake, kwa nini hapa Kenya mtu ana-rape mtoto wa miaka tano huwezi kunyongwa basi ni hayo tu?

Francis Kaka: Jina langu naitwa Francis Kaka. Mkaaji wa hapa Kilifi, nasema kuhusu title deed. Katika hapa Coast, kuna shida sana na title deed tuna mashamba hatuna title deed na huko hakujaendelea sana kimaendeleo. Watu wa nje wajua wakija huku wanasema watu wa pwani ni wavivu na title deed hakuna tunaletewa mapesa ikiwa ni bank hatuwezi kukopa ikiwa title deed huna utapataje pesa na hata title deed huna? Sasa ile njia ya kupata ile title deed mpaka uende Nairobi tena ujaribu njia nyingi sana, lakini mchezo unaweza kukosa hiyo title deed sasa tunataka ile shida ambayo tunapata kule iletwe hapa ili tuweze kupata title deed kwa njia rahisi ikiwa ni kwenda angalia mwenyewe unakwenda ofisi ya hapo lands kwenda Nairobi huko tikiti huna mwenye pesa ndiye ambaye anakwenda Nairobi kupata title deed lakini ambaye hana kitu hapati. Kwa hivyo hata dakika hii wengi sana hawana ma-title deed hapa ndipo ufara unajaa kabisa hapa wilaya ya Kilifi. Kusema hiyo ukweli.

La pili ni NSSF, hapa shida ni NSSF ukiwa unadai NSSF ni shida kubwa sana huna pesa ya kwenda Nairobi kudai kwa NSSF wewe utakaa mpaka ufe. Na yule mtoto wako ataogopa atasema ikiwa baba mwenyewe ameshindwa kupata zile pesa mimi nitazipata kweli? Zinapotea na kama umefanyia kazi kama ni shirika, serikali kama umefanya bure kwa hivyo nataka shida hiyo iwe unawezeka kurekebisha hapa.

Tatu ni kuhusu tumesema tunaunda katiba mpya na itakuwa nzuri kabisa tunataka tuunde hii katiba iwe kama watu wa nje watu wale ambao hawana kazi kuna hazina fulani ambao watu wa nje utaenda kuta mzungu anababaika hapa vichorocho kuomba. Kuna pesa na hazina fulani wanapatiwa kiwango fulani cha kumwelemisha mtoto wake na hivyo mwenyewe kumaanisha lakini utakwenda shika wacha mzungu anashika tama hana la kufanya. Kwa hivyo tunataka hii katiba ikikuwa itakuwa hii ni muweke hiyo kitu ambacho wananchi wanaweza kusema wanakula matunda ya uhuru. Hakuna saa tumepata uhuru sasa umepata uhuru hata ukaenda kuulizwa shilingi mia tano yenyewe huna. Huo uhuru wako ni sasa unaulizwa umepata uhuru sasa unaweza kutekeleza vipi uhuru umeupata vipi. Ni hayo ningelikuwa nayo nimeandika hapa.

Mwisho ni interview ya walemavu. Utakuta mlemavu ana qualifications za kutosha lakini hapo wakati wa kusimamia kwa

interview anaambiwa wewe usiweze weze hufai maanake mwendo wako si haraka haraka. Huyo ana grade (B) mimi nina grade (A) naambiwa weewe tulia kidogo maanake wewe huwezi kukaa na akili unafanya mikono inafanya kwa hivyo jambo hilo linatatiza sana. Asanteni sana.

Said Akida: Mimi kwa majina naitwa Said Akida. Ningependa kuchangia mambo mawili. Kwanza, ni kuhusu uraia ambao bila shaka ulikuwa unatutuzia sehemu za nyuma. Katika mataifa mengine ni kwamba mtu akifika miaka kumi na minane, anapata kitambulisho na pia anapata passport na ilikuwa hapa kwetu ni shida sana mtu hata akipata akitaka passport kuipata inakuwa ni kazi kubwa. Ikiwezekana katika katiba ya sasa, jambo hilo lirekebishwe, iwe mtu anapopata kitambulisho moja kwa moja anafuutilizia passport yake.

Jambo la pili, ni kuhusu hali ambayo hutokea sana katika mambo ya siasa. Kuna mengine huchaguliwa na baada ya siku fulani mtu mwenyewe amefariki kunatokea by-elections. Mimi ningependelea kwenye katiba mpya chama kitakacho kuwa kimepata ushindi wapatiwe nafasi ya kuchagua mtu wao, nominated members kumaliza kipindi kilichosalia badala ya kwenda by-elections. Elections zinginne zinapoteza ma-billion ya pesa na hali bado ni ile ile. Asanteni. Nomination kutoka kwa chama ambacho kilikuwa kimeshikilia kiti hicho. Asanteni.

Mohammed Hambal: Kwa jina langu naitwa Mohammed Hambal moja tu ya kusema. Kwa upande wa wafanyikazi wapate wa chini. Serikali ile katiba yetu ya zamani. Nazungumzia juu ya wafanyikazi wa mapato ya chini kama wengine wanaofanya vibarua sehemu za Bofa kama Kilifini. Mfano nachukua ya kwamba huwa wanalipwa mapato ya chini na kazi wanafutwa wakati wowote kama ni mzungu hata ukienda kulalamika wale wa wizara ya leo hawatambi wanatambua tu wale wakubwa wakubwa ambao tumbo gunia ile. Lakini sisi wafanyikazi wadogo wadogo tunasahauliwa. Yule mzungu yuko tayari alipe ile pesa ambayo wangukulipa wewe awachage wale wewe ukose hautambuliwi wewe mzalendo hautambuliwi, wanatambua wale wazungu. Hata yule mkubwa akifika pale yule mzungu anamsikilia tumbo namna hii. Kwa hivyo tunaadhirika katiba mpya ya sasa iangalie wafanyikazi wa chini wamesahauliwa. Asanteni.

Com. Swazuri: Mwingine huyu hapa na mwisho kabisa hiyo.

Jones Mwakai: Asante mimi kwa jina naitwa Jones Mwakai. Ningependa kuzungumza habari ya lands board. Chairman hapa katika district awe akichaguliwa. Halafu na kitu kingine ningependa pia cost-sharing katika hospitali iwe abolished. Na kama haitakuwa abolished chairman, members wake wawe ni wananchi ambao watakuwa wanachaguliwa maanake kama sasa huwa hatujui ni wakina nani huwa wanakaeti katika hizo members ama hatujui ni qualifications gani ambazo wanatafuta wakitaka mtu awe member katika board. Asanteni.

Com. Swazuri: Kwanza tutaanza na elimu ya bure. Tumesema kwamba elimu ya bure ni ya watoto wote na sheria tumezweka hapa ambazo zinaenda round kuhakikisha kwamba elimu itakuwa ni ya bure. Tumeandika wazi wazi kabisa kwamba ni jukumu

tumeandika katika children's rights katika education kwamba elimu ni lazima iwe ni ya bure. Na sheria zake tumeziweka kuhakikisha kwamba itakuwa ya bure namna gani. Ile ya secondary, secondary tumesema iwahusishe na tukasema bursaries ndiyo ziwe nyingi pale kwa hivyo elimu itakuwa bure. Na district council, locational council ndiyo itakuwa na jukumu sasa ya kutekeleza vile ulikuwa unasema vifaa, madarasa kila kitu kama ambavyo zamani ulikuwa ukiona.

Zamani ulikuwa ukiona elimu ilikuwa ni Kilifi county council ndiyo, EWD wanashikana nao vitabu vyote, barabara zote, kalamu, chaki ilikuwa mwanafunzi yuwaenda darasani tu ndiyo imerudi hiyo sasa. Halafu vyuo vya uma kila town hii ni kwa sababu ya ile problem ya land grabbing na tumeshaeleza kwamba ardhi zote zitaangaliwa. Zile ambazo zimechukuliwa halafu tena katika land planning tumesema kwamba ni kama hivi town planning ni lazima kana hivyo vyuo vya wananchi vya uma vitakuwa ni lazima kwa district council kutengeneza.

Halafu kuvunja katiba tumeweka sheria hapa inayosema kwamba ikiwa mwananchi yeyote ataona kwamba katiba imevunjwa directly anaenda kortini kushitaki. Hiyo iko katika section three directly kabisa unaenda kushitaki kwamba mimi haki yangu ya kikatiba imevunjwa na fulani na sheria inasema hatua lazima ichukuliwe kaa hiyo sasa si jambo la mzaha sasa kuvunja katiba, na vile ambavyo wananchi wenyewe mara ya kwanza wamehusuka. Sasa ile sote tutakuwa macho na ukiona kwamba umevunjiwa katiba imekuruhusu either uwende kwa public defendor au uka-file case kortini kwenyewe mimi fulani bin fulani nimevunjiwa haki yangu kikatiba ni fulani ni fulani.

Watoto wale ambao ni maskini ambao wamewachwa na wazazi ambao wamekufa na ukimwi nafikiri iko policy ambayo tunatengeneza kuhusu hao watoto wale wanafaa kusaidia hiyo ni kundi kabisa. Elias Kiti ameeleza kuhusu mahakama tumeeleza katika haki za kimsingi hapa, tumesema mahakama zote ni lazima ziwe ni mahakama ambazo makazi yake pale ni makazi ambayo ni ya kibinadamu. Nafikiri hiyo nilikuwa nimeweka mahali maalum huoni vile ambavyo tumetilia mkazo.

Habari ya watu ambao watakuwa wameshikiwa section 70. Mtu yeyote ambaye atakuwa ameshikiwa au amefungwa gerezani either yuko rumande au amefungwa gerezani haki zake tumezinukuu pale ni lazima kwanza awe-treated achukuliwe kwenye njia ya kibinadamu, asibaguliwe, mtu yule asitukanwe. Na wale officers tumeandika hapo na sheria tumesema serikali lazima ihakikishe hiyo inafuatwa apatiwe accommodation facilities, malazi yawe yana-satisfy standards za mwananchi wa kawaida ambatiwe decent clothing, nguo za kisawa sawa sio zile zakupasukwa unasema apalewe malazi mazuri nyumba nzuri sio kwamba awekwe pale ambao pavuja chakula kizuri tumeandika pale afya nzuri na choo kizuri guarantee. Kwa hivyo mahakama lazima zijengwe kivingine sasa I mean hizo prisons zijengwe kwingine.

Pia, anatakikana apewe reasonable health care at public expense ni atibiwe si hiari hiyo ni lazima atibiwe na ikiwa hawana matibabu pale lazima ana haki ya kuita daktari wake ambaye mwenyewe atamulipia, wengine wana madaktari wao persons. Kwa hivyo hawezi ku-treatiwe na mtu mwingine ataruhisiwe daktari aende akamtibu pale. Haya kama ni mtu wa kwenda jogging, exercise atarahusiwa kinafanya exercise, yake kama ni mtu ambaye alikuwa mwenyewe afanye degree yake, au

yuwasoma masomo yake lazima education yake iendelee. Sio kwamba nimefunga mambo yake yote umezifunga tukaandika pia kwamba tu-observe their religion kama ni mwislamu swala tano asikose na ni mfungwa hizo zote tumeziandika kwa hivyo swala la haki za wafungwa sasa limetiliwa mkazo sana.

Na, Amos ukasema kuhusu wale wabunge wanaotaka kugombea kiti lazima wapimwe kwanza hao hiyo hatujiandika lakini tutakwenda kuijadili wapimwe wakionekana wana ukimwi wawe disqualified haya. Askari polisi tumeambiwa kwamba tutahakikisha aje kwamba wanafuata sheria ni kama ndivyo sana polisi kwanza tumewapatia ethics code ile ya kufanya kazi. Halafu pili tumesema tutawa-train sasa professionally tatu tumesema kama hawafanyi kazi yao wananchi wanaushusha kuwashitaki public defender polisi nitawashitaki vile mnataka na ikiwa hawafanyi kazi ile mnataka tumeandika hapa.

Halafu mambo ya ku-spread HIV, huku tunawaruhusu malaya nafikiri tumesema kwamba ingawaje kila mtu ana uhuru wa kufanya anavyotaka lakini isiwe unadhuru wananchi. Uliza basi.

Interjection: Je ...(inaudible)... uwezo wa ...(inaudible)... wajue mfanyakazi wa serikali yeye ...(inaudible)...

Com. Swazuri: Tumesema hiyo tumesema legal aid ni lazima. Kwa hivyo wewe ukishitaki polisi kwanza hutamshitaki kwa polisi mwenzake, tunaondoa hiyo. Kwa sababu ukimshitaki kwa polisi mwenzake tunaondoa hiyo kwa sababu ukimshitaki kwa polisi mwenzake case itaenda hivyo hivyo unavyosema halafu hakuna kitu tumepokea kwa ofisi nyingine.

Section three, inasema kwamba ulikuwa umeuliza habari ya nani atatekeleza tumeshaitaja hiyo. Rapists wauliwe tutakwenda kulijadili hilo title deeds bwana kaka ameuliza title deeds tumesema kwamba katika hii sheria ya lands upatikanaji wa zile documents ziwe rahisi na ndiyo naona tumesema hiyo land commission itakuwa mpaka kule chini kwenye location natumesema kwamba tutapitisha sheria ambayo itahakikisha kwamba mambo ya mashamba inaenda haraka iwezekanavyo na wenyewe wananchi ndiyo wataamua. Mambo ya NSSF tulikuwa tumeshajibu kwamba mipango imefanywa sasa itakuwa rahisi na tutapeleka mashinani.

Social welfare, wale ambao hawana kazi na hawajiwezi kuna section hapa ya social security ukiangalia namba hamsini na sita kila mtu ana haki ya social security. Social security ni kama huko kulishwa na kadhalika including if they are unable to support themselves kama hawawezi kujisaidia wao wenyewe na watu wao, vizazi vyao wapatiwe social security ya kutosha na serikali hiyo tumeshaweka ndani hapa kwa hivyo nikutekeleza tu ndiyo tunangojea.

Na walemavu tushasema kwamba hawatakuwa discriminated kuna section nyingi hapa kuhusu walemavu hakuna kuwapunguwa kuna hivyo kama ana akili zaidi kuliko mtu wa kawaida huyo ataandikwa kazi. Citizenship Said amesema kwamba passport ni shida kupatikana katika kitengo namba kumi na sita tumeandika tukasema kwamba section kumi na sita (a) kila mwananchi wa Kenya raia wa Kenya ana haki ya kupata passport hii tumeandika hapa si fedha tena wala si ihara ni lazima mwananchi wa

Kenya ana haki ya kupata passport na document nyingine yeyote ambayo yaonyesha kwamba ni mwananchi wa Kenya section 16 soma hapo utaona kwamba mbunge akifariki tutafanya nomination bado tumesema kwamba mbunge akifariki tutafanya by-election wananchi wachague tena. Wengine walikuwa wanasema kwamba tuwaweke namba 1,2,3 akifa yule aliyeshinda automatically yule wa pili achukuliwe akifa naye yule wa tatu hasa watauwana hasa tulifikira kwamba hii ni njia rahisi sana.

Ukiona mmeshindwa wamungojea akimaliza mwaka wampiga risasi wajuwa wewe nidyo utakuwako. Kwa hivyo tumesema wakifariki yule bwana tunafuta draft kabisa tunaanza upya wanadhulumiwa tumeaangalia wale wa tumbo gunia tumesema section 53. Huyu wa juu tumeandika hapa ana haki kupata mshahara unaofaa na tukasema kwamba lazima afanye kazi katika mazingira ambayo yanafaa kwa binadamu nimeandika hiyo pia hapo. Kwa hivyo hiyo sio wale matumbo gunia peke yao. Land board chairman awe elected sasa hili ni nyinyi wenyewe sasa hapa mtamua wenyewe lakini inilikaji wa hali ni wenu sas nitaangalia nyingi wenyewe kama mtawachagua, mtawateuwa hiyo mi problem yenu sasa.

Cost-sharing katika hospitali wanasema tu-abolish tumeandika hiyo kwamba inapowezekana mwananchi asikose kupata madawa au tiba ya hospitali kwa sababu hasa pesa hiyo tumeandika mwananchi asikose tiba kwa sababu hana pesa haswa emergency treatment. Mtu amepigwa dafrau pale apelekwa pale halafu daktari aseme mimi simuangalii mpaka atoe pesa huyu hilo sasa tumelifuta atatibiwa kwanza halafu ndiyo maneno yazungumzwe. Nafikiri kwa hayo mengi sana nitakomea hapo. Nawashukuru wote waliofika na kutoa maoni yao lakini kama alivyosema Bwana coordinator huyu si mwisho yeye na kamati yake watapanga mikutano zaidi ya watu ambao tumewapatia hizi nakala wasome zaidi pia wan nafasi tena ya kusema hapana juzi si kusema vizuri lakini naona sehemu hii haiko sawa nataka hivi mpaka turidhike kwamba wananchi wote wameridhika na ile katiba ambayo tutapitisha. Kwa hivyo, tunawashukuru sana nyote mliokuwa hapa kutoka asubuhi mpaka saa hizi.

Interjection: (inaudible) katika katiba hii itakuwaje ikiwa.

Com Swazuri: Sisi kazi yetu mlitutuma ni hii tumefanya na hata sisi maoni yetu ni kwamba tufanye uchaguzi ujao kutumia katiba hii mpya hata sisi. Otherwise, itakuwa haina kazi haina maana kufanya kazi yote hiyo halafu uweke kando ufanya kaa ambaye haina maana hata sisi lakini problem ni kwamba sisi uwezo wa kutengeneza katiba iko nao lakini uwezo wa kuitisha uchaguzi hatuna sisi. Sisi twafuata program yetu mpaka pale ambapo itaishia January tarehe tatu vile tuliambiwa mpaka sasa basi hatujui watasema aje. Lakini, uwezo wa kuwachagua kusema uchaguzi ni siku gani au ni lini sasa huo ni baina ya nyinyi na viongozi wenu sisi hapo kidogo mtatujia radhi maanake tuwatuma sisi tuwafanya kuambiwa fanyeni hivi kachukueni maoni tumechukua andikeni ripoti tumeandika lakini fanyeni uchaguzi hatujaambiwa. Kwa hivyo, hiyo ni kazi yenu wananchi. haya tumeahidi kwamba maombi ya mwisho yatalemewa na mwislamu kwa vile maombi ya mwanzo tumeanza na kikristo kwa hivyo sheikh moja hapa tusomee dua ili tuweze kumaliza mkutano wetu. Haya moja, wengi waislamu hapa haya.

Sasa hilo swala mtu ameuliza nikajibu hapa nimesema kwamba sisi uwezo wa kufanya kazi mlitutuma tumeshatekeleza maoni yetu sisi wenyewe kama tume mtufanye uchaguzi unaokuja kupitia kwa hii kazi ambayo tumeifanya hata kama tutachelewa.

